

## **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA SITA**

**Kikao cha Tisa - Tarehe 21 Juni, 2004**

*(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE (MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):**

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Kuhusu Utekelezaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka 2004/2005.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 79

**Televisheni ya Taifa**

**MHE. NJELU E. M. KASAKA** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 2000 Mheshimiwa Waziri Mkuu alitangaza kuwa ifikapo mwezi Oktoba mwaka huo Televisheni ya Taifa ingeonekana kote nchini na kwa kuwa huu ni mwaka wa tatu bado Televisheni hiyo haionekani zaidi ya Mkoa wa Pwani:-

(a) Je, hali hiyo inamaanisha kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu hakupewa taarifa sahihi?

(b) Je, ni lini sasa Televisheni hiyo itaweza kurusha matangazo yake nchi nzima?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mpango wa kujenga Televisheni ya Taifa umekuwepo kwa muda mrefu, tatizo letu limekuwa ni upatikanaji wa fedha. Serikali ilifanya kila jitihada kutenga fedha katika bajeti ya TTVT, lakini mafanikio hayakuwa makubwa hapo awali. Kiasi kidogo kilichokuwa kinatengwa katika bajeti yetu ndicho kimetufikisha hapa tulipo. Hivyo Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipotoa ahadi alikuwa na taarifa sahihi juu ya Mradi wa TTVT na hali ya upatikanaji fedha ndiyo maana ahadi yake ilitilia maanani hali ya upatikanaji wa fedha wakati huo. Kwa uthibitisho hata katika hotuba yake ya bajeti ya mwaka 2001/2002 ukurasa wa 16 alisema namnukuu : "Kwa upande wa Televisheni ya Taifa, Serikali inatafuta fedha ili kufikisha huduma hiyo nchini kote mapema iwekenavyo."

(b) Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali ya kuharakisha TTVT ionekane nchi nzima bado ipo pale pale. Miogoni mwa jitihada zilizofanywa ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa mtambo wa *satellite (Earth Satellite Up-link)* Desemba, 2003 na kukamilika kwa ujenzi wa vituo vipyta vitatu vya Arusha, Dodoma na Mwanza kwa mwaka huu. Aidha, baadhi ya maeneo ya jirani ya vituo hivi TTVT huwa inaonekana. Serikali tayari imetenga fedha kwa ajili ya kujenga vituo saba vya Tabora, Mbeya, Lindi, Kigoma, Bukoba, Musoma na Tanga. Ujenzi wa vituo hivi saba utaanza mwezi ujao yaani Julai, 2004. Hata hivyo, kwa sasa TTVT inaonekana nchi nzima kwa wale wenye madishi zikiwemo Halmashauri mbalimbali za Wilaya, Miji, Manispaa na watu binafsi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, mpango wa Serikali wa kukamilisha mradi huu ili uonekane nchi nzima kwa haraka kama iwezekanavyo upo pale pale.

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Namshukuru Waziri kwa mujibu mazuri kuhusiana na swalii langu, ninalo swalii moja la nyongeza.

Huo mtambo unaojengwa Mkoani Mbeya pamoja na kwamba TTVT itaanza Julai, 2004, je, baada ya kukamilika itaonekana katika Wilaya zote pamoja na Wilaya ya Chunya? (*Makofii*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI WA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB):** Mheshimiwa Spika, nia yetu ni kujenga mitambo hii katika Makao Makuu ya Mikoa na maeneo yale ambayo baadaye ikaonekana kwamba, TTVT haionekani, tutakuwa na utaratibu wa kuongeza nguvu ili kila eneo lioneckane. Kwa hiyo, Chunya pia kama haitaonekana tutaongeza nguvu ili Chunya ionekane pia. (*Makofii*)

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Naomba niulize swalii la nyongeza kama ifuatavyo: Kwa kuwa katika mpango wa mwanzo na *Hansard* inaonyesha hivyo kwamba, baada ya Mkoaa wa Dar es Salaam utafuata Mkoaa wa Dodoma halafu Mkoaa wa Mbeya.

Ningependa kujua mabadiliko haya ya kupeleka Mikoa ya Mwanza na Arusha yamesababishwa na nini badala ya Mkoaa wa Mbeya? (*Makofii*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI WA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB):** Mheshimiwa Spika, sikumbuki ni *Hansard* ya tarehe ngapi, lakini utaratibu wetu ni kwamba, huu ndiyo utaratibu ambao tumeamua uendelee hatua kwa hatua. Cha muhimu ni TTVT kufika Mbeya na Mbeya sasa hivi inafika. (*Makofii*)

Na. 80

### **Muungano wa Nchi za Afrika Mashariki**

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA (k.n.y. MHE. FRANK G. MAGHOBA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikuwa ni kiungo muhimu sana katika Bara la Afrika na aliyepania kuwaunganisha Waafrika wote kuwa kitu kimoja; na kwa kuwa jambo ambalo kwa kiasi kikubwa alifanikiwa katika Afrika Mashariki ni kuwashawishi Viongozi wenzake wa nchi za Kenya, Uganda na Tanzania kuunganisha nchi hizo tatu ziwe nchi moja:-

(a) Je, ni wapi ambapo Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikwama katika kuunganisha nchi hizo tatu kuwa Taifa moja na aliacha wosia gani kwa Mataifa hayo matatu juu ya kuungana kuwa Taifa moja ikizingatiwa kuwa ni jambo muhimu sana katika kuwakomboa Waafrika wote?

(b) Je, Mheshimiwa Rais, aliyeko madarakani sasa amechukua hatua gani kuhakikisha kuwa, Mataifa yaliyotajwa yanaunganishwa hasa ikitiliwa maanani kuwa ni hivi karibuni Viongozi wa Mataifa hayo waliweka saini makubaliano ya kufanya biashara zao bila ushuru?

(c) Je, isingekuwa vyema viongozi wa nchi hizo wakaamuru Wabunge wao kujadili masuala hayo muhimu kwa faida ya nchi husika na kuangalia faida na hasara tutakazopata tukiungana pamoja na kuwa Taifa moja?

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swal la Mheshimiwa Frank Maghoba, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba, Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alikuwa na nia ya kuanganisha nchi za Afrika Mashariki, wakati nchi hizo zilipokuwa zinapata Uhuru. Kwa ajili hiyo, Baba wa Taifa alikuwa tayari kuahirisha Uhuru wa Tanganyika ili nchi zetu zipate Uhuru wakati mmoja na kuungana. Baada ya kuridhika kuwa nchi za Kenya na Uganda hazikuwa tayari kwa Muungano huo, Mwalimu alifanya mambo mawili. Kwanza, alikamilisha taratibu za Tanganyika kupata Uhuru lakini kuwashawishi Viongozi wenzake wa Kenya na Uganda kwamba, pindi wapatapo Uhuru wa nchi zao, nchi zetu ziungane. Pili, baada ya Mapinduzi Matukufu ya Januari, 12, 1964 huko Zanzibar Mwalimu aliendelea mazungumzo na Rais wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, Mheshimiwa Abeid Amani Karume, kuhusu Zanzibar na Tanganyika kuungana. Matokeo ya mazungumzo na mashauriano hayo ni nchi zetu mbili kuungana na kuzaliwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 26 Aprili, 1964. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kujibu swal la Mheshimiwa Frank Maghoba, Mbunge wa Kigamboni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, bahati mbaya hatukujaliwa kupata maoni ya Baba wa Taifa kuhusu sababu ya nchi za Kenya, Uganda na Tanganyika, wakati ule kushindwa kuungana. Hata hivyo, tunachohisi ni kuwa huenda utashi wa kisiasa haukuwepo. Kuhusu suala la Hayati Mwalimu Nyerere kuacha wosia gani kwa nchi hizo, nalo pia hatuna taarifa yoyote ya kuwepo wosia huo. Hata hivyo, dhamira yake na jitihada zake za kuleta umoja Afrika Mashariki na Afrika nzima, zinazojulikana na sote Afrika Mashariki, naamini hiyo inatosha kuwa wosia wa Baba wa Taifa kwa nchi zetu kuendelea kutafuta umoja na muungano. (*Makofii*)

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu hatua alizochukua Rais aliyekuwepo madarakani yaani Mheshimiwa Benjamin William Mkapa za kusaidia kuleta Muungano wa Afrika Mashariki, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Rais wetu yuko mstari wa mbele kabisa katika kufanikisha jambo hili. Katika Mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki imekubaliwa kuwa, hatima ya ushirikiano wa Afrika Mashariki, nchi zetu kuungana na kuwa Taifa moja litakalojulikana kama Shirikisho la Afrika Mashariki, Rais wetu alishiriki kwa ukamilifu katika kubuni wazo hilo na kufikia uamuzi huo na hivi sasa anashiriki kwa hali na mali na kwa makini kabisa katika utekelezaji wa awamu za mpito kuelekea kwenye shirikisho. (*Makofii*)

(c) Mheshimiwa Spika, Bunge ni chombo huru na Wabunge wana mamlaka kamili ya kuzungumzia jambo lolote lenye maslahi kwa Taifa letu. Hivyo basi, Wabunge hawana lazima ya kusubiri kuamrishwa na Viongozi wa nchi zao kuzungumzia Muungano wa Afrika Mashariki, wanaweza kuzungumzia Shirikisho la Afrika Mashariki na hasa kwa nia ya kuamsha ari ya watu wa Afrika Mashariki kutaka kuungana. Hata hivyo, mjadala rasmi kuhusu kuundwa Shirikisho la Afrika Mashariki utafikishwa kwa wananchi na hapa Bungeni wakati wake utakapowadia. (*Makofi*)

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa historia inaonyesha kuwa ukorofî hata wa kiongozi mmoja tu katika jumuiya yoyote unaweza kupelekea kuvunjika au kutoa matatizo makubwa katika Jumuiya yenyewe. Je, kutohana na uzoefu huo hivi sasa Taifa letu linajiandaa vipi kama pakitokea matatizo yoyote ili tusije tukapata matatizo kama haya yanayojitokeza sasa hivi kuwa mpaka hivi leo hatujaweza hata kulipa madeni ya wastaafu wa Jumuiya iliyokuwa ya Afrika Mashariki? (*Makofi*)

(b) Moja katika kitu muhimu sana katika Jumuiya yoyote ni msimamo wa kiuchumi na kwa sasa inaonekana pana jumuiya mbili (*Zonal Cooperation*) na ninakusudia *SADC* na *COMESA* na wanachama wawili katika Jumuiya hizi mbili, Kenya na Uganda wao ni Wanachama wa *COMESA* lakini sisi tuko *SADC*. Je, hili linawenza likatuunganisha vipi katika suala zima la kufanya biashara katika ukanda huu wa Afrika Mashariki? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, ameuliza kwamba tutazua je Jumuiya kuvunjika kama kuna Kiongozi mkorofî? Mimi nadhani kitu kikubwa ni wapiga kura tu kuwa waangalifu, wasichague Viongozi wakorofî. Bahati nzuri Tanzania tunayo historia hiyo ya kuchagua Viongozi wazuri na wasiwasi huo kwa upande wetu mimi nadhani haupo. (*Makofi/Kicheko*)

Tupo katika jumuiya mbili ni kweli wenzetu wa Kenya na Uganda wako *COMESA* na sisi tuko *SADC* na Jumuiya ya Afrika Mashariki tuichukulie kama vile ndiyo daraja linalounganisha sote. Walioko *SADC* wanaunganishwa na wa *COMESA* kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki, walioko *COMESA* wanaunganishwa na *SADC* kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, ni kiungo kizuri, tukiendeleze. (*Makofi*)

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumwuliza Waziri katika jibu lake la msingi amesema kwamba, suala hilo la Shirikisho la Afrika Mashariki litafikishwa kwa wananchi na hatimaye kwa Mabunge ya nchi hizo, ana maana kutakuwa na kura za maoni (*referendum*) ili kuwaliza watu wa nchi za Afrika Mashariki kama wanaamua kuunda Shirikisho au hapana? Ningependa kuwa na uhakika na hilo.

**WAZIRI WA MAMBO YA NCHI ZA NJE:** Mheshimiwa Spika, katika hatua za kujenga Jumuiya ya Afrika Mashariki tumekubaliana kwamba, tutaanza na Umoja wa

Forodha, ndiyo *entry point*. Baada ya hapo tumesema tutakwenda kwenye soko la pamoja, yaani Umoja wa Forodha pamoja na uhuru wa watu na bidhaa kuweza kuvuka mipaka. Baada ya hapo tumekubaliana hatua itakayofuatia itakuwa ni Umoja wa Sarafu (*Monetary Union*), tutakuwa na sarafu moja na tutawianisha sera zetu za fedha na bajeti. Halafu baada ya hapo ndiyo tutakwenda kwenye hatua ya mwisho kabisa juu ya umoja wa kisiasa ambapo nchi zetu zitaungana na kuwa Taifa moja. Sasa ninaposema kwamba, watu na Mabunge yatahusishwa maana yangu ni kwamba, katika kila hatua kama tulivyofanya huko nyuma wananchi watahusishwa hata itafikia kwenye hatua ambayo ni kubwa tutakopofikia mahali *sovereignties zinapotea, mnazi-merge into one sovereign*, ni jambo kubwa sana.

Sasa hatua ipi itakayotumika kwamba itakuwa ni ya moja kwa moja ya *referendum* ama ni hatua ya kutafuta maoni kwa njia ya nyingine, pengine ni mapema sana kusema. Lakini ninachojua ni kwamba, ni lazima wananchi watahusishwa, siyo kitu ambacho watacaa viongozi peke yao wafanye uamuzi huo. (*Makofi*)

Na. 81

### **Ujenzi wa Barabarani Nchini**

**MHE. MARIA D. WATONDOHA** anauliza:-

Kwa kuwa maendeleo ya nchi nyingi ulimwenguni yametokana na wananchi kuwa na elimu na pia kuwa na mawasiliano mazuri ya barabara ambayo yanawezesha urahisi wa kibashara na hivyo kuinua uchumi; na kwa kuwa Tanzania ni miuongoni mwa nchi za Dunia ya Tatu na uchumi wake ni duni; na kwa kuwa hata Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na mtandao wa barabara nzuri nchini, lakini haina uwezo wa kifedha; je ni lini Serikali itakuwa na mpango mbadala wa kujenga barabara badala ya kutegemea wahisani na fedha ndogo za ndani?

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Maria Watondoha, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Kwanza, napenda nimshukuru Mheshimiwa Maria Watondoha, kwa kuweza kutambua kwamba kukua kwa uchumi na maendeleo ya nchi ye yeyote yanategemea sana kukua kwa mtandao wa barabara na njia nyingine za mawasiliano. Ni dhahiri nchi yetu inahitaji mawasiliano ya uhakika ili kuwezesha uzalishaji na usafirishaji wa mazao pamoja na biashara. Aidha, nchi yetu inahitaji mawasiliano ya barabara ya uhakika ili kuweza kuiunganisha na nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kukua kwa mtandao wa barabara ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa gharama za ujenzi, Serikali inaandaa mpango mbadala wa kushirikisha sekta binafsi na wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi katika ujenzi wa barabara na madaraja kwa kutumia mifumo mbalimbali kama *Build, Operate and*

*Transfer (BOT) na Build, Own, Operate and Transter (BOOT).* Aidha, suala la kushirikisha sekta binafsi katika ujenzi wa barabara limesisitizwa pia katika Sera ya Taifa ya Sekta ya Ujenzi, tunaamini barabara kama vile Mtwara - Masasi Songea - Mbamba Bay, Bagamoyo - Pangani - Tanga, Manyoni - Itigi - Tabora - Kigoma, Daraja la Umoja kati ya Tanzania na Msumbiji na Daraja la Kigamboni na kadhalika, zinaweza kuhusishwa katika Mpango wa BOT na BOOT.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa ujenzi wa barabara unahitaji fedha nyingi, inachukua muda kupata wawekezaji kutoka sekta binafsi ambao wana uwezo huo. Vile vile kuna tatizo la masharti ya wawekezaji ambayo ni ya kibiashara na wakati mwengine hayaendani na matakwa au manufaa ya Taifa. Kwa kuzingatia hili, Serikali imeamua kubuni mpango mbadala, ambao kila mwezi jumla ya shilingi bilioni 1.84 hutengwa kutokana na makusanyo ya ndani ambapo katika kipindi cha miaka mitano jumla ya shilingi 210 bilioni zitakusanya na zitatumika katika ujenzi wa barabara za Singida - Manyoni - Dodoma na Somanga - Matandu, Nangurukuru - Lindi - Mingoyo na kadhalika. Mpango huu ni endelevu na ni wa aina yake katika Afrika. Tunaamini kwa njia hizi nilizositaja, kwa kushirikiana pia na wafadhili mbalimbali, tutawenza kubadili mtandao wa barabara zetu na kuwa wa kiwango cha lami, hali ambayo imeanza kuonekana sasa. (*Makofi*)

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili kama ifuatavyo: Kwa kuwa katika mpango mbadala watakusanya shilingi bilioni 210 na kwa kuwa fedha hizi zitakuwa hususan kwa ajili ya barabara kuu kama alivyozitaja na haziangalii *feeder roads*:-

- (a) Je, hizi *feeder roads* ni lini zitashughulikiwa na kwa mpango gani?
- (b) Kuna maeneo mengine ambayo yanazalisha vizuri sana kama Tarafa ya Milola, ambayo ni wazalishaji wakubwa na wanalisha Mikoa ya Lindi na Mtwara, lakini kwa miaka 40 sasa hawana barabara ya uhakika na wakulima kule wanakwama kuzalisha mazao yao, *feeder roads* kama hizi zitafikiriwa kwa mpango gani? (*Makofi*)

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa hizi shilingi bilioni 210 zitahusisha *trunk roads*, lakini si hizi tu, fedha zinazokusanya na Serikali zitakazohusika katika kutengeneza barabara za Kitaifa kwa sababu kuna fedha nyingi nyingine zikiwa ni pamoja na za wafadhili na fedha zinazotoka kwenye *development program* ambazo zinahusika katika kutengeneza barabara hizo. Sasa kwenye swali lake kwamba hizo *feeder roads* zitashughulikiwaje katika ujenzi wa barabara? Kupitia *Amendment Act* ya mwaka 1998, tulipitisha sheria ya kuanzhishwa *Road Fund*, huu Mfuko huwa zinakusanya shilingi 100 kwa kila lita moja ya mafuta inayokusanya.

Katika bajeti ya mwaka huu tunategemea zitakusanya zaidi ya shilingi bilioni 71.456. Kwa hiyo, hizo fedha kutokana na maamuzi ya Bunge zinatumika kwa ajili ya matengenezo ya barabara tu na katika barabara zinazotengenezwa ni pamoja na *feeder roads, regional roads* na katika mgao wa asilimia 70 zinapelekwa Wizara ya Ujenzi na asilimia 30 zinapelekwa TAMISEMI. Kwa hiyo, ninaamini hii barabara aliyoitaja

ambayo imekaa kwa miaka 40 hajatengenezwa, itahusishwa kutengenezwa kwa kutumia Mfuko wa Fedha za Barabara (*Road Fund*), zinazokusanya kuitia kwenye Wizara inayohusika. (*Makofî*)

Na. 82

### **Ujenzi wa Barabara ya Bunda - Nyamuswa**

**MHE. TEMBE K. NYABURI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilipojibu swali langu Bungeni mwaka 2001 iliahidi kutengeneza kwa kiwango cha changarawe/moramu barabara ya Bunda - Nyamuswa yeye urefu wa km. 25 kabla ya Uchaguzi wa 2005 na kwa kuwa hadi sasa imetengenezwa sehemu ndogo na ambayo pia imeharibika tena kutohana na mvua na sehemu kubwa iliyobaki hajatengenezwa:-

- (a) Je, Serikali imetenga fedha kiasi kwa ajili ya barabara hiyo ili kutimiza ahadi yake ambayo wananchi waliisikia wenyewe kwa masikio yao kuitia Redio Tanzania?
- (b) Kama Serikali haikutenga chochote, je, inawaambia nini wananchi wa Bunda wanaoitumia barabara hiyo?

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tembe Nyaburi, Mbunge wa Bunda, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Nyamuswa - Bunda yeye urefu wa kilometra 24 ni sehemu ya Barabara ya Mkoa ya Nyamuswa hadi Kisorya yeye jumla ya kilometra 108. Wizara ya Ujenzi kuitia Wakala wa Barabara (*TANROAD*) Mkoa wa Mara, imekuwa ikiifanya matengenezo barabara ya Bunda - Nyamuswa ili iendelee kuitika muda wote kama ifuatavyo:-

Katika mwaka wa fedha wa 2001/2002, Wizara ilitumia jumla ya shilingi milioni 6.1 kufanya matengenezo ya sehemu korofi katika kilometra 17 za barabara hiyo, matengenezo ambayo yalihusisha kung'oa mawe, kuchonga barabara, kujenga makalvati na kuweka changarawe. Katika mwaka wa fedha wa 2002/2003, Wizara ilitumia jumla ya shilingi milioni 25 kuifanya matengenezo ya kawaida barabara hiyo, yaliyohusisha uchongaji wa barabara, ung'oaji wa mawe na uwekaji wa changarawe. Katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Wizara imetumia jumla ya shilingi milioni 24 kufanya matengenezo ya sehemu korofi katika kilometra 2.4 za barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambaua umuhimu wa barabara hii kwa maendeleo ya wananchi katika kukuza uchumi wao, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 38 kwa ajili ya matengenezo ya sehemu korofi na ya kawaida ya barabara hiyo ili iendelee kuitika katika kipindi chote cha mwaka. Aidha,

Serikali itaendelea kutenga fedha kupitia Mfuko wa Barabara (*Road Fund*) ili kuhakikisha barabara hii inapitika.

Na. 83

### **Wafanyakazi wa Idara ya Maendeleo ya Jamii**

**MHE. LYDIA T. BOMA** aliuliza:-

Kwa kuwa Idara ya Maendeleo ya Jamii ni nyeti kulingana na umuhimu wake Kitaifa na kazi zao kama hamasa, elimu na kusimamia kazi mbalimbali za ujenzi wa Taifa na yale yanayoweza kuleta athari za kiafya kwa wananchi hasa wale wanaoishi vijijini:-

(a) Je, ni tatizo gani linalowafanya watumishi wa Mikoani na Wilayani wasifanye kazi zao kama ilivyokuwa huko nyuma au kulingana na matarajio ya Taifa?

(b) Je, Serikali inajua kuwa watumishi hao hawana ofisi zinazolingana na hadhi zao pamoja na ukosefu wa vitendea kazi?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** aliujibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Lydia Boma, Mbunge wa Viti maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaamini kwamba, watumishi wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, wanafanya kazi kwa bidii kama ilivyokuwa zamani. Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya kijamii na ya kimfumo yaliyojitokeza, hivi sasa watalaan hao wanakabiliwa na changamoto nyingi zaidi na tofauti ikilinganishwa na kipindi anachozungumzia Mheshimiwa Mbunge. Kazi za Idara ya Maendeleo ya Jamii kwa kipindi tulichonacho zimebadilika na zimeongezeka. Kwa mfano, hivi sasa wana jukumu la kuhamasisha kazi za kawaida za kimaendeleo, wakati huo huo yapo matatizo mengine kama vile magonjwa sugu, mmomonyoko wa maadili, uharibifu wa mazingira, vitendo vya udhalilishaji na mengineyo. Hali hii inatoa changamoto za kipekee ambazo zinaweza kufanya kazi za wataalam hawa hivi sasa zikaonekana kuwa nzito zaidi.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inafahamu kuwa, ofisi za Watumishi wa Idara ya Maendeleo ya Jamii zilizo nyingi zimo kwenye majengo ya Halmashauri. Inawezekana hadhi ya ofisi zao ikatofautiana kulingana na uwezo wa Halmashauri husika. Hata hivyo, pale ambapo kumekuwa na tofauti hizo sababu si kushusha hadhi bali ni uwezo wa Halmashauri husika na Serikali kwa ujumla. Aidha, kwa suala la vitendea kazi ni matumaini ya Serikali kwa kupitia Programu ya Uboreshaji wa Serikali za Mitaa inayolenga kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma, Ofisi za Maendeleo ya Jamii, pamoja

na nyinginezo, zitaboreshwa ili kuweka mazingira mazuri ya kazi katika Halmashauri, ambapo ndipo wanapoajiriwa Watalaam wa Maendeleo ya Jamii. (*Makofit*)

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Kutokana na majibu ya Naibu Waziri, nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa sasa hivi wananchi katika maeneo ambayo nayafahamu kabisa wanauliza Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto iko wapi kwa sababu hii Wizara inawasaidia mambo mengi ya afya, malezi ya watoto, kuhamasisha watu halafu watendaji wanakuja kufanya kazi, kitu ambacho sasa hivi hakuna. Je na hilo Waziri atakataa kuwa halijui?

(b) Kwa kuwa *NGOs* nyingi sasa hivi zimesajiliwa, zile ambazo zilikuwa zinasaidia wananchi maendeleo kwa ujumla na sasa hivi ziko nyingi sana. Je, isingekuwa vizuri hizi *NGOs* zikasajiliwa chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ili zisimamie na kuona haki inatendeka?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lydia Boma, anaulizia masuala ya Idara hii, je, ipo au haipo, maana wananchi wanalamika? Naomba nitoe taarifa kwa Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara hii ipo na itaendelea kuwepo, isipokuwa naomba nitoe taarifa ambayo nimepokea kutoka Ofisi ya *RAS* Mtwara kuhusu Watalaam wa Maendeleo ya Jamii kwenye kata maana wana haki ya kulalamika hao wananchi, lakini wananchi hao hawana Watalaam wa Maendeleo ya Jamii kwenye Kata zao na Vijiji vyao. Mfano mzuri ni huu wa Mkoa Mtwara. Katika Mkoa wa Mtwara kuna idadi ya Kata 107 lakini kata zenye Watalaam wa Maendeleo ya Jamii ni 39 tu, yaani kuna upungufu wa Kata 68. Katika jibu langu la msingi nimesema hao Maofisa Watalaam wa Maendeleo ya Jamii, wanaajiriwa na Halmashauri husika. Kwa hiyo, ninatoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu, nikiwemo na mimi mwenyewe kwamba, pale kwenye Halmashauri zetu tuhakikishe kwamba, Wakurugenzi wanawaajiri hao watalaam ili wafike pale vijijini. Ahsanteni sana. (*Makofit/Kicheko*)

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika, naomba na mimi niulize swali dogo la nyongeza: Kwa kuwa wanawake wengi wako vijijini na Mheshimiwa Waziri anasema kwamba wanaajiriwa na Halmashauri za Wilaya. Je, Mheshimiwa Waziri huoni kwamba Wizara yako inaonekana kwamba haipo, ingekuwa vizuri wewe uisimamie vizuri Wizara hii?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kuna mgawanyo wa kazi na mfumo wa Serikali wa kuendesha Serikali, sasa katika mfumo huo ndivyo tulivyoamua sisi wenyewe kwamba, hawa maafisa katika ngazi ya vijiji waajiriwe na Halmashauri husika. Kwa hiyo, bado natoa wito, sisi kwa sababu tuko pale pamoja na mimi na ni Madiwani, basi tukahakikishe kwamba, Wakurugenzi wetu wanawaajiri hao Watalaam wa Maendeleo ya Jamii katika Kata. Ahsanteni sana. (*Makofit*)

**Mikopo ya Tanzania**

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa kipindi kirefu tangu Uhuru, fedha za mikopo kwa nchi yetu zimekuwa zikiletwa kila mwaka kwa shughuli za maendeleo ya wananchi wetu kwa ajili ya huduma za Afya, Elimu, Maji, Barabara, Umeme na kadhalika:-

(a) Je, Serikali inaweza kuliambia Bunge, ni katika maeneo yapi fedha hizo za mikopo zimekuwa zikitumika zaidi kuliko maeneo mengine?

(b) Je, ni faida zipi zinaweza kuonekana kwa wananchi kutokana na matumizi ya mikopo hiyo?

(c) Je, ni maeneo yapi hayakuonyesha mafanikio na ni kwa sababu zipi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, tangu tupate Uhuru, Serikali imekuwa ikipata kila mwaka fedha za mikopo kutoka vyombo vya fedha vya Kimataifa pamoja na baadhi ya nchi wahisani kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Hii imetokana na uwezo mdogo wa Serikali katika kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kutumia mapato yatowanayo na kodi pamoja na misaada (*grants*) hasa katika maeneo ya kipaumbele yanayolenga katika kuondoa umaskini na kukuza Pato la Taifa kama vile elimu, afya, kilimo, barabara, maji, nishati na mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu huo, Serikali imekuwa ikilazimika kukopa kwa lengo la kuleta maendeleo ya haraka kwa wananchi walio wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo fedha hizo za mikopo zimekuwa zikitumika zaidi kuliko maeneo mengine katika vipindi mbalimbali ni kama nilivyobainisha awali kuwa, Serikali imekuwa ikitoa upendeleo katika sekta za kipaumbele. Baadhi ya sekta zinazohusika ni barabara, kilimo, elimu, afya, maji na nishati.

(b) Mheshimiwa Spika, naamini kuwa, Mheshimiwa Paul Kimiti, atakubaliana nami kuwa, kuna faida nyingi zilizopatikana kutokana na mikopo hiyo, baadhi ya faida hizo ni kuongezeka kwa ajira, hasa katika maeneo ambayo miradi hii ya maendeleo imekuwa ikitekelezwa na hivyo kuwaongezea kipato wananchi wa eneo husika, kuboresha huduma za jamii, kama vile afya, elimu na upatikanaji wa maji safi kwa matumizi ya wananchi na kurahisisha usafiri na usafirishaji wa watu na bidhaa.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa maeneo mengi ya nchi yetu yanafikika bila matatizo kutokana na uboreshwaji wa miundombinu (barabara, reli, usafiri wa majini na angani), hivyo basi, imekuwa rahisi kwa mazao ya wakulima na bidhaa za viwandani kusambazwa kwa watumiaji.

Mheshimiwa Spika, hizo ni baadhi ya faida kati ya nyingi ambazo hata Mheshimiwa Mbunge anaziona katika jimbo lake la uchaguzi. Kwa mfano, ujenzi wa madaraja katika Barabara ya Tunduma - Sumbawanga.

(c) Mheshimiwa Spika, ipo miradi kadhaa ambayo malengo ya mikopo hayakufikiwa kutokana na ufanisi duni wa usimamizi wake. Miradi hiyo ni pamoja na uanzishwaji wa viwanda viliyyolenga kuzalisha hapa nchini bidhaa zilizokuwa zinaagizwa kutoka nje (*Import Substitution Industries*), pamoja na viwanda vyta usindikaji wa mazao ya kilimo kama vile viwanda vyta kubangua korosho. Miradi mingi ya aina hii iliathiriwa na uhaba wa fedha za kigeni kwa ajili ya kuagizia malighafi, zana mbalimbali na vipuri.

Aidha, baadhi ya miradi ya kilimo, hasa ya mashamba makubwa, haikuwa na tija iliyotarajiwa kutokana na uendeshaji usiokidhi mahitaji halisi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kurekebisha hali hii. Hatua hizo ni pamoja na kubinafsisha mashirika haya ili kupunguza mzigo wa Serikali wa kuyahudumia. Aidha, kutokana na sera ya sasa ya Serikali ya kujitoa katika jukumu la kuzalisha bidhaa na kufanya biashara, maeneo haya sasa Serikali haitaendelea kuwekeza isipokuwa kusaidia kuweka mazingira mazuri ya kuwezesha sekta binafsi kushughulikia.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, maswali yafuatayo ningependa nipate maelezo ya kutosha:-

(a) Kwa kuwa suala zima la mikopo linawahu Watanzania wote kwa ujumla na kwa kuwa sisi Wabunge ambao tunatoka sehemu mbalimbali katika nchi hii tunajua matatizo makubwa ya wananchi ambayo wanakabiliwa nayo katika maeneo yao. Je, isingekuwa vizuri kabla ya maamuzi yoyote kuhusiana na mikopo, Waheshimiwa Wabunge tukahusishwa ili tutoe kipaumbele katika maeneo ambayo ni sugu na yana matatizo kwa wananchi wetu? (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Naibu Waziri amekubali ya kwamba yapo matatizo mengi. Je haoni ya kwamba tatizo ambalo linatokana na hali ya mazingira ya mikopo yetu ni kukosekana kwa Sera maalum ambayo inahusiana na mikopo ili Sera itoe maelekezo nini kifanyike, utaratibu upi ufanyike, je, atakubaliana nalo hili kwamba ni vizuri tukawa sasa na Sera Maalum ambayo inahusiana na mikopo ili sisi wote tujue madhumuni na shabaha ya mikopo yetu? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, bila shaka sote tunajua kwamba kazi zetu zimegawanyika katika sehemu tatu. Serikali kama *Executive* ni lazima ihakikishe kwamba, ni hiyo hiyo ndiyo inayochukua dhamana ya mikopo mbalimbali na tunafanya hivyo kwa niaba yenu wote. Mara nyingi miradi ambayo inachukuliwa mikopo nina hakika Wabunge wengi wanaijua, kwa mfano, barabara, Mbunge aliyehusika atakuwa anaelewa mradi na kwamba una manufaa na yote haya yanakwenda kwa mujibu wa *Poverty's Strategy Paper* yetu tunayoitengeneza na haya yamechukuliwa baada ya kufanya utafiti wa kutosha, mahitaji yetu hasa ni yepi katika kuendeleza maendeleo ya nchi yetu.

Lakini kusema kwamba, kumekosekana Sera Maalum ya Mikopo, hilo si sawa, kwa sababu kama nilivyosema, yale yote tunayoyafanya ya maendeleo ni kutokana na utaratibu tuliuweka kwamba, tutasisitiza katika miundombinu, tutasisitiza mambo yale ya ustawi wa jamii, afya, elimu na kilimo, kama nilivyosema hapo mwanzo. Kwa hiyo, kuna mkakati maalum, siyo kwamba hakuna Sera, Sera ipo.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Nashukuru sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa vile majibu ya Naibu Waziri yamekuwa wazi na ameeleza kwamba, mikopo hii ni kwa faida yetu sote wananchi kwa pamoja na nilitegemea kwamba sera ya mgao wa mikopo hii ingelingana ili sote twende sawa, pasiwe na mmoja ambaye anapata zaidi. Ningependa kujua kwamba matatizo tunayoyapata kwa mfano, Mikoa ya Ziwa pamoja na Mwanza ya kuwa na barabara mbaya, ya kuwa na shule chache na huduma chache za jamii inatokana na kwamba mgao unakuwa na sehemu fulani ambazo zinapendelewa? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, bila shaka tumekwishapitisha Bajeti nzima ya Serikali na kwa yale ambayo yatafanywa kwa sehemu mbalimbali na kama alivyoelezea Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi hapo mwanzo, kwa mfano, barabara unayosema ya kwenda Shinyanga - Mwanza baada ya kuona kwamba ile mikopo peke yake haitusaidii, ndiyo mbinu ya kukusanya fedha zetu wenyewe na kuziendeleza barabara hizi kuhakikisha kwamba kuanzia Dar es Salaam mpaka Mwanza barabara inapitika ni kwa kutumia mpango huu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, katika hali ya kawaida ya kukopa na kutumia mikopo, haiwezekani ukaenda Kiwilaya au Kimkoau Kikanda. Kwa mfano, hivi sasa tunavyozungumza, tumekopa fedha kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya Programu ya Elimu ya Sekondari nchi nzima, tumekopa sasa hivi hela kwa ajili ya TANESCO nchi nzima. Lakini kuna mahali tunaweza tukakopa kwa ajili ya Daraja la Mkapa. Ni eneo lile lile la Daraja la Mkapa pale Rufiji, haiwezekani Daraja la Mkapa

ukaligawa likaenda Rombo, likaenda Rufiji, likaenda Mwanza. Kwa hiyo, ndivyo tunavyofanya lakini hatimaye nchi nzima, Taifa zima, litafaidika kutokana na programu au miradi mahususi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa zima au aina fulani katika Taifa.

Na. 85

### **Benki za Biashara za Kigeni**

**MHE. EDSON M. HALINGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Benki nyingi zilizopewa leseni kufanya shughuli za biashara hapa nchini ni za kigeni:-

(a) Je, ni kiasi gani cha faida kila mwaka hubakizwa nchini kwa maendeleo ya Taifa letu?

(b) Je, hesabu zao za mapato na matumizi zinadhibitiwa vipi?

(c) Je, utaratibu wa kutokuwa na Benki ya Taifa yenyе kusimamia uchumi hakutazidi kuifanya fedha yetu ya ndani (shilingi) izidi kushuka thamani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swal la Mheshimiwa Edson Halinga, Mbunge wa Mbozi Mashariki, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwishoni mwa Novemba, 2003, kulikuwa na jumla ya benki ishirini na tatu zilizopewa leseni kufanya biashara hapa nchini na taasisi za fedha nane. Kati ya hizo, benki kumi na nne na taasisi moja zilikuwa za kigeni, zikimiliwi asilimia mia moja na wageni ambapo benki nne zinazosalia ni zile ambazo ndani yake kuna wanahisa Watanzania au Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo mafupi, sasa napenda kujibu swal la Mheshimiwa Edson Halinga, Mbunge wa Mbozi Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, jumla ya faida ambayo imebakizwa nchini (*Retained Earnings*) na mabenki ya kigeni ilikuwa kama ifuatavyo: Kwa mwaka 2000 kulikuwa na faida ya shilingi 42.9 bilioni. Mwaka 2001 kulikuwa na faida ya shilingi 43.8 bilioni. Mwaka 2002 shilingi 50.5 bilioni na kuanzia mwaka 2000 hadi Novemba, 2003 shilingi 59.0 bilioni zilibakizwa nchini. Faida hizo pamoja na mambo mengine, hutumika katika kuongeza mitaji katika benki hizo na kuongeza uwezo wa kutoa mikopo katika sekta mbalimbali za uchumi, kama vile kilimo, ufugaji, madini, usafirishaji, mawasiliano, ujenzi, utalii na kadhalika.

(b) Mheshimiwa Spika, hesabu za mapato na matumizi ya benki zote nchini, pamoja na zile za kigeni, hukaguliwa kila mwaka na Wakaguzi wenyewe uzoefu na utaalamu wa kutosha kwa shughuli hiyo na ambao wameidhinishwa na Benki Kuu ya Tanzania kufanya shughuli hizo za ukaguzi wa mahesabu ya benki na taasisi za fedha. Itakumbukwa kwamba, Benki Kuu imepewa mamlaka ya kusajili na kuidhinisha wakaguzi wa mabenki na taasisi za fedha chini ya kifungu Na. 31 cha Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha (*Banking and Financial Institutions Act, 1991 as amended*) na pia chini ya kifungu Na. 4 cha Mwongozo wa Wakaguzi wa Mahesabu waliosajiliwa na Benki Kuu ya Tanzania (*Independent Auditors Regulations*) ya mwaka 2001.

(c) Mheshimiwa Spika, siyo kweli kwamba, hakuna benki ya Taifa iliyopewa jukumu la kusimamia uchumi wa nchi yetu. Benki Kuu ya Tanzania imepewa dhamana ya kusimamia uchumi wa nchi hii kama inavyoidhinishwa kwenye Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 1995 (*Bank of Tanzania Act, 1995*). Benki Kuu ya Tanzania ilianzishwa kwa madhumuni ya kubuni na kutekeleza sera ya fedha inayodhibiti mfumuko wa bei, kwa lengo la kuleta ongezeko la haraka katika ukuaji wa Pato la Taifa. Hivyo, jukumu mojawapo la Benki Kuu ya Tanzania ni kuishauri Serikali kuhusu mambo ya Uchumi na Fedha, ikiwa ni pamoja na mikakati ya kuimarisha thamani ya fedha yetu.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Fedha ya Benki Kuu hulenga pamoja na kuongeza akiba yetu ya fedha za kigeni, kulinda thamani ya shilingi na kuhakikisha kuwa inaendana na hali halisi ya uchumi. Akiba nzuri ya fedha za kigeni sio tu huongeza imani ya wawekezaji kwa nchi yetu bali pia hutoa kinga dhidi ya kuyumba kwa shilingi katika soko la fedha za kigeni.

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naomba niulize maswali mawili mafupi ya nyongeza. Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba, kuipa mamlaka *NMB* ilipe mishahara ya Serikali, inaiongezea kuwa na amana kubwa ambayo mpaka sasa inaelekea ni zaidi ya milioni 300, lakini haijapewa leseni, je, haoni huku ni kuhatarisha amana za wananchi kukabidhi taasisi ambayo haina leseni ya uhakika kisheria?

Swali la pili, hivi faida inayopatikana na mwekezaji wa nje si inapelekwa kwao, kwa nini tusishawishi wananchi hapa ambao wana uwezo wakaendesha benki hizi au ndiyo kwamba wafanyakazi na wasomi wetu hawana uwezo wa kuendesha benki ndiyo sababu wamenyimwa leseni?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA(MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, hili tumelielezea si mara moja, si mara mbili, *Memorandum of Understanding* waliyopewa *NMB* ni kuwawezesha kwa sababu walikuwa hawajafikia kile kiwango cha akiba inayohitajika kuendesha ile benki kama zilivyo benki nyingine. Huu ni uamuzi uliofanywa kwa makusudi, kuiwezesha hii benki iweze kujiendesha yenye na sasa hivi ndiyo inakwenda. Ni kweli mishahara ya wafanyakazi kupitia *NMB* ni mojawapo ya njia ya kuiwezesha *NMB* ifikie lengo hilo.

Kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi kwamba, faida iliyopatikana kuanzia mwaka 2000 mpaka Novemba, 2003 ni shilingi bilioni 59 ambazo zimesalia hapa hapa nchini. Bila shaka kama nilivyoeleza, baadhi ya mabenki haya fedha zao zote zimetokana na nchi yao. Bila shaka hatutarajii kwamba, mmekuja kufanya biashara hapa kwamba *at least* mllichohuma chenyewe msipeleke nyumbani, lakini kilichobakia bado kinaendelea kuwa uchumi wa nchi hii.

Na. 86

### **Benki ya Dunia Kufadhili Miradi ya Maji**

**MHE. LUCAS L. SELELII** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, Serikali ilisema kuwa Benki ya Dunia imekubali kufadhili miradi ya maji katika Wilaya thelathini na Nzega ikiwemo na kwa kuwa wananchi wapo tayari kuchangia shughuli za maji kama walivyofanya kwenye MMEM. Je, ni lini utekelezaji wa ahadi hiyo utatimizwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Lucas Selelii, Mbunge wa Nzega, kama ifuatavyo:-

Katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara yangu ya mwaka 2003/2004, nilitoa taarifa kuwa, Benki ya Dunia imekubali kufadhili miradi ya maji katika Wilaya 38 zaidi ikiwemo Wilaya ya Nzega na hivyo kufanya jumla ya Wilaya zitakazotekeleza Mradi huo kufikia 50.

Mheshimiwa Spika, baada ya makubaliano ya Serikali na Benki ya Dunia, Wizara yangu imekuwa ikiendelea na maandalizi ya kuanza utekelezaji wa Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijiini. Maandalizi hayo yanahusu uandaaji wa takwimu sahihi, uhamasishaji wa wananchi ili waweze kuchangia sehemu ya gharama za ujenzi wa miradi na kuwaandaa Viongozi wa Wilaya husika kuhusu usimamizi na uendeshaji wa programu hiyo. Wizara yangu imekwishafanya mawasiliano na Wilaya zote 38 kuhusu maandalizi yanayohitajika. Wilaya ya Nzega imeshirikishwa kikamilifu katika maandalizi hayo na tayari wanajiandaa kwa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, tangazo la kupata wahandisi washauri na mashirika yasiyokuwa ya Serikali kwa ajili ya usanifu wa miradi na uwezeshejaji wa wananchi wakati wa utekelezaji wa programu hiyo, lilikwishatolewa kwenye magazeti mwezi Juni, 2004 na taratibu zingine za kuwapata makandarasi hao zinaendelea. Utekelezaji wa programu utaanza katika kipindi hiki cha fedha tunachokipitisha hapa kwenye Bunge lako Tukufu. Hivyo, ahadi ya Serikali itakuwa imeanza kutekelezwa.

Namshauri Mheshimiwa Mbunge, aendelee kuhamasisha wananchi wa Wilaya ya Nzega ili wawe tayari kushiriki kikamilifu kwenye utekelezaji wa programu mara itakapoanza. Uhamasishaji huo pamoja na mambo mengine, ni uanzishwaji wa akaunti za watumiaji maji katika ngazi za vijiji.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Majibu ya Mheshimiwa Waziri ni sahihi na wananchi wako tayari, wameshajiandaa wanangojea. Je, Wizara ina mikakati gani wa kuhakikisha utekelezaji huu unakuwa wa haraka zaidi ili kukabiliana na ukame ambao umeikumba nchi nzima pamoja na ukosefu wa maji?

Swali la pili, kwa kuwa Mji wa Nzega utakuwa Mji Mdogo kuanzia Julai, 2004 na ambapo Mji wa Nzega umefanikisha mradi mkubwa wa maji safi na salama na kuwa baadhi ya vijiji ambavyo tungevielekeza katika mradi huu wa Benki ya Dunia vitaingia katika Mji wa Nzega. Je, Wizara ipo tayari kushirikisha Mamlaka ya Maji au Bodi ya Maji ya Nzega katika Mradi huu wa Benki ya Dunia ili kuvikamilisha vijiji ambavyo vitaingia katika Mji Mdogo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi, programu hii inatarajiwa kuanza katika mwaka huu wa fedha na matayarisho yameshaanza kama nilivyoeleza. Hivyo, napenda tu nirudie wito wangu kwa kumwomba Mheshimiwa Mbunge, aendelee kuhamasisha kama alivyosema na kama tunavyofahamu jitihada zake, ahamasishe wananchi ili kuwe na *account* ili miradi itakapokuwa tayari kuanza waweze kuanza mara moja.

La pili, kuhusu kuhusishwa kwa vijiji vilivyo kando kando ya Mji Mdogo wa Nzega, sioni tatizo kwa sababu programu ya miradi inayohusishwa katika programu hii ya maji na usafi wa mazingira vijijini inahusisha wadau. Hivyo, miradi wanayochagua wananchi ndiyo miradi ambayo itatekelezwa na ninapenda niongeze tu kidogo kusema kwamba, mafunzo tuliyoyapata kwenye programu katika Wilaya 12 imeonyesha kwamba, kunakuwepo wakati mwingine kidogo kutokuwa na uchangamfu wa kutumia hizo fedha na tunaangalia uwezekano sasa hivi wa fedha hizo kutumika kwa yeote na Wilaya yoyote itakayokuwa tayari ili kuhamasisha ushindani ili programu hii iende haraka.

Na. 87

#### **Ulipaji wa Ankara za Maji - Kwa Taasisi Mbalimbali**

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA (k.n.y. MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO)** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na matatizo makubwa ya ucheleweshaji wa ulipaji wa ankara za maji kwa Mamlaka za Maji Safi/Taka nchini kutoka kwenye Taasisi mbalimbali za Serikali licha ya kwamba ankara hizo zimehakikiwa na Taasisi husika kwa mfano, Mamlaka ya Maji Safi/Taka Mjini Tabora (*TUWASA*) hadi kufikia Machi, 2004

ilikuwa inaidai JWTZ shilingi 302,299,494/10, Polisi shilingi 59,128,364.00 na Magereza shilingi 14,594,491.00, Shule za Sekondari na Vyuo shilingi 43,357,152.00:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani mahususi ya kuzisaidia Mamlaka kulipa fedha zao mapema?

(b) Je, *TUWASA* italipwa lini fedha inazodai kutoka kwenye Taasisi za Serikali nilizozitaja?

#### **NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swal la Mheshimiwa Prof. Henry Mgombelo, Mbunge wa Tabora Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba, Taasisi mbalimbali za Serikali zimekuwa zikichelewa au kutolipa kwa muda mrefu gharama zao za matumizi ya maji na hivyo kusababisha ulimbikizaji wa madeni makubwa ya maji ambayo yanatishia kuzorota kwa huduma hii muhimu. Kwa mfano, Taasisi za Jeshi, Polisi na Magereza, ambazo zinatumia maji kwa wingi, zinaongoza kwa kuwa na madeni makubwa yanayofikia jumla ya shilingi milioni 772.4 kwa nchi nzima.

Kuanzia mwaka 2002/2003, Serikali kupitia Wizara ya Fedha, imekuwa na utaratibu maalumu wa kulipia huduma (*Utilities*) ikiwa ni pamoja na maji, umeme na simu kwa kutumia vifungu maalum vinavyodhibitiwa moja kwa moja na Hazina. Lengo la utaratibu huu ni kuhakikisha kuwa, fedha zilizotengwa kwa ajili ya huduma hizi hazitumiki kwa shughuli nyingine.

(b) Kuhusu madeni yanayodaiwa na *TUWASA* kwenye Taasisi alizozitaja Mheshimiwa Mbunge, *TUWASA* na Wizara yangu, zinaendelea kufuatilia kwa karibu ulipaji wa madeni hayo. Tayari Wizara ya Elimu imelipa shilingi milioni 26 kati ya milioni 43, zilizokuwa zinadaiwa kutoka Shule za Sekondari na Vyuo. Tatizo lililojiteza katika ufuatiliaji huo ni kwamba, Taasisi husika hazikutenga fedha za kutosha mwaka 2003/2004, kwa ajili ya kulipa deni hilo pamoja na kulipia gharama za matumizi ya sasa (*Current Bills*). Makao Makuu ya Magereza wameahidi kutenga fedha kwenye bajeti ya mwaka huu tunaouanza (2004/2005), JWTZ wameahidi kulipa shilingi milioni 26.9 kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha (2003/2004) na Polisi hadi sasa hawajatoa utaratibu wao wa kulipa. Kwa hali hii deni lililobaki itabidi liendelee kulipwa mwaka wa fedha unaofuata. *TUWASA* inaendelea kuwasiliana na Taasisi hizo kuhusu utaratibu wa kulipa madeni yaliyobaki.

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri maswali mawili ya nyongeza. Kwa kutumia mfano wa *Net Group Solution* ambao wanaongoza *TANESCO*, wao baada ya kukabidhiwa lile Shirika walifanya kazi moja kubwa sana ya kukusanya madeni na walifanikiwa kwa kiwango kikubwa kwa sababu hawakuingiliwa kabisa pale walipotekeleza majukumu yao ikiwa ni pamoja kukata huduma kwa ambaye hakulipa bili zake.

Je, Serikali inaweza ikatoa tamko rasmi hapa kwamba, watamlinda huyu Mtendaji Mkuu pamoja na watu wake endapo wataamua kufanya hivyo, kwa sababu taasisi zinazoguswa ni nyeti vile vile?

Pili, katika jibu lake la msingi Mheshimiwa Waziri amesema kuna vifungu maalum ambavyo vinatengwa kwa ajili ya kulipia *utilities*, sasa inaelekea hawa hawatumii jinsi ambavyo wanaagizwa. Sijui Serikali inawachukulia hatua gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli *Net Group Solution* walipochukua *TANESCO* kulikuwepo na hamasa kubwa ya wananchi hasa Taasisi kulipa madeni yaliyolimbikizwa. Lakini hii haina maana kwamba, inazuia Mamlaka ya Maji Tabora kudai kwa kutumia njia zile zile, kwa bahati mbaya sana kumekuwepo na *perception* ya Mameneja wetu kuwa na *self sensorship*, kitu ambacho nadhani kinatokana na historia tulikotoka. Lakini sijawahi kuona Meneja ambaye amechukuliwa hatua kwa kukata huduma hiyo ya maji kwa Taasisi ambayo hailipi madeni na ushahidi wakiwa nao na ninapenda kutoa rai kwamba, wanaodaiwa walipe, la sivyo hatua zinazostahili zitachukuliwa.

Kuhusu Wizara au Taasisi au Idara zinazotengewa mafungu kutokulipa madeni yake au kutumia fedha hizo kwa matumizi mengine badala ya kulipa madeni, ninapenda ieleweke kwamba, mara nyingine hawafanyi makusudi, ni fedha zinavyotoka Hazina ukilinganisha na upatikanaji wa fedha. Kwa hiyo, pia wana matatizo ya kimsingi na kuna wachache ambao wanafanya hayo makosa ya kutumia fedha zilizotengwa kwa mafungu mengine lakini utaratibu wa Hazina uliopo sasa hivi uko *strict* sana kiasi kwamba, itakuwa ni vigumu sana kuhamisha fungu lililokuwa *approved* na Bunge kwa matumizi ya aina hii kuyapeleka sehemu nyingine.

Na. 88

### **Usumbuu wa Wasafiri Lango Kuu TRC Dar es Salaam**

**MHE. ESHA H. STIMA** aliuliza:-

Kwa kuwa wasafiri wengi kwa njia ya treni husumbuliwa sana na watumishi wa *TRC* kwenye lango kuu la Dar es Salaam, hasa wakati wa kuingia kwa abiria wenywewe na mizigo yao kwa madai ya kupimwa kwa mizigo yao na kulipia na kwa kuwa sehemu ya kupimia mizigo ni mbali na lango kuu la kupitia abiria:-

- (a) Je, *TRC* itabainisha lini kilo zinazosafirishwa bure na abiria kama yanavyofanya mashirika ya ndege nchini kwa daraja zote za treni?
- (b) Je, Shirika hilo halioni kuwa sasa ni wakati muafaka kuweka mizani miwili kwenye lango kuu ili wasafiri waweze kupima na kulipia kilo za mizigo yao inayozidi kwa misingi ya kupunguza manung'uniko ya abiria na kuongeza kipato cha Shirika kwa njia ya halali?

## **WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esha Hassan Stima, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Shirika la Reli Tanzania, tayari limebainisha uzito wa mizigo inayoweza kusafirishwa bure na abiria kwa madaraja yote ya treni za Shirika la Reli kama ifuatavyo: Abiria daraja la kwanza kilo 70, abiria daraja la pili kilo 40 na abiria daraja la tatu kilo 20.

Mizigo/vifurushi vinavyoruhusiwa kwenye kila daraja ni vile ambavyo ni muhimu kwa safari ya abiria kwa mfano, sanduku la kawaida, kikapu au mkoba, magazeti au vitabu vya kuvisomea, kiti cha mlemavu na mwamvuli.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda kumjulisha Mheshimiwa Esha Stima kuwa, Shirika la Reli sasa limeweka mizani karibu na lango kuu la kuingilia Stesheni ya Dar es Salaam ili kuwezesha wasafiri kupima na kulipia uzito unaozidi kwa nia ya kupunguza msongamano ndani ya mabehewa na usumbufu kwa abiria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru Mheshimiwa Esha Stima, kwa kubaini na kusema kero zinazowasibu watumiaji wa huduma za reli. Tutaendelea kupokea na kuyafanya kazi malalamiko, maoni na ushauri kuhusu Shirika la Reli kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na kuititia masanduku ya maoni, barua za wasomaji katika magazeti na malalamiko yanayotolewa moja kwa moja.

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, sijui kama Mheshimiwa Waziri anatambua kwamba hivi sasa lango kuu haliruhusu abiria kusindikizwa na ndugu zao kuingia na mizigo katika eneo husika na hii husababisha hasara kwa abiria kwa sababu inalazimika watumishi wale wale wa Shirika la Reli kulipwa pesa kusafirisha mizigo kuingia ndani. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba imefika wakati sasa kuweka utaratibu wa vitoroli vya kutosha ili abiria waweze kubeba mizigo yao wao wenyewe kama linavyofanya Shirika la Ndege pale Dar es Salaam? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli haturuhusu wasindikizaji kusindikiza wasafiri. Tatizo tulilolipata ni kwamba, watu wenye nia mbaya walikuwa wanakata tiketi za kusindikiza halafu wao wenyewe wanasafiri bila malipo, ilikuwa shida sana kuwadhibiti. Hata hivyo, tutajitahidi kufuata mtindo wanaotumia viwanja vya ndege ili kusaidia wenye vifurushi kubebewa vifurushi vyao kwa magari maalum. Napenda kumhakikisha Mheshimiwa Esha Stima kwamba, jana (20 Juni, 2004), mimi mwenyewe ili kuweza kujibu swali hili kwa uhakika, saa sita na dakika tano, nilipita pale *station* kuhakikisha kwamba kunakuwa na mtindo bora wa kusimamia suala hili, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha. Kwa leo kuna kikao kimoja cha Kamati nayo ni Kamati ya Fedha na Uchumi, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Njelu Kasaka, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane saa tano asubuhi hii katika chumba cha mikutano ya Kamati Na.232.

Waheshimiwa Wabunge, leo tunaanza mjadala wa Hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Hadi sasa tumeshapata maombi ya kuchangia kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge 55. Nikumbushe tu utaratibu wetu wa kawaida kwamba, kwa kuwa mjadala wa Ofisi ya Waziri Mkuu vile vile ni mjadala kuhusu Serikali kwa ujumla, kama ilivyokuwa wakati wa Bajeti kwa hiyo wale waliochangia katika Hotuba ya Bajeti watawekwa mwisho, wale ambao hawajachangia ndio watapewa nafasi ya kwanza. (*Makofii*)

Mwisho wa matangazo, tunaendelea na *Order Paper*, Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2004/2005 Ofisi ya Waziri Mkuu**

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, iliyochambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge lako sasa lipokee na kujadili mapitio ya utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka 2003/2004 na mwelekeo wa kazi za Serikali kwa mwaka 2004/2005. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake na yale ya Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, wakati Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge unaanza, ndugu zetu, Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Omar Kigoda, walifiwa na baba yao mzazi. Napenda kuwapa pole na kuiombea roho ya Marehemu ipumzike mahali pema peponi, *amin*.

Aidha, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, alivamiwa na majambazi katika Kijiji cha Maseyu Mkoani Morogoro. Majambazi hayo yalipora mali na kujueruhi vijana wawili ambapo yeeye alinusurika bila kuumizwa. Napenda kumpa pole Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na pia Mheshimiwa John Samwel Malecela, kwa mkasa huo uliompata mke wake.

Vilevile Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, alipata ajali ya gari na kuumia na hivi sasa amelazwa hospitalini. Mheshimiwa Estherina Kilasi, naye alipata ajali ya gari. Napenda kuwapa hao wote pole na kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu wapone haraka.

Mheshimiwa Spika, tarehe 30 Mei, 2004, nchi yetu ilifanya chaguzi ndogo kwa ngazi ya Madiwani katika Kata 19 nchini na ngazi ya Ubunge katika Jimbo la Bariadi Mashariki. Matokeo ya chaguzi hizo ni kuwa, Chama cha Mapinduzi kilishinda kwa

kishindo katika Jimbo la Bariadi Mashariki, ambapo Mheshimiwa Danhi Makanga, alichaguliwa kuwa Mbunge. Hongera sana CCM na hongera sana Mheshimiwa Danhi Makanga. (*Makofî*)

Kwa upande wa Madiwani, CCM pia ilishinda kwa kishindo kwa kupata viti 16 kati ya 19 vilivyogombewa nchini. Hongereni sana Madiwani mlioshinda na hongera sana CCM, hasa ukizingatia kuwa vingi ya viti hivyo vilikuwa vikishikiliwa na Vyama vyta Upinzani. Nawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge, waliopata nyadhifa mbalimbali za uwakilishi katika vyombo mbalimbali vya Kitaifa na Kimataifa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda niwapongeze kwa dhati Mheshimiwa Dr. Abdallah Omari Kigoda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Waziri wa Fedha, kwa hotuba zao kuhusu Hali ya Uchumi nchini na Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2004/2005. Ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yao mizuri wakati wa kujadili hotuba hizo na hatimaye kukubali kupitisha Bajeti ya Serikali. Serikali itazingatia ushauri wao katika utekelezaji wa Bajeti hiyo.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kuishukuru Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge lako Tukufu, kwa kuchambua Bajeti na Mpango wa Maendeleo wa Serikali wa mwaka 2004/2005 na kuishauri Serikali ipasavyo. Aidha, nawashukuru wadau wote ambao wametoa michango yao ya mawazo katika hatua mbalimbali za utayarishaji wa Bajeti na Mpango huo. Nazishukuru Kamati za Kudumu za Bunge lako Tukufu, kwa kupitia makadirio ya matumizi ya kila Wizara, Ofisi na Idara za Serikali zinazojitegemea na kwa ushauri uliotolewa. Kwa namna ya pekee, napenda niishukuru Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya uongozi shupavu wa Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe, kwa kupitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla nchi yetu imeendelea kuwa na amani na utulivu. Tarehe 26 Aprili, 2004, tulisherehekea miaka 40 ya Muungano. Muungano wetu ndiyo chimbuko na mhimili wa umoja, mshikamano, upendo, amani na ushirikiano tulio nao nchini mwetu. Haya ni matokeo ya juhudhi kubwa zilizofanywa na Waasisi wa Muungano, Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume, ambao ujasiri wao ndio uliowezesha kuanzishwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, wapo baadhi ya watu wanaokerwa na Muungano huo. Wanajitahidi kutumia hila mbalimbali kutaka kuutia dosari kwa malengo yao binafsi. Napenda kuwashakikishia wananchi kuwa, Muungano hauwezi kutetereka kamwe. Changamoto iliyo mbele yetu ni kuimarisha misingi imara iliyowekwa na Waasisi wetu na kuutetea Muungano wetu dhidi ya maadui. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilisimamia uchaguzi mdogo wa Jimbo la Bariadi Mashariki na chaguzi ndogo za Madiwani katika Kata 60 katika Mikoa mbalimbali. Katika Jimbo la Bariadi Mashariki, vyama vyta CCM na UDP vilishiriki. Kama nilivyoeleza awali, mgombea wa CCM, Mheshimiwa Danhi

Makanga, aliibuka mshindi kwa kumshinda mgombea wa *UDP* na Mwenyekiti wa Taifa wa Chama hicho, Mheshimiwa John Momose Cheyo. (*Makofit*)

Vilevile, chaguzi ndogo za Madiwani zilifanyika Januari 11, 2004 na Mei 30, 2004 na kuhusisha Vyama vya CCM, *CUF*, *UDP*, *TLP*, *NCCR-MAGEUZI*, *CHAUSTA*, *PPT-MAENDELEO*, *TADEA*, CHADEMA na *DP*. Matokeo ya chaguzi hizo ni kuwa CCM ilipata viti vya Madiwani 55, *TLP* 1, *CUF* 1, CHADEMA 2 na *UDP* 1. Navipongeza Vyama vyote vilivyoshiriki chaguzi hizo na zaidi vile vilivyoshinda. Kwa namna ya pekee nkipongeza sana Chama cha Mapinduzi kwa kushinda kwa asilimia 100 katika nafasi ya Ubunge na asilimia 91.7 katika nafasi ya Udiwani. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeendelea vizuri na shughuli zake za maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa 2005. Maandalizi ya wakati huu ni makubwa zaidi kwa sababu Tume inakabiliwa na maandalizi ya Daftari la Wapiga Kura, jambo ambalo ni geni na la gharama kubwa. Daftari hilo linakisiwa kugharimu kama shilingi 30 bilioni. Daftari hilo ni muhimu sana kuziba mianya inayoweza kutumika kwa urahisi kufanya vitendo vya udanganyifu wakati wa upigaji wa kura. Hivi sasa Tume kwa kushirikiana na wadau wengine, inaendelea na hatua mbalimbali za uanzishaji wa Daftari hilo. Hata hivyo, kila mdau hana budi kutambua kuwa utekelezaji wa Sheria ya Uchaguzi na uanzishaji wa Daftari la Wapiga Kura unafanyika kwa mujibu wa Katiba ya Nchi yetu. Naviomba Vyama vyote vya Siasa, vitoelimu kuhusu umuhimu wa Daftari hilo kwa wanachama wao. Nawaomba Watanzania wote wafahamu haki na wajibu wao katika suala la upigaji kura ili wasiyumbishwe. Napenda kuwahimiza wote wenye umri wa kupiga kura wajandikishe kwa wakati muafaka ili wasipoteze haki yao ya kupiga kura kuchagua viongozi wao. Aidha, nawatahadharisha wale wote wanaotaka kutumia visingizio vya uchaguzi huo kuvuruga amani kuwa hawatavumiliwa hata kidogo. Vyama vya Siasa na wanachama wao wanahimizwa kufanya shughuli zao za kisiasa kwa kufuata sheria, kanuni na maadili ya jamii. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, idadi ya Vyama vya Siasa vyenye usajili wa kudumu imeendelea kuwa 16 kama mwaka uliopita. Vyama viwili vya Siasa, SAFINA na Harakati za Mabadiliko Sahihi (HAMASA), vilivyokuwa vimepata usajili wa muda, vimefutwa baada ya kushindwa kutimiza masharti kwa mujibu wa Sheria. Katika mwaka 2003/2004, mazingira ya kazi katika Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Dar es Salaam na Ofisi Ndogo Zanzibar yameboreshwa. Kufunguliwa kwa Ofisi Ndogo Zanzibar kumeweza kutolewa kwa huduma za usajili wa Vyama vya Siasa kwa karibu zaidi kwa Watanzania walioko Visiwani. Aidha, Mheshimiwa Rais alimteua Bwana Rajab Baraka Juma kuwa Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa nchini. Ni matarajio yetu kuwa, uteuzi huo utaimarisha utendaji katika ofisi hiyo. Nachukua nafasi hii kumpongeza Bwana Rajabu Baraka Juma, kwa uteuzi huo. (*Makofit*)

Katika mwaka 2004/2005, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa itaendelea kutekeleza majukumu yake ya usajili pamoja na utoaji wa mafunzo kwa viongozi na watendaji wa Vyama vya Siasa nchini ambayo ni muhimu hasa katika kipindi cha kuelekea Uchaguzi Mkuu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, Bunge lako Tukufu limeendelea kutekeleza barabara majukumu yake ya Kikatiba. Bunge lilifanya mikutano minne ambapo shughuli za kutunga sheria, kuridhia Mikataba ya Kitaifa na Kimataifa, kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Serikali na kuihoji Serikali kuhusu utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya wananchi ilitekelezwa. Bunge pia lilipitisha Miswada ya Sheria 23, liliridhia Mikataba 19 ya Kitaifa na Kimataifa na maswali 837 ya msingi na mengine mengi ya ziada yaliyoulizwa na Waheshimiwa Wabunge, yaliyibiwa na Serikali. Vilevile, Serikali ilipokea na kushughulikia ushauri na mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati za Kudumu za Bunge ambazo pia zilipitia Makadirio ya Matumizi ya kila Wizara kwa mwaka 2003/2004. Taarifa ya Utekelezaji wa Ahadi za Serikali zilizotolewa Bungeni katika mwaka 2003/2004, zitawasilishwa katika Mkutano huu wa Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Ofisi ya Bunge itaendelea kutekeleza mipango ya kuimarisha shughuli za Bunge ikiwa ni pamoja na kuongeza elimu ya Kibunge na mafunzo kwa Watendaji, kuimarisha mahusiano na Mabunge ya nchi rafiki na kuboresha huduma za kiutawala. Aidha, baada ya kukamilika kwa ukarabati wa Ofisi Ndogo ya Bunge Dar es Salaam na hatua mbalimbali za ujenzi wa Ofisi ya Bunge Zanzibar, Serikali itaendelea na maandalizi ya ujenzi wa Ukumbi mpya wa kisasa Mjini Dodoma, ili kukidhi pamoja na mahitaji mengine, matarajio ya ongezeko la Wabunge baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005. Vilevile, Ofisi za Waheshimiwa Wabunge Majimboni zitaendelea kuimarishwa hatua kwa hatua kwa kuendelea kutenga fedha katika bajeti kupitia mamlaka za Mikoa husika. Hivyo, Wilaya zote zihakikishe zinatenga katika bajeti zao fedha za kuimarisha ofisi hizo. Naomba Waheshimiwa Wabunge, tushirikiane na mamlaka hizo kuona jambo hilo linatekelezwa kikamilifu hasa wakati wa kupitisha bajeti zetu katika Vikao vya Halmashauri na katika Kamati za Ushauri za Mikoa. Aidha, kwa Majimbo ya Tanzania Zanzibar, Ofisi ya Waziri Mkuu inawasiliana na Ofisi ya Waziri Kiongozi kuhusu uimarishaji wa ofisi hizo.

Mheshimiwa Spika, hali ya usalama ndani ya nchi ni shwari ingawa vitendo vya uhalifu viliendelea kujitokeza. Uhalifu uliojitokeza nchini unatokana na sababu mbalimbali zikiwemo imani za kishirikina, ulipizaji visasi na uingiaji haramu wa wageni, baadhi yao wakiwa na silaha. Aidha, hivi karibuni yamekuwepo matukio machache, hususan Visiwani Zanzibar ya ulipuaji wa mabomu na uchomaji moto wa mali na majengo yakiwemo ya Viongozi wa Serikali na wa dini. Hali ya ulinzi katika mipaka yetu imeendelea kuwa shwari katika maeneo mengi isipokuwa mpaka wa Magharibi, yaani kwenye Mikoa ya Kigoma, Kagera na Rukwa. Mikoa hiyo iliendelea kushuhudia vitendo vya ujambazi wa kutumia silaha, utekaji nyara wa wananchi, wizi wa mifugo, uporaji wa mali za wananchi na hasa boti za kuvulia samaki katika Ziwa Tanganyika. Serikali inaendelea kudhibiti vitendo hivyo katika maeneo yote ya mipaka. Aidha, bado tunalo tatizo kubwa la wakimbizi nchini. Nawaomba wananchi wasiwhafadhi wakimbizi katika nyumba zao kwa visingizio vya kupata vibarua rahisi kwani kufanya hivyo ni kosa la jinai. Kisheria wakimbizi wote wanatakiwa kukaa makambini. Ninawaomba wananchi wawe na moyo wa uzalendo na washirikiane na Serikali kufichua wahalifu wa aina zote.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na mpango wa kuimarisha vyombo vya ulinzi na usalama ili viendelee kutekeleza kwa ufanisi zaidi majukumu yao ya msingi.

Baadhi ya hatua zilizochukuliwa ni pamoja na ujenzi wa makazi ya Askari, ukarabati wa nyumba na majengo katika kambi mbalimbali na kuyawezesha Majeshi kimafunzo, kivifaa na kuyapatia maeneo ya kutosha kuendesha shughuli zake. Hata hivyo, kutokana na hali halisi ya shughuli za Kijeshi, maeneo yanayohitajika ni makubwa na wakati mwingine huonekana na raia kuwa ni maeneo ya wazi. Hali hiyo imesababisha uvamizi wa baadhi ya maeneo ya Majeshi na hatimaye kuwa chimbuko la migogoro kati ya Wanajeshi na raia. Ili kuondoa migogoro hiyo, Serikali inaendelea na upimaji wa maeneo ya Majeshi kwa kuweka alama za mipaka ili kuyatofautisha na maeneo ya raia.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), vijana wa "Operesheni Mkapa" walimaliza rasmi awamu ya kwanza ya mkataba wa miaka miwili wa mafunzo mwezi Oktoba, 2003. Mafunzo hayo yaliendeshwa kwa ufanisi na mafanikio makubwa ambapo takriban vijana 1,834 walipata nafasi za ajira katika vyombo vya ulinzi na usalama na mashirika mengine mbalimbali. Vijana wengine wapya wapatao 2,000 wameanza kupokelewa katika Kambi mbalimbali kwa ajili ya kuanza mafunzo mwezi Juni, 2004. Juhudi za kuboresha Kambi za JKT ikiwa ni pamoja na kukarabati karakana zimeendelea kwa lengo la kuongeza uwezo wa kupokea vijana wengi zaidi na kuimarisha uendeshaji mafunzo mbalimbali hasa ya ufundi stadi.

Mheshimiwa Spika, Tanzania kama nchi nyingine duniani, bado inakabiliwa na tatizo la dawa za kulevyta. Katika mwaka 2003, kulikuwa na matukio 4,592 ya uhalifu wa dawa za kulevyta ambayo yalihusisha Watanzania 6,102. Ili kukabiliana na hali hiyo, Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevyta kwa kushirikiana na wadau wengine, imeendelea kutoa elimu kwa umma, ushauri nasaha, tiba kwa watumiaji wa dawa za kulevyta na kutekeleza mikakati ya Kikanda na Kimataifa kudhibiti dawa hizo. Aidha, Serikali imehamasisha na kuziwezesha baadhi ya asasi zisizo za Kiserikali kushiriki katika mapambano dhidi ya dawa za kulevyta. Katika mwaka 2004/2005, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, itakamilisha Sera ya Udhibiti wa Dawa za Kulevyta na kuendeleza utekelezaji wa Mpango Kamambe wa Taifa wa Kudhibiti dawa hizo. Shughuli za uratibu na uhamasishaji zitapewa kipaumbele kwa lengo la kuongeza uelewa wa Watanzania kuhusu tatizo la dawa za kulevyta.

Mheshimiwa Spika, msongamano wa wafungwa Magerezani bado ni tatizo hapa nchini. Hata hivyo, Serikali inaendelea kulishughulikia tatizo hili kwa kutumia taratibu mbalimbali. Taratibu hizo ni pamoja na kutolewa kwa msamaha wa Rais, kuimarisha taratibu za kuharakisha kesi za mahabusu, kuhimiza hukumu za vifungo vya nje na kuendelea na maandalizi ya utekelezaji wa Sheria ya Huduma kwa Jamii ya mwaka 2002. Hivi sasa Serikali imekamilisha uundaji wa Kamati ya Kitaifa ya Huduma kwa Jamii ambayo itasimamia kwa karibu utekelezaji wa sheria hiyo. Lengo la Serikali ni kuunda Kamati za aina hiyo katika ngazi za Mikoa na Wilaya nchi nzima katika kipindi cha miaka miwili ijayo. Pamoja na juhudi hizo za Serikali, wananchi nao wanapaswa kutambua kuwa wanalo jukumu la msingi la kushirikiana na Serikali katika kurekebisha wahalifu ndani ya jamii zao na kuwafichua walioshindikana ili wachukuliwe hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kuboresha Utendaji Kazi na Utoaji Huduma katika Utumishi wa Umma ni mkakati wa Serikali kuimarisha Utawala Bora ndani ya Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ili ziweze kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi na wadau wengine. Wizara na Idara za Serikali zimeandaa mikakati ya utendaji kazi ambayo itaanza kutekelezwa katika mwaka huu wa 2004/2005. Ili kupunguza migogoro na kuendeleza mazingira ya amani katika maeneo ya kazi, Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma, ambayo imeweka utaratibu wa waajiri na waajiriwa kujadiliana namna ya kutatua migogoro katika maeneo ya kazi na kuishauri menejimenti katika masuala ya maslahi na ustawi wa watumishi. Katika mwaka 2004/2005, Serikali itaendelea na programu za kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi kwa watumishi wa umma. Kwa upande wa uimarishaji wa vyombo vya utoaji haki, Serikali imeiwezesha Mahakama kutekeleza mpango wa kupunguza mlundikano wa kesi. Lengo la mpango huo ni kuharakisha utoaji wa maamuzi kwa mashauri yaliyopo Mahakamani ili kupunguza kwa kiwango kikubwa malalamiko ya wananchi kuhusiana na tatizo hilo. Aidha, Mahakama zitaanzisha mfumo wa kalenda katika kuendesha kesi ili kuongeza kasi ya kutatua tatizo la mlundikano wa kesi na hivyo kupunguza kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendeleza mapambano dhidi ya rushwa kwa kuimarisha Taasisi ya Kuzuia Rushwa kwa kuipatia majengo na vitendea kazi na kuiwezesha kuendelea kufungua ofisi katika Wilaya mbalimbali. Katika mwaka 2003/2004, Serikali ilipokea malalamiko mapya 2,286 na kuyafanya kazi. Baadhi ya malalamiko hayo yalihusu hujuma mbalimbali ambazo zingeisababishia Serikali hasara kubwa. Katika mwaka 2004/2005, Serikali itaongeza uwezo wa Taasisi ili kuiwezesha kuchuja malalamiko mbalimbali kuhusu rushwa na hivyo kutopoteza muda wa kuchunguza malalamiko ambayo hayahusiani na rushwa. Aidha, kazi ya kuhamasisha na kuelimisha wananchi kuhusu madhara ya rushwa na jinsi ya kupambana na kujiepusha na vitendo vya rushwa itaendelezwa. Taasisi imeanza kijiandaa kikamilifu kufuatilia kwa karibu shughuli zote zinazohusu Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005, ili kuhakikisha kuwa vitendo vya rushwa katika uchaguzi huo vinadhibitiwa mapema. Vita dhidi ya rushwa vitaendelea katika ngazi zote za utawala na uongozi. Serikali inawashukuru sana wananchi wanaoshiriki vita hivi na tunaomba ushirikiano huo uendelee na kuimarishwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliendelea kuimarisha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Katika mwaka 2003/2004, Tume imeandaa taarifa kuhusu hali ya haki za binadamu nchini na kutoa ushauri wa kisheria. Vilevile, Tume imefanya ukaguzi wa Magereza na Vituo vya Polisi nchini. Hali kadhalika, elimu kwa wananchi kuhusu haki za binadamu ilitolewa kwa taasisi na shule mbalimbali katika Mikoa. Katika mwaka 2004/2005, Tume inaendelea kutoa taarifa za utekelezaji wa Haki za Binadamu nchini kwenye Taasisi za Kimataifa kwa mujibu wa mikataba na kutetea hatua zinazochukuliwa kulinda demokrasia na ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, nchi yetu imeshuhudia matukio kadhaa ya moto ambayo yamesababisha hasara kubwa ya maisha na mali. Moto huangamiza maisha ya watu na wakati mwingine huleta hasara kubwa kwa kuunguza majengo, mazao na malisho ya mifugo, hali ambayo husababisha umaskini na njaa.

Kutokana na hali hiyo ni muhimu taasisi zote na wananchi kulichukulia suala la moto kwa uzito unaostahili katika maeneo na makazi yetu. Hatua za kujikinga na matukio ya moto zichukuliwe na taasisi zote za umma na binafsi, kwa kuhakikisha kuwa majengo ya ofisi na makazi yanawekewa viashiria moto na vifaa vingine vya kuzimia moto na kutoa mafunzo ili kupunguza madhara yatokanayo na moto.

Mheshimiwa Spika, vilevile, moto umekuwa ukisababisha madhara makubwa kwa raslimali ya misitu inayokadiriwa kuchangia asilimia mbili mpaka tatu kwenye Pato la Taifa na kuchangia kwa kiasi kikubwa katika kuhifadhi mazingira. Pamoja na umuhimu huo, bado raslimali hiyo imekuwa ikiharibiwa kwa kuchomwa moto hasa wakati wa kiangazi.

Athari za uchomaji misitu ni pamoja na kutoweka kwa misitu, kukauka kwa vyanzo vya maji, mmomonyoko wa udongo na kukaribisha jangwa. Natoa wito kwa Serikali za Vijiji kuwa makini zaidi katika kudhibiti uchomaji moto misitu kwa kushirikisha wananchi. Wale wote wenye tabia ya kuchoma misitu wachukuliwe hatua za kisheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imeendelea kukumbwa na matukio mengi ya ajali za barabarani na ajali za vyombo vya majini. Hata hivyo, ajali nyingi zingeweza kuepukika endapo wananchi wangeacha ushabiki, kujazana kupita uwezo ndani ya vyombo vya usafiri na madreva kutoendesha kwa mwendo wa kasi. Mafuriko ni janga lingine liloyakumba maeneo mbalimbali ya nchi yetu na hata kusababisha wananchi kupoteza maisha. Natoa tena wito kwa wananchi kuepuka kuishi sehemu za mabondeni na maeneo ya mikondo ya maji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Serikali imekamilisha utafiti wa kutambua aina za maafa yanayotokea katika maeneo mbalimbali nchini. Aina za maafa zilizobainishwa ni pamoja na ukame, mafuriko, moto, magonjwa ya milipuko kwa binadamu na mifugo, ajali za vyombo vya usafiri na za viwandani, athari za wakimbizi, vimbunga na pepo kali, migogoro ya kijamii, matetemeko ya ardhi, milipuko ya volkano na wadudu na wanyama waharibifu wa mimea.

Serikali itatumia taarifa hiyo pamoja na Sera ya Maafa iliyozinduliwa tarehe 19 Juni, 2004, kuandaa Mikakati na Mipango ya Kukabiliana na Maafa Nchini. Aidha, Serikali itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu mbinu za kukabiliana na maafa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, hali ya chakula hapa nchini haikuwa ya kuridhisha kutokana na uzalishaji mdogo wa mazao ya chakula katika msimu wa 2002/2003 uliosababishwa na ukame ulioyakumba maeneo mengi ya nchi yetu. Kutokana na hali hiyo, mwezi Julai, 2003 Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, ilifanya tathmini ya upungufu wa chakula nchini. Tathmini hiyo ilibainisha kuwa mwaka 2003/2004, kulikuwa na upungufu wa chakula uliokithiwa kuwa tani 800,000 wakati akiba ya chakula iliyokuwepo nchini ilikadiriwa kuwa tani 450,000. Kwa mujibu wa

tathmini hiyo, wananchi walioathirika zaidi ni wa Mikoa ya Shinyanga, Singida, Dodoma, Mwanza, Pwani na Manyara. Mikoa mingine ni Morogoro, Arusha, Kilimanjaro, Tabora, Mara, Tanga, Mtwara, Lindi, Iringa na Mbeya.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na upungufu huo wa chakula, Serikali ilitenga tani 32,000 za mahindi kutoka Hifadhi ya Chakula ya Taifa na kuwauzia wananchi kwa bei nafuu ya shilingi 50 kwa kilo. Hadi kufikia mwezi Juni, 2004, tani 30,224 zilikuwa zimechukuliwa na Halmashauri mbalimbali za Wilaya kutoka katika vituo vya Hifadhi ya Chakula ya Taifa kwa ajili ya kusambazwa kwa walengwa. Hatua nyingine zilizochukuliwa kukabiliana na upungufu huo ni pamoja na kutoa jumla ya tani 21,742 za mahindi kutoka katika Hifadhi ya Chakula ya Taifa na kuuzia taasisi na wafanyabiashara ili kupunguza makali ya bei kwenye masoko. Serikali pia ilinunua jumla ya tani 32,000 za mahindi kutoka nje ya nchi ili kuongeza akiba ya chakula nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia iliwahamasisha wafanyabiashara waagize chakula kutoka nje ya nchi kwa kuondoa kodi kwenye bidhaa za mahindi na mchele. Kutokana na uhamasishaji huo, hadi kufikia mwishoni mwa Aprili, 2004, jumla ya tani 556,650 za chakula zilikuwa zimeshaingizwa nchini zikiwemo tani 42,697 za mahindi, tani 112,597 za mchele na tani 401,356 za ngano. Hali kadhalika, Serikali iliziomba nchi na mashirika wahisani jumla ya tani 45,000 za chakula kwa ajili ya kaya zilizoathirika zaidi ambapo tani 29,068 zilipatikana kuititia Shirika la Mpango wa Chakula Duniani. Chakula hicho kilisambazwa katika Mikoa ya Singida, Dodoma, Shinyanga, Mwanza, Tabora, Mtwara, Lindi, Iringa, Arusha, Mara, Manyara na Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, sambamba na misaada ya chakula, Serikali pia iliomba msaada wa mbegu kiasi cha tani 3,200 ili kuzipatia kaya 302,026 zilizoathirika zaidi na upungufu wa chakula. Baadhi ya wahisani walioombwa msaada huo walitoa jumla ya Dola za Kimarekani 1,494,000 kuititia Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa zilizotosha kununulia tani 915.8 za mbegu mbalimbali zikiwemo za mahindi, mpunga, mtama, maharage na kunde ambazo zilisambazwa kwa wananchi. Katika msimu wa 2004/2005, hali ya chakula inatarajiwu kuwa nzuri katika baadhi ya Mikoa iliyopata mvua za kuridhisha. Hata hivyo, mvua za masika zimekatika mapema katika baadhi ya maeneo nchini na hivyo kuauthiri ukuaji wa mazao katika maeneo hayo. Kwa hiyo, mavuno katika maeneo hayo yanaweza kuwa pungufu kuliko matarajio. Nachukua fursa hii kuendelea kuwakumbusha wananchi wote kuhifadhi chakula katika kaya zao kama njia ya tahadhari dhidi ya njaa. Kila kaya ijinunulie chakula wakati huu ambapo bei za mazao zimeshuka sana. Napenda kuwashukuru wote waliotusaidia kwa njia moja au nyingine wakati wa upungufu wa chakula. Hao ni pamoja na nchi rafiki, Mashirika ya Dini na asasi zisizo za Kiserikali, Mashirika ya Umoja wa Mataifa, wafanyabiashara mbalimbali, Watumishi wa Serikali na wananchi kwa ujumla. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa zaidi ya wiki moja Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakijadili hotuba zilizotolewa na Mawaziri wa Mipango na Ubinafsishaji na Fedha kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa na Bajeti ya Serikali ya mwaka 2004/2005 na hatimaye kuitisha bajeti hizo. Uchumi wetu kwa ujumla unakwenda vizuri na unatekeleza sera, mikakati na mipango tulioyojiwekea ambayo ni pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo

2025, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000 ambayo ni dira muhimu kwa utekelezaji wa shughuli za Serikali, Mkakati wa Kupunguza Umaskini na Mikataba na makubaliano mengine ya Kimataifa na kikanda kama vile *NEPAD* na *Millenium Development Goals* ya Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, ukuaji wa Pato la Taifa umepungua kuliko ilivyokuwa inatarajiw. Pato letu la Taifa limekua kwa asilimia 5.6 mwaka 2003 ikilinganishwa na matarajio ya asilimia 6.3 na ikilinganishwa na ukuaji halisi wa asilimia 6.2 kwa mwaka 2002. Mfumuko wa bei ambao ulikuwa umefikia asilimia 4.0 mwezi Julai 2003, sasa umepanda na kufikia asilimia 4.6 mwezi Machi, 2004. Kupungua kwa ukuaji wa Pato la Taifa na kupanda kwa mfumko wa bei, kumesababishwa na hali ya ukame katika baadhi ya maeneo nchini iliyoanza msimu wa mwaka 2002/2003 na kuendelea hadi 2003/2004. Hali hiyo imeathiri uzalishaji katika sekta kubwa ya kilimo, hasa sekta ndogo ya mazao ya chakula na biashara. Hata hivyo, hali ya uchumi imeendelea kuwa tulivu ikiwa ni ishara ya mafanikio katika utekelezaji wa sera nzuri za kiuchumi za Chama Cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Akiba yetu ya fedha za nje sasa ni nzuri inayotosheleza kugharamia uagizaji wa bidhaa muhimu kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minane. Aidha, mapato yatokanayo na makusanyo ya ndani kwa mwaka 2003/2004, yameongezeka na kuvuka makadirio tuliyojiwekea na sasa tunakusanya wastani wa shilingi 108 bilioni kwa mwezi ikilinganishwa na wastani wa shilingi 95 bilioni kwa mwezi mwaka 2002/2003. Serikali itaendelea kuweka mazingira bora ili kuwezesha uchumi kuendelea kukua. Tegemeo kuu la kukua kwa uchumi wetu ni pamoja na kuongeza kiwango cha uwekaji akiba na kasi ya uwekezaji mitaji, kuongeza mauzo nje na wananchi wote kufanya kazi kwa bidii, maarifa, ubunifu na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji unatoa mchango mkubwa na endelevu katika kukuza uchumi na kuziendeleza sekta zinazoibuka kuchangia zaidi katika uchumi, hususan sekta za madini na utalii. Kiwango cha uwekezaji mitaji ya moja kwa moja nchini kimeongezeka kutoka Dola za Kimarekani 240.4 milioni mwaka 2002 hadi Dola za Kimarekani 300 milioni mwaka 2003. Hali hiyo inafanya nchi yetu kuongoza katika kuvutia wawekezaji katika Kanda ya Mashariki na Kati katika Afrika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ongezeko la uwekezaji na kukua kwa sekta binafsi nchini ni matokeo ya jitihada mbalimbali za Serikali za kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini kwa kuondoa usumbufu na urasimu usio wa lazima na kutoa vivutio mbalimbali kwa wawekezaji. Aidha, Serikali imepanua maeneo ya ushiriki wa sekta binafsi katika kukuza uchumi wetu na kutoa huduma zote muhimu na za haraka kuitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania kwa wawekezaji wote wa ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Serikali imeendelea kutekeleza kwa dhati Sera ya Urekebishaji na Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma kama njia muhimu ya kuboresha na kurekebisha uchumi. Tathmini ya zoezi hilo inaonesha kuwa kuna mafanikio mazuri. Kwa ujumla mashirika mengi yaliyobinafsishwa yanafanya kazi vizuri baada ya kufufuliwa.

Mashirika hayo yanalipa kodi na kutoa gawio kwa wenyewe hisa badala ya kutegemea ruzuku ya walipa kodi, yameongeza ajira ndani na nje ya mashirika yenyewe na kuzalisha bidhaa bora. Wakulima pia wamefaidika na mashirika yanayoendeshwa vizuri, kwani sasa wana uhakika wa soko la mazao yao. Kwa mfano, kufufuliwa kwa viwanda vya chai, tumbaku, kahawa na sukari, kumeleta manufaa na msisimko kwa wakulima wa mazao hayo, kwa kuwa mapato yao sasa yameongezeka na kuwa endelevu. Aidha, makampuni binafsi yaliyonunua Mashirika ya Umma yameweza kuleta teknolojia mpya na ya kisasa, mbinu mpya za uongozi, pamoja na uwezo mkubwa wa kifedha ili kuongeza ufanisi, tija na faida. Hali hiyo imeliwezesha Taifa kujijengea mazingira mazuri ya kuanza kuwiana na mahitaji ya utandawazi yanayoendelea kutawala dunia kwa kasi kubwa na kujiweka katika nafasi nzuri ya kupenya kwenye masoko ya nje. Serikali itaendelea na mikakati ya kurekebisha mashirika machache yaliyobaki, hasa mashirika makubwa yatoayo huduma muhimu kwa wananchi, kama vile Shirika la Umeme, Shirika la Reli na vitengo vya biashara vya Mamlaka ya Bandari.

Mheshimiwa Spika, uwezeshaji wa wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za uchumi ni sehemu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000. Hata hivyo, ushiriki wa wananchi wengi katika shughuli za uchumi wa kisasa hapa nchini, bado ni mdogo. Ili kukabiliana na hali hiyo, mwaka 2003/2004, Serikali ilikamilisha Sera ya Taifa ya Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi, ambayo pia ilizinduliwa rasmi Mjini Dodoma 19 Juni, 2004. Ofisi ya Waziri Mkuu imepewa jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sera hiyo na Mheshimiwa Rais amemteua Bwana Melkizedek Sanare kuwa Naibu Katibu Mkuu atakayesimamia kitengo hicho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Sera hiyo ni kutoa mwongozo wa jumla utakaohakikisha wananchi wanapata fursa za kushiriki katika uchumi katika sekta mbalimbali. Kwa maana hiyo, sera za kisekta zitalenga katika kuwainua wananchi kwa kuwawezesha kuwa na kauli na ushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi. Katika mwaka 2004/2005, Serikali itawasilisha ndani ya Bunge lako Tukufu, Muswada wa Sheria utakaota utaratibu wa utekelezaji wa sera hiyo.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha umaskini hapa nchini bado ni kikubwa, hususan maeneo ya Vijijini. Katika mwaka 2003/2004, Serikali iliendelea kusimamia utekelezaji wa sera na mikakati ya kuondoa umaskini na kuratibu mfumo wa ufuatiliaji na kutathmini juhudhi zake katika kupiga vita umaskini. Kulingana na Ripoti ya Tatu ya Utekelezaji wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini ya mwaka 2002/2003, uchumi wetu unakua na Tanzania ni moja ya nchi maskini zenye uchumi unaoimarika. Hata hivyo, mafanikio hayo hayajaweza kujiongesha katika hali ya maisha ya mwananchi, kwani kiwango cha umaskini bado ni kikubwa, hasa Vijijini na kinapungua kwa kasi ndogo sana Vijijini ikilinganishwa na Mijini. Umaskini unachangiwa na kiwango kidogo cha uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, mitaji midogo, mbinu hafifu za biashara, ukame unaoikumba nchi yetu mara kwa mara, kilimo kisichoizingatia teknolojia ya kisasa na mwamko mdogo wa baadhi ya wananchi katika kujiletea maendeleo. Hii ni changamoto ya kimaendeleo kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Serikali imejizatiti kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Sera ya Mikopo Midogo Midogo, Sera ya Taifa ya Kuhudumia Wawekezaji Wadogo (*National Microfinance Policy*) na mpango wa dhamana kwa wawekezaji wadogo na wakubwa katika miradi mbalimbali ya maendeleo. Kwa mfano, Serikali itaendelea kutekeleza Programu ya Huduma za Fedha Vijijini ili kuwawezesha wakulima wadogo wadogo na kaya zeny kipato kidogo Vijijini kuwa na kipato endelevu, mali na uhakika wa chakula kwa kuwaongezea uwezo wa kutunza amana na kuwekeza kwa ufanisi katika shughuli za kiuchumi. Wananchi wengi watahamasishwa kujiunga katika vikundi vya kuweka na kukopa na kuboresha uwezo wao kiuongozi na kiutendaji. Hatua hizo zinalenga kuwawezesha wananchi wengi zaidi hapa nchini kujiendeleza kiuchumi na kupata mikopo kutoka vyombo vya fedha vilivyopo. Kuimariswa kwa mifuko ya dhamana ya mikopo na mitaji kunakofanywa hivi sasa na Serikali, ni miongoni mwa hatua madhubuti zinazochukuliwa kuhakikisha kwamba, wananchi wanawezeshwa kushiriki kikamilifu katika uendeshaji wa uchumi na kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutoa mapendekezo ya kuzifanya marekebisho sheria mbalimbali za kodi ili kuwawezesha wananchi kufanya shughuli zao za kiuchumi na kibiashara kwa lengo la kukabiliana na umaskini. Katika jitihada hizo za kupambana na umaskini, Serikali imeanzisha programu ya upimaji wa ardhi, ambapo wananchi watawezesha kupata leseni za umilikaji halali wa ardhi na makazi ambazo zitatumika kama dhamana za kupatiwa mikopo kutoka taasisi zetu za fedha. Serikali itaendelea kuboresha miradi inayoisimamia ili iweze kuwanufaisha wananchi wengi zaidi. Aidha, Serikali imewezesha kuundwa kwa Bodi ya Taifa ya Uratibu wa asasi zisizo za Kiserikali na Baraza la Taifa la asasi hizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kuwa sekta ya kilimo bado ni mhimili wa uchumi wetu, Serikali imeendelea kuongeza bajeti ya sekta hiyo kila mwaka. Lengo la hatua hiyo ni kuongeza mapato ya fedha za kigeni, kuinua hali ya maisha ya mkulima na pia kuwa na uhakika wa chakula. Eneo mojawapo ambalo Serikali imelipa kipaumbele zaidi ni kilimo cha umwagiliaji ili kukabiliana na ukame unaoyakumba maeneo mengi ya nchi yetu. Katika mwaka 2003/2004, ukarabati na ujenzi wa skimu za umwagiliaji maji mashambani na mabwawa ulifanyika. Katika mwaka 2004/2005, mkazo mkubwa utawekwa katika kuendeleza matumizi ya maji kutoka katika maziwa yetu makuu na mito mikubwa kwa ajili ya umwagiliaji, kueneza teknolojia ya uvunaji maji ya mvua, ujenzi wa mabwawa na ukarabati wa skimu za wakulima wadogo. Mafunzo kwa wakulima na wataalam yatapewa kipaumbele hasa katika matumizi bora ya maji, uanzishaji wa vyama vya watumiaji maji na huduma za ugani katika skimu za umwagiliaji. Msisitizo mkubwa utawekwa katika upandaji wa mazao yanayostahimili ukame, uendelezaji wa skimu za umwagiliaji maji mashambani na kuimariswa usimamizi wa kitaalam.

Mheshimiwa Spika, ufanisi wa kilimo unategemea matumizi ya pembejeo hasa mbolea. Katika mwaka 2003/2004, Serikali ilifidia sehemu ya gharama za usafirishaji kwa aina tano za mbolea kwa wakulima wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kwa sababu Mikoa hiyo ina mvua za kutosha. Aidha, Mikoa hiyo ina wakulima wazuri wa mazao ya chakula, lakini ardhi imechoka na haistawishi chochote bila mbolea. Katika mwaka

2004/2005, Serikali itaendelea na utaratibu huo wa kufidia sehemu ya gharama za usafirishaji wa mbolea katika baadhi ya Mikoa kama itakavyofafanuliwa na Waziri wa sekta husika. Viongozi katika Mikoa hiyo wanatakiwa kusimamia kwa karibu usambazaji wa mbolea hiyo ili kuhakikisha kuwa inawafikia walengwa kama ilivyopangwa. Aidha, wakulima wa maeneo hayo waongeze juhudili kuongeza kasi ya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, sambamba na juhudili hizo za Serikali katika sekta ya kilimo, Serikali pia imeendelea kuhamasisha uanzishaji, uimarishaji na uendelezaji wa ushirika. Lengo ni kuwa na Vyama vya Ushirika endelevu na vyenye uhai wa kiuchumi vinavyokidhi mahitaji ya wanachama. Aidha, Sheria ya Vyama vya Ushirika ya Mwaka 2003 iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu, imeweka mazingira mazuri ya kuimarisha ushirika na kuwapa wanachama kauli kubwa zaidi ya kidemokrasia katika uendeshaji Vyama vyao. Kwa kuzingatia sheria hiyo, Serikali itafanya mapitio ya Kanuni za Vyama vya Ushirika ili kuwezesha utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya Mwaka 2002 pamoja na Programu ya Kurekebisha Mfumo wa Uendeshaji wa Vyama vya Ushirika nchini. Sheria iliyoanzisha Shirika la Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika ya Mwaka 1982 pia itafanyiwa marekebisheshi ili kuliwezesha kutekeleza majukumu yake kulingana na Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweza mawasiliano kati ya Vyama vya Ushirika na Benki za Biashara ili kupata mikopo ya kununulia mazao chini ya utaratibu wa dhamana ya mikopo kwa mauzo nje (*Export Credit Guarantee Scheme*). Katika mwaka 2003/2004, Benki ya CRDB iliidhinisha mikopo ya shilingi 13.7 bilioni kwa Vyama Vikuu vya Ushirika 12 na jumla ya shilingi 2.2 bilioni kwa Vyama vya Msingi vitano vya Mkao wa Ruvuma vinavyohusika na zao la kahawa. Hali kadhalika, Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa (*SACCOS*), vimeendelea kuwavutia wananchi. Katika kipindi hicho pia, idadi ya *SACCOS* imeongezeka kutoka 1,236 mwezi Mei, 2003 hadi kufikia 1,375 mwezi Machi, 2004 na hisa na amana zimeongezeka kutoka shilingi 20.9 bilioni kufikia shilingi 27.3 bilioni katika kipindi hicho hicho. Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine, itaendelea kuhamasisha wananchi kuhusu umuhimu wa kuanzisha Vyama vya Ushirika katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kuwajasirisha ili wamiliki na kuendesha Vyama vyao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza Programu ya Uendelezaji wa Mfumo wa Masoko ya Mazao ya Kilimo ili kuongeza kipato na uhakika wa chakula kwa wananchi wanaoishi Vijijini. Lengo la Programu hiyo ni kuendeleza miundo ya masoko kwa wakulima wadogo, wafanyabiashara wadogo na wasindikaji ili waweze kuongeza uzalishaji. Ili kufanikisha malengo hayo, Programu itawezesha uandaaji wa sera, mkakati, sheria na kanuni ili kuboresha sekta ya masoko. Aidha, itawezesha upatikanaji wa mikopo kwa wakulima wadogo, wafanyabiashara wa kati na wasindikaji mazao ili waongeze ukubwa na ufanisi wa biashara zao. Pia, miundombinu ya masoko, hasa barabara za Vijijini zitakarabatiwa. Serikali pia imeimarisha na kuboresha upatikanaji, ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa za masoko. Wigo wa maeneo ya ukusanyaji wa taarifa za bei za rejareja kwa mazao ya kilimo na mifugo umepanuka kutoka masoko 50 mwaka 2000 hadi masoko 75 mwaka 2003. Lengo ni kukusanya

taarifa za bei za jumla katika masoko na minada muhimu nchini na hasa katika ngazi za wilaya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Serikali itakamilisha Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo. Sera hiyo itaweka mazingira bora na mwongozo wa utekelezaji wa shughuli za masoko ya mazao ya kilimo na miundombinu ya masoko nchini. Pia itasimamia uendeshaji wa masoko kwa kuzingatia taratibu na kanuni na hivyo kuondoa migongano katika soko kwa wadau mbalimbali. Aidha, itatoa elimu ya kanuni na taratibu za masoko ya nchi mbalimbali za nje, hususan nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika, Amerika na nchi za Umoja wa Ulaya, ili wafanyabiashara wazingatie viwango vya ubora na umakini unaohitajika katika masoko hayo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, mifugo bora ilisambazwa kwa wafugaji wadogo wadogo kwenye Mikoa 14 nchini na mitamba 619 ilisambazwa kutoka kwenye mashamba ya Serikali ya kuzalishia mitamba. Serikali kwa kushirikiana na asasi mbalimbali imeendelea kutekeleza programu ya kupeleka mifugo Mikoa ya Kusini ili kuongeza kasi ya uendelezaji mifugo katika Mikoa hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi wa Mifugo ulianza huko Umwe, Ikwiriri, karibu na Daraja la Mkapa, ikiwa ni utekelezaji wa Mradi wa Uendelezaji wa Miundombinu ya Masoko ya Mifugo. Katika mwaka 2004/2005, mitamba 1,000 itazalishwa kutoka kwenye mashamba ya Serikali na kusambazwa kwa walengwa. Aidha, Serikali itaimarisha huduma za ugani zinazopelekwa Wilayani ili kuongeza ufanisi kwa wafugaji, kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa maeneo ya malisho katika Halmashauri za Wilaya 50 na kutafuta vyanzo vya maji kwa ajili ya mifugo katika maeneo yenye ukame. Hali kadhalika, Serikali itaboresha ufanisi wa masoko ya mifugo na miundombinu mingine ili kuongeza uuzaaji wa mifugo na mazao yake nje ya nchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sekta ya viwanda imekua kutoka asilimia 8.0 mwaka 2002 hadi asilimia 8.6 mwaka 2003. Aidha, mchango wa sekta hiyo katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 8.7 mwaka 2003 ikilinganishwa na asilimia 8.4 mwaka 2002. Mafanikio hayo yanatokana na ongezeko la uzalishaji, utulivu wa mfumo wa sera zetu za uchumi na ubinafsishaji ambapo viwanda vingi vimepata wawekezaji wenyewe uwezo na uzoefu wa kuviendesha. Aidha, sera ya uwekezaji imehamasisha uanzishaji wa viwanda vipyta hasa katika sekta ya usindikaji wa mbegu za mafuta ya kula, utengenezaji wa nguo, usindikaji wa matunda na bidhaa nyingine za kilimo, usagishaji wa nafaka, bidhaa za ujenzi, kemikali, vinywaji, sabuni na madawa ya binadamu. Kuimarka kwa sekta hiyo ya viwanda kumewezesha upatikanaji wa bidhaa muhimu kwa wananchi, ongezeko la ajira, mauzo ya bidhaa za viwanda nje ya nchi na ongezeko la mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa programu ya kuhamasisha, kuwezesha na kuelekeza wawekezaji katika kujenga viwanda vya usindikaji wa mazao ya kilimo ili kupunguza upotevu unaotokea baada ya mavuno. Programu hiyo ina lengo la kuwianisha maendeleo ya viwanda na kilimo ili sekta ya viwanda iweze kuwa kichocheo cha

maendeleo ya sekta ya kilimo. Serikali pia ilikamilisha Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo. Sera hiyo inalenga katika kuendeleza viwanda vidogo vinavyosindika mazao ya kilimo Mijini na Vijiji ili kuinua maendeleo ya Vijiji na sekta ya kilimo. Aidha, sera hiyo imezingatia mahitaji ya biashara ndogo ndogo yakiwemo ya kutenga maeneo maalum kwa shughuli hizo, kurahisisha taratibu mbalimbali zikiwemo zile za upatikanaji wa fedha na huduma nyingine muhimu. Sera mpya ya biashara pia imekamilika na itaiwezesha nchi yetu kufaidika kikamilifu na mabadiliko katika kuendeleza mikakati ya kujenga uchumi wenyewe uwezo wa ushindani wa biashara ya Kimataifa. Kwa upande mwingine, Sera hiyo itatuwezesha kutekeleza mabadiliko ya kiuchumi katika misingi ya soko huria na kutumia nyenzo mbalimbali kuufanya uchumi huo kuingia katika mfumo wa utandawazi. Ni vema basi Watanzania tuendelee kutumia fursa hizo hasa katika kuuza bidhaa zetu za viwandani katika masoko ya Afrika Mashariki, nchi zilizo Kusini mwa Afrika na kwingineko duniani.

Mheshimiwa Spika, utalii ni mionganoni mwa vyanzo vya kutegemewa vya Pato la Taifa. Nchi yetu ina vivutio vingi vya utalii na biashara ambavyo ni tegemeo kubwa la uchumi. Ili kuongeza soko la utalii, Serikali imeboresha miundombinu muhimu kama barabara ziendazo katika mbuga za wanyama na hoteli za kitalii. Maeneo mapya ya utalii nayo pia yamefunguliwa hasa Magharibi na Kusini mwa nchi yetu. Aidha, utangazaji wa vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi ulifanyika kwa kutumia vyombo mbalimbali ikiwemo Tovuti ya utalii na Ofisi za Balozi zetu. Kwa kuwa utalii unategemea zaidi soko la nje ambalo halitabiriki kwa sasa kutokana na tatizo la ugaidi, ni wajibu wetu kuhakikisha kuwa, watalii wanaoingia nchini wanahakikishiwa usalama wao. Ni vyema wananchi waongeze ushirikiano na vyombo vya dola ili kudhibiti tishio hilo ambalo linaweza kuathiri ukuaji wa mapato yatokanayo na sekta ya utalii.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Madini imekua kutoka asilimia 15 mwaka 2002 hadi asilimia 17 mwaka 2003. Aidha, mauzo ya madini nje ya nchi yameongezeka kwa asilimia 17.4 kutoka Dola za Kimarekani milioni 471 mwaka 2002 hadi Dola za Kimarekani milioni 553.1 mwaka 2003. Madini yaliyochangia katika ongezeko hilo ni dhahabu, ambapo uzalishaji ulikuwa kilo 45,299 mwaka 2003 ikilinganishwa na kilo 34,065 zilizozalishwa mwaka 2002. Ongezeko hilo limetokana na mitaji mikubwa iliyowekezwa na makampuni ya uchimbaji wa dhahabu yakiwemo yale ya *Kahama Mining Corporation Limited, Afrika Mashariki Gold Mine Limited, Geita Gold Mine Limited* na *Buhemba Mine*. Haya ni matokeo ya utekelezaji wa Sera ya Madini ya mwaka 1998, ambayo pamoja na mambo mengine, imefanya nchi yetu kuwa kivutio kikubwa kwa wawekezaji wakubwa kutoka nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ongezeko la wawekezaji katika sekta ya madini, ongezeko la uzalishaji wa madini, ongezeko la mapato ya mauzo nje na ongezeko la ajira, kumekuwapo na malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi kupitia kwa Waheshimiwa Wabunge na pia Vyombo vya Habari kuhusu sekta ya madini. Kwa kuzingatia malalamiko hayo, Serikali imeunda Kamati Maalum ya Wataalam ya kuchunguza na kuchambua matatizo ya sekta ya madini na kutoa mapendekezo ya kuboresha Sera ya Madini na ikibidi kufanya marekebisho ya sheria husika ili kuimarisha usimamizi na udhibiti wa shughuli za madini nchini kwa kadri itakavyoonekana inafaa. Kamati hiyo

ilianza kazi yake Februari, 2004 na inatarajia kuikamilisha kazi hiyo Agosti, 2004. Tayari Kamati imetembelea baadhi ya Mikoa yenyе migodi na wachimbaji wadogo ili kupata maoni na michango yao kutoka kwa wananchi, watafiti, watendaji wa Serikali, wachimbaji wakubwa na wadogo na pia wafanyabiashara wa madini nchini. Lengo ni kuwa na utaratibu wa sheria muafaka ambao utaendelea kuwavutia wawekezaji katika sekta ya madini na wakati huo huo nchi kuendelea kufaidika na madini yake.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza Mpango wa Miaka Kumi wa Kuendeleza Mtandao wa Barabara kwa kipindi cha 2001 - 2010. Mpango huo unatumika kama mwongozo wa kuteua barabara kuu na za Mikoa zitakazofanyiwa ukarabati. Ujenzi wa Daraja la Mto Ruffiji umekamilika na daraja limefunguliwa na Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Agosti 2003 na kwa kutambua mchango wake mkubwa katika ujenzi na ukamilishaji wake, daraja hilo limepewa jina la Daraja la Mkapa. Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya ukarabati na ujenzi wa barabara kuu na zile za Mikoa. Katika mwaka 2003/2004, barabara kuu na zile za Mikoa zenyе urefu wa kilomita 16,274 zilipangwa kutengenezwa. Madaraja 1,809 yalipangwa kutengenezwa. Hadi Machi, 2004, jumla ya kilomita 3,511 za barabara kuu na kilomita 4,178 za barabara za Mikoa nazo zimetengenezwa. Aidha, madaraja 259 yaliyoko katika barabara kuu na 236 yaliyoko katika barabara za Mikoa yametengenezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Serikali itafanya matengenezo ya kilomita 13,474 za barabara na madaraja 1,692 katika barabara kuu na za Mikoa. Kwa vile ukuaji wa uchumi wetu na maendeleo kwa ujumla yanategemea barabara hizo, hatuna budi kuzitunza ipasavyo. Tunaomba wananchi waone umuhimu wa kutunza raslimali hiyo muhimu kwa uchumi wetu ikiwa ni pamoja na kutokuingilia maeneo ya hifadhi ya barabara. Kwa wale ambao tayari nyumba zao zimewekewa alama za “X” ni vyema wafahamu kuwa wapo katika hifadhi ya barabara. Ili wananchi wasipate hasara ya kuvunjiwa nyumba zao, Halmashauri zinazohusika zihakikishe zinatoa kipaumbele kuwapatia wananchi hao wenye alama ya “X” viwanja ili waanze polepole kuhamisha nyumba zao kwenda maeneo yanayloruhusiwa kisheria. Kama mtu aliywewkewa alama ya “X” hatatumia nafasi hiyo, kwa uhakika wakati ujenzi wa barabara utakapofika, nyumba yake itavunjwa na atapata hasara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Sekta ya Mawasiliano na Uchukuzi imeendelea kuimarika kutokana na uboreshaji wa miundombinu pamoja na huduma zake. Sera ya Taifa ya Uchukuzi ilikamilika na kuzinduliwa rasmi Oktoba, 2003. Aidha, mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Mawasiliano na Habari utakamilika mwaka 2004/2005. Nchi yetu imeendelea kuelekeza juhud zake katika mapinduzi ya kuelekea kwenye jamii-habari kwa kutumia teknolojia za mawasiliano na upashanaji habari. Lengo ni kuongeza kiwango cha matumizi ya teknolojia hiyo kama njia ya kutoa msukumo katika utekelezaji wa demokrasia na Utawala Bora, kuendeleza na kuimarisha dhana ya ushirikiano mionganoni mwa watu, taasisi, nchi na mabara kwa kubadilishana taarifa na upashanaji habari. Ili kutimiza lengo hilo, juhud zimeanza kuelekezwa katika kujenga uwezo wa watu wetu kwa kutoa mafunzo katika kiwango cha Kimataifa kwa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano

katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo cha Ufundı Arusha. Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa aina hiyo ya mafunzo inasambazwa katika vyuo vingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kurekebisha huduma za usafiri wa anga ili kuondoa kero mbalimbali zinazowakabili wananchi. Vituo vya safari za ndege vimeongezeka kutoka saba mwaka 2002/2003 hadi 15 mwaka 2003/2004 na idadi ya safari kwa wiki zimeongezeka kutoka 28 hadi 97 katika kipindi hicho hicho. Kiwango cha ndege kuondoka kwa wakati kimefikia asilimia 90 kutoka asilimia 54 miaka michache iliyopita. Vilevile, Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuimarisha usalama katika viwanja vya ndege ikiwa ni pamoja na kuweka mitambo mbalimbali ya usalama. Aidha, katika mwaka 2003/2004, Serikali imefanya mapitio ya Makubaliano ya Usafiri wa Anga kati ya Tanzania na nchi za Botswana, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Msumbiji, Malawi, Nigeria, Uganda, Falme za Kiarabu na Zimbabwe.

Serikali itaendelea kufanya mapitio ya makubaliano mengine na kuanzisha makubaliano mapya kwa lengo la kuyapatia makampuni yetu fursa ya kutoa huduma katika masoko ya nje na pia kutoa nafasi ya ushindani ili kuboresha huduma. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa sekta ya umeme umeongezeka kutoka asilimia 3 mwaka 2002 hadi asilimia 5 mwaka 2003. Uzalishaji wa umeme ulipungua kwa asilimia 4.8 toka saa za gigawati (*Gwh*) 2,791.3 zilizozalishwa mwaka 2002 hadi kufikia saa za gigawati (*Gwh*) 2,668.3 mwaka 2003. Kupungua kwa uzalishaji wa umeme kumesababishwa na ukame ulioathiri uzalishaji wa umeme unaotokana na nguvu za maji. Hata hivyo, Serikali ilifanya ukarabati wa mfumo wa umeme katika maeneo mbalimbali nchini ambao umechangia kupungua kwa upotevu wa umeme kutoka asilimia 27 mwaka 2001 hadi asilimia 23 mwaka 2003. Serikali pia imeendelea na miradi ya upolekaji wa umeme katika Miji Mikuu ya Wilaya za Serengeti, Biharamulo, Ngara na Ukerewe. Usambazaji umeme katika Wilaya za Urambo na Rufiji utafanyika mwaka 2004/2005. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa bomba la gesi ya Songo Songo umekamilika na gesi hiyo itatumika kwa ajili ya uzalishaji wa umeme katika mitambo ya umeme Ubungo na baadaye katika mitambo ya *IPTL*. Hii itasaidia kupunguza utegemezi wa umeme unaozalishwa kwa mitambo inayoendeshwa kwa nguvu za maji. Gesi hiyo itatumika pia kwenye baadhi ya viwanda vikubwa kama Kiwanda cha Saruji cha *Wazo Hill*, Kiwanda cha Bia na matumizi ya nyumbani. Aidha, katika mwaka 2004/2005, maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi ya *Mnazi Bay* kwa ajili ya Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma yataanza.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa ardhi kama raslimali muhimu kwa maendeleo ya sekta nyingine, Serikali imechukua hatua zenye lengo la kuweka mipango mizuri na endelevu ya ardhi. Katika mwaka 2003/2004, Serikali iliandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika wilaya mbalimbali nchini. Aidha, Serikali imeanza kutoa vyeti vya ardhi kwa Serikali za vijiji ili kuvipa uwezo zaidi wa kupanga vyema matumizi bora ya ardhi yao. Kwa upande wa upimaji wa viwanja kwa ajili ya makazi na huduma, zoezi maalumu la upimaji viwanja katika Jiji la Dar es Salaam

limefanikiwa kwa kiwango cha juu. Hadi tarehe 30 Aprili, 2004, jumla ya viwanja 26,793 vilikuwa vimepimwa katika eneo la mradi ikilinganishwa na viwanja 20,000 vilivyokadiriwa awali.

Aidha, Serikali inashughulikia pia tatizo la ujenzi ulio nje ya utaratibu wa mipango miji, hasa katika Jiji la Dar es Salaam. Ujenzi huo unahusu nyumba za kuishi, nyumba za biashara na vituo vya mafuta, ambavyo vimejengwa bila vibali au kinyume cha taratibu na sheria. Kuhusu uanzishaji wa Hazina ya Ardhi, Serikali imeshabaini maeneo ya ardhi yenye jumla ya hekta milioni 3.1 ambayo yanafaa kwa uwekezaji. Kati ya hayo, eneo la hekta milioni 1.5 limepimwa. Lengo la zoezi hilo ni kukiwezesha Kituo cha Uwekezaji cha Taifa kuwa na hazina ya ardhi inayofaa kwa uwekezaji na hivyo kupunguza usumbufu wa kutafuta ardhi kwa wawekezaji. Katika mwaka 2004/2005, Serikali itaendelea na zoezi la uhakiki wa maeneo yaliyopimwa kwa ajili ya Hazina ya Ardhi. Aidha, wananchi wataendelea kuelimishwa ili watambue kwamba, kuwa na hati ya ardhi kutawawezesha kuitumia kama dhamana ya kupata mikopo ambayo wanawenza kuitumia kwa ajili ya shughuli za kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi unaendelea kwa viwango vya kuridhisha. Uandikishaji wa watoto wenye umri wa kuanza shule umeendelea kuwa wa kuridhisha kwa miaka mitatu mfululizo tangu mpango huo uanze. Katika mwaka 2004, jumla ya watoto 1,319,297 waliandikishwa kuanza darasa la kwanza ikiwa ni asilimia 80 ya lengo lililotarajiwa la kuandikisha wanafunzi 1,640,969. Ili kukabiliana na ongezeko la wanafunzi, katika mwaka 2003/2004, Serikali iliajiri walimu wapya 15,921 sawa na asilimia 76.7 ya lengo lililokuwa limewekwa la kuajiri walimu 20,751. Serikali pia imetoa msukumo katika uanzishaji wa shule za awali ambazo zitatumika kuwaandaa watoto wanaoanza darasa la kwanza. Idadi ya shule za awali zilizoandikishwa, za Serikali na zisizo za Serikali, imeongezeka kutoka 11,846 mwaka 2003 hadi 12,984 mwaka 2004. Uandikishaji wa watoto umeongezeka kutoka 744,750 mwaka 2003 hadi kufikia watoto 960,470 mwaka 2004. Aidha, Kamati za Elimu katika Halmashauri zimepata mafunzo ya uongozi, udhibiti wa fedha, utunzaji wa vifaa vya shule na mpango wa jumla wa maendeleo ya shule. Suala muhimu ambalo ni lazima tuendelee kulisisitiza na kuimarisha utekelezaji wake ni lile la wananchi kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa Mpango huo. Mpango una lengo la kusaidia nguvu za wananchi na siyo mbadala wa nguvu hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Elimu ya Sekondari, Serikali imekamilisha maandalizi yote muhimu kwa ajili ya kuanzisha Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari. Mpango huo utaanza rasmi Julai, 2004. Lengo la Mpango huo ni kuongeza nafasi kwa vijana wa kike na kiume wanaohitimu na kufaulu elimu ya msingi ili waweze kujiunga na elimu ya sekondari, kuboresha na kutoa kwa usawa elimu ya sekondari, kuimarisha na kuboresha uongozi na usimamizi wa utoaji wa elimu na kuboresha elimu yenye. Ili kuhakikisha watoto wengi wanaofaulu wanapata nafasi ya kusoma, mpango una lengo la kupunguza ada za shule za sekondari ili wazazi wengi zaidi waweze kumudu kusomesha watoto wao. Utaratibu kamili utatolewa na Wizara husika. Ili kufanikisha Mpango huo, wito wangu kwa wananchi ni kuwa wajitokeze kwa wingi kushiriki katika Mpango huo kama walivyofanya kwenye Mpango wa Elimu ya Msingi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tunayo Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Serikali kwa Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu ya mwaka 2004. Chini ya sheria hiyo, utawekwa utaratibu utakaowezesha utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vya umma na binafsi wasio na uwezo, kuwatambua wakopaji wenyewe mahitaji zaidi ili waweze kusaidiwa, kuongeza udahili katika vyuo vikuu vya binafsi na vile vya umma na kuziwezesha taasisi binafsi za elimu ya juu kutumia vyema miundombinu hiyo. Bodi hiyo itahakikisha kuwa wale wanaopatiwa mikopo hiyo wanawajibika kuirudisha baada ya kumaliza masomo yao wakiwa wamepata ajira au wanajitegemea. Fedha zinazorudishwa pamoja na fedha zinazotengwa na Serikali, zitajenga mfuko mkubwa zaidi utakaokuwa na uwezo wa kuwakopesha vijana wengi zaidi. Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2004/2005, Serikali itaunda Bodi hiyo na kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ili tuweze kuwa na utaratibu endelevu utakaowawezesha vijana wengi zaidi kujiunga na elimu ya juu kwa kutumia mikopo. Nataka kusisitiza tena kuwa, lengo la Mfuko ni kuwawezesha wanafunzi wengi zaidi kupata elimu ya juu na siyo kuwakwaza kama ilivyokuwa inatafsiriwa na baadhi ya watu na wanafunzi. Hakuna mwanafunzi atakayekosa kusoma kwenye Vyuo vya Elimu ya Juu kwa kukwazwa na masharti ya Mfuko huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Serikali imeendelea kuifanyia marekebisho sekta ya afya ili kuboresha utoaji wa huduma na kuondoa kero mbalimbali zinazowakabili wananchi. Uhamasishaji wananchi kuanzisha Mfuko wa Afya ya Jamii katika Halmashauri za Wilaya umeendelea. Hadi sasa Halmashauri 88 zimehamasishwa kuhusu umuhimu wa kuanzisha Mfuko wa Afya ya Jamii na tayari Halmashauri 40 zimeshaanzisha Mfuko huo. Aidha, uundaji wa Bodi za Huduma za Afya za Halmashauri na Kamati mbalimbali za vituo vya kutolea huduma za afya unaendelea vizuri. Hadi Mei, 2004, jumla ya Halmashauri 89 zilikuwa zimefanya uhamasishaji wa kuunda Bodi za Huduma za Afya na kati ya hizo, Halmashauri 34 tayari zimeunda Bodi hizo. Zoezi la uhamasishaji na uundaji wa Bodi hizo, linatarajiwa kukamilika Desemba, 2004. Halmashauri zilizohamasishwa hazina budi kufanya jitihada ya kukamilisha utungaji wa sheria ndogo ndogo kuruhusu uundaji wa Bodi na Kamati zinazohusika kama inavyotamkwa na Sheria ya Mfuko wa Afya ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Bima ya Afya umeendelea kuboresha huduma zake kwa kusajili wanachama wapya na kuongeza usajili wa vituo vinavyotoa huduma hizo. Hadi Aprili 30, 2004, Mfuko ulikuwa umesajili jumla ya wanachama 242,508 ikilinganishwa na wanachama 167,989 kipindi kama hicho mwaka 2003. Aidha, vituo vya huduma za matibabu 3,583 na maduka ya dawa 21 yamesajiliwa. Ili kupunguza usumbu kwa wanachama, Mfuko ulifungua Ofisi saba za kanda zilizoanza kazi rasmi Mei, 2003 na hivyo kuwezesha kuwasiliana na wadau wake wengi kwa karibu zaidi. Kwa mwaka 2004/2005, Mfuko wa Bima ya Afya utaendelea kuboresha huduma zake kwa kuimarisha ofisi za kanda kwa kuzipa nyenzo, vifaa na watumishi wa kutosha. Ofisi hizo pia zitaunganishwa na Makao Makuu kwa njia ya mtandao ili kurahisisha mawasiliano na kuwalipa watoa huduma kwa haraka zaidi.

Aidha, ukaguzi wa mara kwa mara wa vituo vya matibabu utaendelezwa ili kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa zinakidhi ubora unaotakiwa. Mfuko vilevile

utaendelea kutoa elimu kwa watoa huduma na wanachama ili waweze kufahamu vizuri majukumu yao na mabadiliko mbalimbali yanayoendelea kufanywa.

Mheshimiwa Spika, hali ya UKIMWI nchini bado ni mbaya. Takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2002, takriban watu milioni mbili nchini walikuwa wakiishi na virusi vya UKIMWI. Katika kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI hapa nchini, Serikali imeimarisha mapambano dhidi ya ugonjwa huo ambapo Kamati Shirikishi za kudhibiti UKIMWI za Halmashauri za Serikali za Mitaa zimeundwa. Kamati hizo zipo katika ngazi za Halmashauri, Kata, Vijiji, Mitaa na Vitongoji. Waheshimiwa Wabunge na Madiwani ni Wajumbe wa Kamati hizo katika ngazi ya Halmashauri na Kata. Ili kuimarisha uwezo wa Serikali za Mitaa wa kudhibiti UKIMWI, Wajumbe wa Kamati katika Halmashauri 114 wamepatiwa mafunzo kuhusu kupanga, kusimamia na kuratibu mipango shirikishi ya kudhibiti UKIMWI kati ya Machi na Mei, 2004. Mafunzo hayo yataendelezwa katika ngazi za Kata, Vijiji, Mitaa na Vitongoji. Napenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge, washiriki kikamilifu katika kufuatilia mipango yote ya kudhibiti UKIMWI katika ngazi hizo.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Serikali iko katika maandalizi ya kuhakikisha upatikanaji wa dawa dhidi ya virusi geuzi kwa wagonjwa wa UKIMWI. Kwa kuanzia, wagonjwa 33,000 watapatiwa dawa hizo kwa mwaka huu wa 2004. Idadi hiyo itaongezeka hadi kufikia wagonjwa 220,000 ifikapo mwaka 2005 sawa na asilimia 50 ya wagonjwa wote wa UKIMWI walio katika hatua ya kuanzishiwa dawa hizo.

Aidha, Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI, umeshaanzisha Kitengo cha Huduma na Tiba, ambacho kitaratibu na kusimamia shughuli zote zinazohusu dawa dhidi ya virusi geuzi. Kwa kuanzia, Serikali imetenga shilingi bilioni mbili kwa ajili ya ununuzi wa dawa hizo. Kupatikana kwa dawa dhidi ya virusi geuzi ambazo humsaidia mgonjwa wa UKIMWI kuboresha afya na kurefusha maisha yake, ni faraja kwa Watanzania waishio na virusi vya UKIMWI. Ili kuweza kufaidika na mpango huo, ni lazima hali ya afya ya mhusika iwe imejulikana.

Nawasihi Watanzania tupime afya zetu ili kama tumeathirika tupate huduma hiyo ya dawa za kurefusha maisha mapema. Hata hivyo, ikumbukwe kwamba, dawa hizo haziponyeshi ugonjwa, bali zinapunguza tu makali ya UKIMWI na kumwezesha mgonjwa kuishi kwa muda mrefu zaidi. Dawa sahihi ya ugonjwa huo ni kubadili tabia na kuacha uasherati au ikibidi kufanya mapenzi salama. Kwa msingi huo, shughuli na harakati za udhibiti wa UKIMWI hazina budi kuendelezwa ikiwa ni pamoja na kuimarisha mipango yote ya kisekta ya kupambana na Ugonjwa wa UKIMWI. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kuwawezesha wananchi kupata maji safi na salama. Ujenzi wa mradi mkubwa wa maji wa Wami-Chalinze, uliofadhliliwa na Serikali yetu na ile ya Watu wa China umekamilika na unatoa huduma kwa watu zaidi ya 62,000 katika vijiji 17 vya Wilaya ya Bagamoyo na Mji Mdogo wa Chalinze. Pia miradi ya maji katika baadhi ya vijiji katika Mikoa ya Morogoro, Mwanza, Shinyanga, Mbeya, Kagera, Iringa, Singida, Kilimanjaro, Arusha, Tabora, Mara, Manyara na Mtwara imekamilishwa. Vilevile, maandalizi ya kuanza kwa

mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria hadi Miji ya Shinyanga na Kahama, utakaogharimu karibu shilingi bilioni 85.1 yamekamilika na ujenzi ulianza Machi, 2004.

Katika mwaka 2004/2005, Serikali itaanzisha programu ya maji vijijini ambayo lengo lake ni kuhusisha vijiji karibu vyote nchini ifikapo Julai, 2005. Kuhusu maji Mijini, baada ya mafanikio makubwa ya kukarabati vyanzo vya maji na mifumo ya majitaka katika baadhi ya Miji, Serikali itasaidiana na Mamlaka za Majisafi na Majitaka za Miji 10 kuimarisha uwezo wa uendeshaji na matengenezo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi nchini yanapata maji kutoka kwenye visima au mabwawa. Hadi Aprili, 2004, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imechimba jumla ya visima 433. Aidha, Serikali imetekeleza zoezi la kutambua vyanzo vya maji katika baadhi ya mabonde nchini, kufanya ukaguzi na vilevile kushirikiana na wadau mbalimbali kudhibiti uharibifu na uchafuzi wa mazingira. Pamoja na ongezeko la mahitaji ya maji mwaka hadi mwaka, zipo dalili za kukauka kwa vyanzo vya maji katika maeneo mbalimbali nchini kutokana na ongezeko la shughuli nyingi za kijamii, kama vile kilimo, ufugaji, ujenzi wa makazi na hata uchomaji wa misitu. Serikali kwa kushirikiana na wadau wa raslimali za maji, itaendelea kutoa kipaumbele katika juhudhi za kuhifadhi vyanzo vya maji na kuondoa migongano isiyo ya lazima katika matumizi ya raslimali hiyo muhimu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, Serikali ilikamilisha awamu ya kwanza ya kurekebisha sera na sheria za kazi ili ziende na wakati na kuondoa kero kwa wananchi. Sheria ya Mahusiano Kazini na Sheria ya Taasisi za Utekelezaji wa Sheria ya Kazi zilirekebishwa na kupitishwa na Bunge lako Tukufu. Serikali inashirikiana na wadau mbalimbali kuandaa mikakati ya kupambana na ajira ya watoto.

Kazi ya kuelimisha jamii inaendelea ikiwa ni pamoja na kuendesha warsha kwa wadau mbalimbali ili kuongeza uelewa wao wa mikataba na sheria za Kimataifa zinazopiga vita utumikishwaji watoto. Aidha, watoto wanaoishi katika mazingira magumu wanaongezeka katika maeneo mengi nchini, hususan Mijini. Tatizo la UKIMWI, linachangia kwa kiasi kikubwa ongezeko hili. Taasisi zinazohudumia watoto hao zimeshindwa kukidhi mahitaji kutokana na uwezo mdogo. Natoa wito kwa viongozi wa ngazi zote za mitaa, vitongoji, vijiji, kata, tarafa na Wilaya, kuwahamasisha wananchi katika maeneo yao juu ya umuhimu wa kutambua na kuwasaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikihimiza maendeleo ya jamii yanayozingatia jinsia kwa kuingiza masuala ya jinsia katika sera, mikakati na programu mbalimbali za Kitaifa. Katika kufanikisha lengo hilo, Serikali imeamua kuanzisha madawati ya jinsia katika Wizara, Taasisi, Mikoa na Wilaya zote nchini. Wizara na Idara za Serikali zinao wajibu wa kuteua maafisa hao ili Serikali kwa ujumla iweze kutekeleza masuala ya jinsia kwa vitendo. Aidha, Serikali inayo mifuko mbalimbali ya maendeleo ya wananchi, mmojawapo ukiwa Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake. Madhumuni ya Mfuko huo ni kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wanawake wenye kipato kidogo ili kuwawezesha kuijendeleza kiuchumi na hivyo kuondokana na umaskini. Ili Mfuko

huo uwe endelevu na uweze kuwanufaisha wakopaji wengi zaidi, wakopaji hawana budi kurudisha mikopo yao na Halmashauri za Wilaya na Miji zirejeshe pia mikopo hiyo kwa Wizara husika. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Habari hapa nchini, sasa inaongozwa na Sera mpya ya Habari na Utangazaji iliyopitishwa na Serikali Oktoba, 2003. Lengo ni kuifanya sekta iendane na hali halisi ya mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi na kijamii na iweze kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya Taifa. Sera hiyo imeweka mazingira mazuri ya kuwezesha kushamiri kwa Vyombo vya Habari vinavyozingatia maadili ya taaluma ya Uandishi wa Habari na vinavyolinda, kudumisha na kuendeleza maadili mema ya jamii yetu.

Aidha, Sera hiyo itaondoa malalamiko mengi ya wananchi yaliyokuwepo kama vile kutozingatiwa kwa wajibu wa Vyombo vya Habari kwa jamii, huduma ya vyombo hivyo kutowafikia wananchi wote, uduni wa viwango vya taaluma na kutozingatiwa kwa maslahi ya Taifa. Sera hiyo pia itaiwezesha Serikali na watu binafsi kuanzisha na kuendeleza huduma za habari katika sehemu yoyote nchini. Katika mwaka 2004/2005, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itadurusu sheria zinazosimamia shughuli za Vyombo vya Habari kwa lengo la kuwasilisha marekebisho ya sheria katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kuunda Taasisi ya Utangazaji Tanzania ambayo inaunganisha Redio Tanzania Dar es Salaam na Televisheni ya Taifa bado inaendelea. Hivi sasa Taasisi hiyo ipo chini ya Mamlaka moja kiutawala na kiuendeshaji. Aidha, Serikali, ilikamilisha ujenzi wa mitambo ya kurushia matangazo ya redio na televisheni kwa njia ya satelaiti. Hii imewawezesha wananchi kote nchini kupata matangazo hayo. Serikali pia ilikamilisha ujenzi wa vituo vya matangazo ya moja kwa moja ya televisheni katika Mikoa ya Dodoma, Arusha na Mwanza. Usikivu wa Redio Tanzania umeendelea kuongezeka baada ya kukarabati mitambo katika vituo vya kurushia matangazo vya Dar es Salaam, Mbeya, Arusha na Mwanza na kuunganisha vituo vya Lindi, Nachingwea, Kigoma na Songea na Makao Makuu kwa njia ya satelaiti.

Katika mwaka 2004/2005, Serikali itakamilisha ujenzi wa vituo vya Mbeya, Tabora, Lindi, Kagera, Kigoma, Tanga na Mara. Pamoja na juhudhi hizo, ni matarajio ya Serikali kuwa vituo vya kurushia matangazo ya televisheni na redio vinavyomilikiwa na Halmashauri za Wilaya na Miji vitarusha matangazo ya Taasisi ya Utangazaji ili wananchi wanufaika na huduma ya chombo chao cha Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha utendaji wa Idara ya Mpiga Chapa ili iweze kumudu ongezeko la kazi na vilevile ushindani. Katika mwaka 2003/2004, Idara imewezeshwa kupata mitambo ya kisasa yenye uwezo wa kuchapisha kazi kwa wepesi na unadhifu. Mwaka 2004/2005, Serikali itaendelea kuiwezesha Idara kuboresha na kuimarisha uwezo wa utendaji ili kukidhi, pamoja na mambo mengine, mahitaji makubwa ya uchapishaji wa nyaraka zinazohusu Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005. Pia Idara itawezeshwa kupata mtambo wa teknolojia ya hali ya juu zaidi wa kudhibiti usalama wa nyaraka za Serikali. Idara itakuwa mwenyeji wa Mkutano Mkuu wa

Wapiga Chapa wa Serikali Duniani utakaofanyika Mei, 2005. Kwa upande wa Kampuni ya Magazeti ya Serikali, jitihada za kuimarisha muundo wa Kampuni hiyo ziliendelea ili kuiwezesha kuijendesha kibiashara zaidi katika mazingira ya ushindani. Kwa mwaka 2004/2005, Kampuni itaanzisha gazeti la Kiswahili kwa lengo la kuwafikia wasomaji wengi zaidi, hususan maeneo ya vijiji. Aidha, Serikali itaisaidia Kampuni hiyo kuimarisha mtaji wake ili iweze kupata mtambo wa kuchapisha magazeti na hivyo kumudu ushindani wa soko la uchapishaji uliopo hivi sasa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mpango wa uboreshaji wa mfumo wa Serikali za Mitaa unazingatia Sera ya Serikali ya kupeleka madaraka kwa wananchi. Ili kutekeleza azma hiyo, katika mwaka 2003/2004, Serikali imepitisha rasmi pendekezo la kupeleka sehemu kubwa ya pato lake kwenye Serikali za Mitaa kwa ajili ya maendeleo ya wananchi kwa kutumia vigezo maalum. Utaratibu huo ambao utaanza kutumika mwaka 2004/2005, utasaidia kuhakikisha kuwa na fedha kwa ajili ya maendeleo ya wananchi zinagawiwa kwa uwazi na kwa kuzingatia hali halisi ya mahitaji ya huduma.

Mheshimiwa Spika, uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa ngazi za vitongoji, vijiji na mitaa utafanyika mwezi Novemba, 2004. Wadau wote wa uchaguzi huo wameshirikishwa kikamilifu katika maandalizi yake. Kazi kubwa iliyopo kwa muda mfupi uliobaki ni kutoa elimu kwa wananchi kuhusu uchaguzi huo ili tuendelee kuimarisha demokrasia katika ngazi zote. Jukumu hilo siyo la Serikali peke yake, bali ni la wadau wote. Matarajio yetu ni kuwa vyama vyote vyenye usajili wa kudumu vitashiriki kikamilifu katika uchaguzi huo kama ilivyokuwa kwa uchaguzi wa mwaka 1999. Napenda kutoa wito kwa wadau kushirikiana na Serikali ili chaguzi hizo ziweze kuendeshwa kwa uhuru na haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha programu ya ustawishaji Makao Makuu kwa kuweka mazingira bora ya uendelezaji kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2003/2004, jumla ya viwanja 6,500 vimeainishwa katika maeneo mbalimbali ya mji wa Dodoma. Kati ya viwanja hivyo, 3,000 tayari vimepimwa na kugawiwa. Aidha, vibali 300 vya uendelezaji vimetolewa vikiwemo vya ujenzi wa nyumba 300 za makazi ya Serikali katika eneo la Mwangaza, hospitali kubwa inayojengwa na wafadhili wa Marekani kwa kushirikiana na Kanisa la Kilutheri, Ukumbi wa Bunge na mradi wa ujenzi wa nyumba za makazi za gharama nafuu zinazojengwa kwa vikundi vya kuchangiana unaofadhiliwa na Shirika la *Habitat for Humanity* maeneo ya Chidachi na Kisasa. Juhudi pia zinafanywa kuwawezesha wananchi wote waliojenga bila kupewa viwanja katika maeneo ya *Oysterbay*, Mailimbili, Chang'ombe na Mnadani kupimiwa na kupewa hati za kumiliki viwanja vyao. Zoezi hilo linatekelezwa kwa kuwashirikisha wananchi katika kupanga na kuchangia gharama na zaidi ya shilingi 60 milioni zimechangwa. Katika mwaka 2004/2005, viwanja 10,000 vitapimwa na matayarisho ya eneo la Mnara wa Nyerere katikati ya mji yataanza.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano na uhusiano kati ya nchi yetu na nchi nyingine rafiki pamoja na mashirika mbalimbali ya kimataifa ulikuwa mzuri kwa kipindi chote cha mwaka 2003/2004. Tumeshirikiana vizuri na nchi jirani na za kikanda, wanachama wa Umoja wa Afrika, Umoja wa Mataifa na Mashirika ya Kimataifa kama vile Benki ya

Dunia, Shirika la Fedha Duniani na Benki ya Maendeleo ya Afrika. Nchi yetu imeshiriki kikamilifu katika majadiliano ya kuundwa kwa Kamisheni ya Umoja wa Afrika ambapo Mtanzania mwenzetu, Ndugu Rosebud Kurwijila, aliteuliwa kuwa Kamishna anayeshughulikia Idara ya Maendeleo Vijiji na Kilimo. Nampongeza kwa uteuzi alioupara. Nchi yetu imeshiriki pia katika kuanzisha Baraza la Usalama la Umoja wa Afrika ambalo liliundwa rasmi mwezi Machi, 2004. Hali kadhalika tulishiriki kikamilifu katika uanzishwaji wa Bunge la Afrika ambapo Bunge lako Tukufu liliwachagua Waheshimiwa Dr. William Shija (Mb.), Dr. Amani Kaborou (Mb.), Balozi Getrude Mongella, (Mb.), Remidius E. Kissassi (Mb.) na Athumani Janguo (Mb.) kuwa Wabunge wa Bunge hilo. Bunge hilo lilizinduliwa rasmi mwezi Machi, 2004 na kumchagua Balozi Getrude Mongella, (Mb.) kuwa Rais wake wa kwanza. Nachukua nafasi hii kumpongeza tena Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella na Wabunge wote waliochaguliwa kuwa wajumbe wa Bunge hilo anzilishi la Afrika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania imeendelea kuwa mstari wa mbele katika kuimarisha ushirikiano wa nchi tatu wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mwezi Machi, 2004, viongozi wa Jumuiya hiyo walitia saini itifaki ya mkataba wa kuanzisha Umoja wa Ushuru wa Forodha baina ya nchi wanachama mjini Arusha. Itifaki hiyo inasubiri kuridhiwa na nchi wanachama, ili iweze kuanza kutumika rasmi. Chini ya itifaki hiyo, bidhaa zinazozalishwa Tanzania zitauzwa katika nchi wanachama bila ushuru wa forodha. Ni muhimu kwa jumuiya ya wafanyabiashara na wananchi kwa jumla, kuijandaa kutumia fursa inayotolewa na mkataba huo kwa kutafuta masoko katika nchi za Uganda na Kenya.

Mheshimiwa Spika, Tanzania pia ni mwanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika. Mwezi Agosti 2003, Tanzania ilikuwa mwenyeji wa mkutano wa kilele wa viongozi wa umaja huo ambapo Rais Benjamin Mkapa alichukua uenyekiti. Mkutano huo uliridhia mkakati wa maendeleo katika eneo la nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika na kuyawekea kipaumbele masuala ya kushughulikia ambayo ni kujitosheleza kwa chakula, kukabiliana na janga la UKIMWI na kudumisha utawala bora.

Katika kutekeleza mojawapo ya *agenda* hizo, mwezi Mei, 2004, Tanzania iliitisha mkutano maalum wa wakuu wa nchi wanachama kuijwekea mikakati ya muda mfupi na mrefu ya kuongeza kasi ya uzalishaji na uhakika na upatikanaji wa chakula, ili tuondokane na baa la njaa. Mojawapo ya mikakati ya muda mfupi ni kuhakikisha upatikanaji wa pembejeo na zana za kilimo, ikiwemo mbolea, madawa na mbegu bora ifikapo 2006. Mikakati ya muda mrefu ni pamoja na nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika kutenga asilimia isiyopungua 10 ya bajeti zao za mwaka ili kuendeleza kilimo. Napenda nitumie fursa hii kumpongeza Rais Benjamin Mkapa kwa uongozi wake imara na thabiti kwa Jumuiya hiyo wakati huu ambapo ye ye ni Mwenyekiti. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika nyanja hizo hizo za kimataifa, Tanzania imeendelea kutoa mchango wake katika kutafuta amani na maendeleo duniani. Kwa miaka miwili, Rais Benjamin William Mkapa, alikuwa Mwenyekiti Mwenza wa Tume ya Kimataifa

Kuhusu Masuala ya Kijamii katika Utandawazi. Tume hiyo ilikabidhi rasmi ripoti yake kwa Shirika la Kazi Duniani huko Geneva, Uswisi, mwezi Machi, 2004. Pamoja na mambo mengine, ripoti hiyo imebainisha jinsi utandawazi ulivytengua na kupunguza sana umuhimu wa mipaka kati ya nchi na nchi na kati ya dola na dola. Badala yake utandawazi umeongeza mwingiliano na ushirikiano mionganoni mwa watu wengi zaidi duniani kuelekea kwenye jamii moja ya kimataifa. Ripoti imebainisha pia kuwa japo utandawazi una manufaa makubwa, bado haujatumiwa kikamilifu. Linalosisitizwa na ripoti hiyo ni umuhimu wa utandawazi kuanzia katika nchi zetu wenyewe. Jukumu letu la msingi ni kuweka mazingira bora kitaifa ya kukuza uchumi, kuongeza ajira na uwezo wa kupambana na umaskini. Kwa namna hiyo tutafaidi matunda ya utandawazi na kupunguza athari zake. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge kusoma ripoti hiyo na kuendeleza mijadala ya jinsi ambavyo tunaweza kutekeleza mapendekezo ya Tume hiyo.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu pia inaendelea na juhudu za kumaliza migogoro ya kisiasa katika Ukanda wa Nchi za Maziwa Makuu. Juhudi kubwa zimeelekezwa katika nchi za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ambazo zimekumbwa na migogoro ya kisiasa ya muda mrefu. Mpaka sasa kuna matumaini makubwa ya kupatikana kwa amani ya kudumu katika nchi hizo. Nchini Burundi, amani imeanza kurejea ingawa bado ipo milipuko ya mapigano ya hapa na pale. Hali ya amani katika Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo pia inatia matumaini kufuatia kuanzishwa kwa Serikali ya Mpito inayoongozwa na Rais Joseph Kabila na Makamu wa Rais wanne. Ili kuhakikisha amani ya kudumu inapatikana katika eneo la Maziwa Makuu, Tanzania inatarajia kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Maziwa Makuu utakaofanyika mwezi Novembra, 2004.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la mkutano huo ni kuzungumzia masuala ya amani na usalama, haki za binadamu na utawala bora, maendeleo na umoja wa kiuchumi wa nchi za kanda, maendeleo ya kijamii na misaada ya kibinadamu. Kuwepo kwa amani katika nchi hizo kutaisaidia Tanzania kwani wakimbizi walioko amba ni mzigo mkubwa kwa wananchi na Serikali, watarejea makwao na hivyo kuiwezesha nchi yetu kutumia rasilimali yake adimu kwa maendeleo ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwezi Aprili, 2004, Mabalozi wanaowakilisha Tanzania nje, walikutana huko Ngorongoro kwa lengo la kujifunza na kubadilishana mawazo na viongozi na watendaji mbalimbali kuhusu masuala ya kisiasa, kiuchumi na kijamii yatakayowawezesha kuiwakilisha vyema nchi yetu. Mkutano huo ulitoa mwelekeo wa siasa yetu ya nje kulingana na mazingira ya sasa ya utandawazi. Mwelekeo huo unazingatia zaidi masuala ya uchumi na uwekezaji. Siasa yetu ya nje inatokana na mahitaji ya maendeleo yetu ya ndani ambayo yataletwa kwa kuwekeza zaidi katika sekta za uchumi na huduma za kijamii, kumudu ushindani na kuweza kupata soko la bidhaa zetu mbalimbali. Tunahitaji kuwa makini zaidi kuzishawishi Serikali za nje na sekta binafsi ili tupate mitaji na wawekezaji. Mabalozi wetu wamepewa maelezo kuhusu mwelekeo huo wa sera yetu ya nje na watautumia kama mwongozo wa utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inaendelea kuathirika kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia, hali ambayo kwa sehemu kubwa imesababishwa na hali ya vita katika Mashariki ya Kati ambapo ndipo mafuta mengi huzalishwa. Hali hiyo imesababisha gharama za huduma mbalimbali kupanda na wananchi kuilalamikia Serikali na hata wakati mwingine kuzigomea huduma hizo. Upandaji ghafla wa bei za sukari, petroli, dizeli, mafuta ya taa, nauli na gharama za usafirishaji ni baadhi tu ya mifano hiyo. Serikali itafanya kila linalowezekana ili kupunguza makali ya athari hizo, lakini Watanzania ni vyema tufahamu kwamba kama bei hizo hazitashuka katika soko la dunia ni dhahiri zitaathiri sana uchumi wetu. Hata hivyo, endapo itadhiihirika kuwa wapo wafanyabiashara wanaotumia hali hiyo kujipandishia bei kiholela bila uwiano na bei za soko la dunia, Serikali haitasita kuingilia kati na kuwachukulia hatua wahusika hao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na matukio hayo bado kwa vigezo vingi uchumi wa Tanzania unakua vizuri, ingawa haujafikia kiwango kizuri cha kukidhi mahitaji yetu ya msingi ndiyo maana ni tegemezi. Hivi sasa huduma zetu za jamii zimeboreka kwa kiasi kikubwa na tunasifiwa kimataifa. Fedha tulizopata katika mpango wa *HIPC* tulizielekeza katika sekta muhimu za huduma za jamii na kuondoa umaskini. Ili huduma hizo zisiporomoke tena, hatuna budi kujenga uchumi unaojitegemea. Hivyo, ni lazima juhudu sasa zielekezwe katika kuongeza uzalishaji wa bidhaa, usindikaji wa mazao na mauzo nje ya nchi. Wakati tunaboresha huduma za jamii ni vema tukaangalia pia ujenzi wa utajiri nchini. Tukumbuke kuwa uwekezaji katika huduma za jamii kama vile elimu, afya, maji na barabara ni wa gharama kubwa na manufaa yake huchukua muda mrefu kuonekana. Ili nchi iweze kubeba mzigo huo bila kutetereka, ni lazima iwe na uwezo wake wa ndani wa kugharamia huduma hizo bila kutegemea wahisani. Hivyo, inatakiwa mipango yetu ilenje katika kukuza uchumi ambaa utabeba huduma hizo na nyinezo.

Mheshimiwa Spika, kilimo ni eneo moja muhimu sana linalotegemewa kwa sehemu kubwa katika ukuaji wa uchumi na maisha ya watu wetu. Pato la Taifa linategemea kilimo kwa asilimia 45 na kwa fedha za kigeni kilimo kinategemewa kwa asilimia 75.

Aidha, Watanzania zaidi ya asilimia 80 wanategemea kilimo kwa maisha yao. Umuhimu wa kilimo upo katika sehemu tatu. Kwanza, ni katika upatikanaji endelevu wa chakula. Taifa lolote ambalo halina uhakika wa upatikanaji wa chakula kwa watu wake haliwezi kutabiri matokeo ya mipango yake ya maendeleo.

Aidha, kutokuwa na chakula huyumbisha sana vigezo muhimu vya uchumi kama ukuaji wa Pato la Taifa na mfumuko wa bei, kama tulivyoshuhudia kwa nchi yetu. Hivyo, kuwa na uhakika wa chakula kwa wananchi ni msingi muhimu wa kujenga uchumi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili muhimu ni kuongeza uzalishaji na ubora wa mazao ya kuuza nje katika masoko ya kimataifa. Masoko hayo kwa mazao ya kilimo yanazidi kuwa na ushindani mkubwa sana na ili kuzalisha na kupata faida hatuna budi kuongeza uzalishaji kwa ekari na kuongeza ubora wa mazao.

Aidha, wataalam wetu wa kilimo na masoko wawasaidie wakulima kutambua aina ya mazao ya kilimo na upatikanaji wa masoko yake. Haina maana kung'ang'ania kulima zao ambalo linawapa wakulima hasara wakati yapo mazao mengine ambayo endapo yatalimwa, yataleta faida kubwa zaidi kwa wakulima.

Lazima tuwafundishe wakulima wetu kilimo cha biashara. Sehemu ya tatu muhimu ni kuwa kilimo lazima kitoe malighafi kwa baadhi ya viwanda vyetu. Kwa kufanya hivyo, viwanda vyetu vitapata malighafi ndani ya nchi, mazao yetu ya kilimo yatabadilishwa na kuwa bidhaa zitakazouzwa nje na kutuletea faida kubwa zaidi na wakulima wetu watafaidika zaidi na jasho lao. Kilimo kinachoweza kukidhi vigezo hivyo ni lazima kiwe cha kisasa kinachotumia teknolojia ya kisasa, pembejeo za kutosha na utaalam wa kuaminika. Ili kupata mafanikio kwa haraka, ni lazima tukubali kuwa kilimo cha mashamba ya kati hadi makubwa kina nafasi ya pekee. Watanzania wenye uwezo na wanaotaka kulima mashamba makubwa, watapewa nafasi na kusaidiwa kufanya hivyo kwa kuzingatia taratibu na sheria ya ardhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine muhimu ni la uzalishaji viwandani. Ni lazima tuzalishe bidhaa kwa ajili ya soko la ndani na hasa soko la nje. Nchi yoyote yenye mwelekeo mzuri wa maendeleo ni lazima ikuze sekta ya viwanda ili iweze kuuza bidhaa zake nje, kuipatia Serikali mapato na kuwapatia watu ajira. Viwanda vyta kusindika mazao ya kilimo ni lazima vipewe kipaumbele.

Hapa ni vyema tukahimiza usindikaji kuanzia viwanda vidogo, vyta kati hadi vikubwa. Eneo hilo lina umuhimu wa pekee kwa sababu siyo tu hutoa nafasi nyingi za ajira, lakini pia huzuia uharibifu mkubwa wa mazao kama matunda jambo ambalo mara kwa mara huwapa wakulima hasara kubwa. Usindikaji wa mazao pia ni muhimu sana kuongeza thamani ya bidhaa za kilimo ili kuwanufaisha wakulima.

Mheshimiwa Spika, eneo linaloambatana na hayo yote ni kukuza uuza nje wa bidhaa zetu. Katika ulimwengu wa soko huria, tusipouza bidhaa tutabaki kuwa soko la wengine na hatutaweza kuzuia hali hiyo kutokea. Hivyo, tujitahidi kuuza bidhaa nje kwa wingi. Tunazo bidhaa nyingi ambazo hazipatikani katika nchi nyingine kama vile bidhaa za kilimo, misitu, samaki na madini.

Tukitumia vyema bidhaa tulizonazo tutakuwa na nafasi nzuri ya kushinda katika masoko yetu ya kanda na hata nje ya Bara letu. Watanzania tunayo nafasi nzuri ya kukuza uchumi wetu kama tutatumia fursa zilizoko vizuri. Soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki na Soko la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ni mahali pazuri pa kuanzia. Tuingie katika masoko hayo na ya nje ya kanda zetu na tushindane bila woga. Tukiweza kushindana na kufanikiwa kuuza bidhaa zetu tutakuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, ili Serikali yoyote itekeleze majukumu yake, inahitaji uwezo wa kifedha na raslimali nyingine. Hivyo, nchi yetu lazima iendelee kuongeza mapato yake ili iweze kujitegemea zaidi. Serikali itaendelea kuimarisha Mamlaka ya Mapato Tanzania ili tusirudi nyuma katika makusanyo yetu.

Ili kusimamia jambo hilo, Bunge lako Tukufu lilipitisha Muswada wa Sheria ya Kodi ya Mapato wa mwaka 2004. Kwa kutumia sheria hiyo na nyingine zilizopo, matumaini yetu ni kuwa makusanyo ya kodi yataongezeka. Elimu kuhusu umuhimu wa kila mtu kulipa kodi, itaendelea kutolewa na wigo wa kodi utapanuka hatua kwa hatua. Mianya yote ya ukwepaji kodi ikiwa ni pamoja na utoaji na upokeaji rushwa itapigwa vita kwa nguvu zote. Sambamba na kuongeza mapato, matumizi nayo yatasimamiwa kikamilifu kama yalivyoidhinishwa na Bung lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Watanzania tunayo nafasi ya kufanya vizuri kama tutasimamia maeneo haya muhimu ya uchumi. Luga ya kila Mtanzania iwe nifanye nini kupata fedha zaidi kihalali na kupata ziada ili kuwekeza katika maendeleo ya familia yangu. Kwa mkulima mawazo yawe nilime nini na kwa utaratibu na ufanisi gani ili nipaye mazao zaidi na ziada ya kuuza. Wafanyabiashara nao wauze bidhaa zao hivyo hivyo. Twende katika masoko ya Kenya, Uganda na nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika tuone nini tunaweza kuuza kwa sababu sasa bidhaa za asili ya Tanzania hazina kodi. Wale wenye upeo mpana zaidi waende katika masoko ya nchi nyingine za nje na kushiriki katika biashara.

Tusiogope kukosea, lakini tujihadhari kupata hasara kubwa zinazoweza kutukatisha tamaa kibashara. Tuwe tayari kujifunza ikibidi kwa kuijunga na waliotutangulia na kufanikiwa katika biashara zao. Waheshimiwa Wabunge, hakuna wa kutuondoa katika umaskini isipokuwa sisi Watanzania wenyewe. Tufanye kazi kwa bidii na maarifa na tutafanikiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, maendeleo mazuri ya uchumi wetu yanatokana na mazingira ya amani na utulivu tuliyonayo nchini. Yapo matukio yenye dalili za kuchafua utulivu wetu. Matukio hayo hujitokeza zaidi wakati chaguzi zinapokaribia. Mwaka huu tutakuwa na uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambapo Serikali za ngazi hizo zitachaguliwa. Mwaka 2005 tutakuwa na Uchaguzi Mkuu.

Natoa wito kwa viongozi wa vyama vyote vya siasa wakemee hali za vurugu zinapoitokeza kwa wanachama au washabiki wao. Wananchi wapewe elimu ya siasa ili kuepuka uchochezi na chuki ndani ya jamii. Serikali haitavumilia mtu au kikundi cha watu ambao wanafanya vitendo vya uvunjifu wa amani. Amani ni raslimali kubwa kwa kuendeleza uchumi wa Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya utekelezaji wa shughuli za Serikali ni matokeo ya uongozi wa pamoja na mshikamano mkubwa wa viongozi na watumishi wa umma.

Napenda kuwashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa kutekeleza majukumu yao ya kitaifa kwa ufanisi. Aidha, nawashukuru wafanyakazi wote wa Serikali na taasisi zake chini ya uongozi wa Katibu Mkuu Kiongozi, Bwana Marten Lumbanga, pamoja na vyombo vyote vya dola kwa kutekeleza majukumu yao kikamilifu na hivyo kuiwezesha Serikali kutoa huduma zake kwa wananchi kama ilivyopangwa.

Aidha, nawashukuru kwa kuiwezesha Serikali kukamilisha maandalizi yote ya Bajeti yake ya mwaka 2004/2005, pamoja na makadirio ya matumizi ya fedha ya kila wizara, mikoa, taasisi na idara zinazojitegemea. Nawashukuru Watanzania wote na Washirika wetu wa Maendeleo kwa michango yao ambayo ndiyo imeiwezesha Serikali kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu imeweza kutekeleza majukumu yake kikamilifu kutokana na ushirikiano mkubwa kati ya viongozi kwa upande mmoja na kati ya viongozi na wafanyakazi kwa upande mwingine. Kwa sababu hiyo, napenda kwa namna ya pekee niwashukuru Mheshimiwa William Lukuvi, Waziri wa Nchi (Sera) na Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Waziri wa Nchi (Habari na Siasa) kwa msada mkubwa na ushirikiano walionipa katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, chini ya uongozi wa Katibu Mkuu, Bibi Rose Lugembe, kwa ushauri wao wa kitaalam ambao wamenipa mimi na Mawaziri wa Nchi katika ofisi yangu. Aidha, nawashukuru kwa kukamilisha maandalizi yote ya Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2004/2005. Namshukuru Mpiga Chapa wa Serikali kwa kuichapa hotuba hii kwa unadhifu na kwa wakati. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, nchi yetu imepata misaada na mikopo kutoka kwa wahisani mbalimbali. Misaada na mikopo hiyo imetoka kwa nchi rafiki, nchi fadhibili, Taasisi za Fedha za Kimataifa, Mashirika ya Umoja wa Mataifa, mifuko mbalimbali duniani, madhehebu ya dini na asasi zisizo za ki-serikali.

Misaada na mikopo hiyo imechangia sana katika kutekeleza miradi ya maendeleo na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi. Napenda kuwashukuru wote kwa dhati na kuwahakikisha kuwa Watanzania tunathamini misaada na mikopo yao na tutaendelea kushirikiana nao katika jitihada za kuondoa umaskini na kujenga uchumi imara. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2004/2005, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake pamoja na Ofisi ya Bunge, inaomba jumla ya shilingi 76,184,477,800 kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo. Kati ya fedha hizo, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake inaomba jumla ya shilingi 59,544,419,100 na Ofisi ya Bunge inaomba jumla ya shilingi 16,640,058,700.

Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake inaomba jumla ya shilingi 41,078,378,800 kwa ajili ya kugharimia miradi ya maendeleo. Kati ya hizo, shilingi 2,000,000,000 ni fedha za hapa nchini na shilingi 39,078,378,800 ni fedha za nje. Ofisi ya Bunge inaomba jumla ya shilingi 1,899,913,000 fedha za hapa kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofit*)

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea ingawa tuna sera ya kutokuwakaribisha Watanzania katika *gallery* za Bunge letu, lakini ningependa kutambua kuwepo kwa Viongozi wa Serikali, Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa ambao wako kwenye *gallery* na tutakuwa nao kwa wiki nzima hii. (*Makofi*)

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni namba 81 kifungu kidogo cha kwanza cha Kanuni za Bunge 2004, naomba kuwasilisha taarifa na maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na kuliomba Bunge lako Tukufu lipokee na kuijadili.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati hii walioshiriki katika kazi hii ni hawa wafuatao:- Mheshimiwa Athumanji Janguo - Mwenyekiti, Mheshimiwa George Lubeleje - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Chifu Abdallah Fundikira, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Rosemary Nyerere, Mheshimiwa Mwanne Mcemba, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Juma N'hunga, Mheshimiwa Khamis Salum Ali, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai , Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Ramadhani Hashim Khalfan, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Pascal Degera na Mheshimiwa Nimrod Mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tarehe 27 Mei, 2004 Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ilikutana Jijini Dar es Salaam, kuititia na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Mipango ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2003/2004 na Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005. Taarifa hiyo iliwasilishwa na Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib (Mbunge); Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Habari na Siasa.

Mafungu yaliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ni Fungu 25 Waziri Mkuu, Fungu 27 Msajili wa Vyama vya Siasa, Fungu 37 Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 42 Ufisi ya Spika, Fungu 54 Redio Tanzania, Fungu 61 Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Fungu 91 Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevyta na Fungu 92 Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha unaomalizika, Kamati yangu ilitoa ushauri na maagizo katika maeneo kadhaa ambayo yalilenga kuboresha utendaji kazi wa ofisi hii muhimu sana hapa nchini. Ninafurahi kuliarifu Bunge hili kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu imeyafanya kazi maeneo karibu yote na hatua kadhaa za kiutekelezaji zimeonekana. Aidha, pale ambapo Wajumbe walihitaji ufanuzi, maelezo yalitolewa kwa kina. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kwamba kwa mwaka wa fedha unaomalizika, Ofisi ya Waziri Mkuu iliidhinishiwa kwa mafungu yote kiasi cha Sh.64,340,671,200/= kati ya hizo Sh.20,094,794,900/= zikiwa ni kwa mpango wa maendeleo na Sh. 44,245,876,300/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake zimefanikiwa katika utekelezaji wa: -

- (i) Kuratibu misaada ya maafa mbalimbali yaliyotokea nchini.
- (ii) Kukamilisha Sera ya Maafa.
- (iii) Kukamilisha Sera ya Habari na Utangazaji ambayo tayari imezinduliwa.
- (iv) Kukamilisha ujenzi wa *Satellite Uplink* ya Televisheni ya Taifa ili matangazo yake yaonekane nchi nzima
- (v) Kukamilisha ujenzi wa vituo vya kurushia matangazo Mikoa ya Arusha, Dodoma na Mwanza.
- (vi) Taasisi ndogo ndogo za kifenda vijiji zimepewa mafunzo kuhusu namna bora ya kutunza vitabu, kuweka akiba na kambo ya jinsia.
- (vii) Viwanja 300 vimepimwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Serikali hapa Dodoma.
- (viii) Uzinduzi wa jengo la Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa huko Zanzibar na ukarabati wa Ofisi ya Bunge Dar es Salaam.
- (ix) Mafunzo ya uraia yametolewa kwa Viongozi wa Vyama vya Siasa ngazi ya Mikoa na Wilaya.
- (x) Maandalizi ya Daftari la Kudumu la Wapiga kura zikiwemo semina ya wadau na Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa ujumla imeridhishwa na jinsi Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi za chini yake zilivyotekeliza majukumu yao hususan kwa kuzingatia ushauri ambaa umekuwa ukitolewa na Wajumbe wa Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake ya kusimamia, kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Serikali, Kamati imeambiwa kuwa mpango wa maendeleo wa mwaka 2004/2005 wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake una malengo yafuatayo:-

- (i) Kuandaa mazingira mazuri ya kustawisha na kuendeleza Vyombo vya Habari vya Umma yaani Taaasisi ya Utangazaji Tanzania.
- (ii) Kuratibu na kuendeleza mikakati ya kupambana na UKIMWI.
- (iii) Kuboresha mandhari na miundombinu ya Makao Makuu Dodoma.
- (iv) Kuratibu utekelezaji wa program za huduma za kifedha vijijini na uendelezaji wa mifuko ya masoko ya kilimo nchini; na
- (v) Kukarabati Ofisi ya Bunge Dar es Salaam na kukamilisha ujenzi wa Ofisi Ndogo ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2004/2005, Kamati yangu imetoa maoni na ushauri katika maeneo kadhaa. Ushauri wa Kamati umelenga kuboresha ushauri na maagizo tuliyoyatoa katika mwaka wa fedha unaomalizika na kuangalia mapungufu yaliyojitekeza wakati wa kujadili Bajeti ya ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango wa kuhamia Makao Makuu Dodoma, Kamati yangu baada ya kutafakari maendeleo ya mpango huu imeagiza Ofisi ya Waziri Mkuu kuwa na ratiba ya utekelezaji wa shughuli zote za kuhamia Dodoma awamu kwa awamu, ratiba hii iwe wazi ikionyesha Wizara/Taasisi zinazohamia Dodoma na ni lini. Aidha, katika kutekeleza hilo, Serikali imeagizwa kuweka kipaumbele katika kuimarisha Taasisi zilizokwishahamia Dodoma kama vile Bunge.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Kamati yangu imeagiza Serikali iangalie namna nzuri ya kuhuisha Katiba ya Jamhuri ya Muungano na ile ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuhusu utaratibu mzuri wa kuandaa Daftari la Kudumu la Wapigakura katika chaguzi zote za Muungano na Tanzania Visiwani.

Mheshimiwa Spika, katika suala la maafa hapa nchini, Kamati yangu inasisitiza kuwa Serikali iwe inazingatia na kufanya kazi taarifa za majanga katika maeneo mbalimbali ili yaweze kudhibitiwa mapema, hususan janga la njaa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Televisheni ya Taifa, Kamati imebaini kuwa majengo ya chombo hiki bado ni chakavu, hivyo inashauri Serikali iweke mkakati wa makusudi wa kukarabati na kumalizia ujenzi wa majengo ya chombo hiki muhimu kwa umma. Aidha, Kamati yangu imefurahishwa na hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali kuwezesha Televisheni ya Taifa ionekane nchi nzima. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuridhishwa na utendaji katika mipango ya utangazaji katika Redio Tanzania, Kamati imebaini kasoro katika matumizi ya lugha sanifu hasa katika taarifa za habari, hivyo Kamati inaishauri Serikali kuusositizia uongozi wa Redio Tanzania kusositiza na kusimamia matumizi ya lugha sanifu katika taarifa za habari.

Kuhusu usikivu wa chombo hiki muhimu, Kamati yangu inaisisitizia Serikali iendelee kuchukua hatua za makusudi za ukarabati wa mitambo ya utangazaji iliyoko maeneo mbalimbali hapa nchini ili redio hii iweze kutoa matangazo yenyewe usikivu mzuri kote nchini. Aidha, Kamati yangu inaikumbusha Serikali kuhusu uboreshaji wa maslahi ya Watumishi wa Redio Tanzania na Televisheni ya Taifa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ili kuinua na kuimarisha hadhi ya Vyama vya Siasa hapa nchini, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaishauri Serikali kuangalia upya viwango vya ada ya usajili wa muda na kudumu kwa Vyama vya Siasa kwa maana ya kuzipandisha ada hizo ili zilingane na hadhi ya vyama hivyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ofisi ya Spika, Kamati yangu imeridhika na shughuli za ukarabati wa majengo ya Ofisi ya Bunge iliyopo Dar es Salaam na ujenzi wa jengo jipya la ofisi ndogo ya Zanzibar. Pamoja na hayo na kwa kuzingatia hali tete ya usalama duniani, Kamati inashauri ulinzi na usalama katika maeneo ya Bunge uimarishwe zaidi kwenye milango yote ya kuingia maeneo ya Bunge na ile ya ukumbi wa Bunge. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tume ya Taifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevyta, jengo la ofisi ya Tume hii bado haliridhishi, hivyo tunahimiza ukarabati uliokwishaanza uendelezwe na kukamilishwa ili watendaji wake waweze kutekeleza shughuli zao katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu iliombwa iidhinishe Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa mafungu yote kiasi cha Sh.120,062,800,600/=. Kati ya fedha hizo Sh.76,184,477,800/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh.43,878,374,800/= kwa ajili ya mpango wa maendeleo. Kamati yangu ilikubaliana na maombi ya fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kutoa maoni ya Kamati. Pia, niwashukuru Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib (Mbunge), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Habari na Siasa na Mheshimiwa William Lukuvi (Mbunge), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera), Mheshimiwa Andrew Chenge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ndugu Rajab Kilavo, Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, pamoja na wataalam wao kwa ushirikiano mkubwa waliotoa kwa Kamati yangu.

Aidha, nawashukuru kwa namna ya pekee Wajumbe wa Kamati hii ya Katiba, Sheria na Utawala kwa ushirikiano wao na mchango wao mzuri katika kipindi chote cha vikao vya Kamati. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, naishukuru Ofisi ya Katibu wa Bunge inayoongozwa na Ndugu Kipenka Mussa na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Ernest Zulu na Aggrey Nzowa, kwa kazi yao nzuri ya kuishauri na kuihudumia Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, naiunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE - KIONGOZI WA UPINZANI BUNGENI NA MSEMAJI MKUU KWA OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwa mwaka mwininge tena wa kujadili bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, nasimama hapa kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kutoa maoni yetu kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu Na. 43(5) (b) na (c) toleo la mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wake wote wawili na Wataalam kwa kutuwasilishia Bajeti yao, Bajeti ya kutuomba tuwape pesa Sh.120,062,800,600/= za kutekeleza na kusimamia mipango iliyopangwa chini ya ofisi yao kwa kipindi cha mwaka 2004/2005. Tunaelezwa kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu ndio yenyé jukumu la kuratibu na kusimamia kwa umakini na ufanisi shughuli zote za Serikali katika Sekta zote na ndani ya Bunge. Hivyo umakini na uchapakazi wa wale waliokabidhiwa kuisimamia kuiendesha ofisi hii ndicho kigezo na msingi mkuu wa kutekelezeka mipango yote inayopangwa na kuitishwa hata katika maeneo mengine ya Kiserikali. Ofisi ya Waziri Mkuu pia ndio yenyé kuhusika kikamilifu na shughuli za Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Ofisi ya Bunge, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevyaa na Tume ya Kudhibiti UKIMWI. Kwa ujumla wanayo kazi kubwa na tunawapongeza kwa yale ambayo wameweza kuyasimamia na kuyafanya mwaka wa bajeti uliopita. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mwaka jana wakati tunawasilisha maoni yetu kuhusu bajeti ya 2003/2004 tulisema na naomba kunukuu: “Kupongezana kwa bajeti nzuri iliyoadaliwa ni suala moja na kutekelezeka kwa bajeti hiyo ni suala jingine.” Kambi ya Upinzani mwaka jana iliikubali bajeti nzuri yenyé maneno matamu ya Mheshimiwa Basil Mramba kwa mtazamo wa “mtoto akililia wembe mpe.” Lakini kutokana na yale tuliyoyabaini sisi sote na hasa namna ya kutekelezeka baadhi ya yale tuliyointiwa humu Bungeni mwaka jana; mwaka huu Kambi ya Upinzani imeamua kuipigia bajeti kura ya kutokuwa upande wowote (*Abstain*). Kambi ya Upinzani siku zote inapenda kuwa wazi kuhusiana na umuhimu wa Bajeti kama sheria muhimu itungwayo kila mwaka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kura ya abstain yaani kutokuwa na upande, tunataka kuwashakikishia Watanzania kuwa yale machache mazuri yaliyoko katika Bajeti hatuyakatai, tunayaunga mkono na kusisitiza kuwa yasiishie kwenye makaratasibali yatekelezwe katika hali halisi na kwa umakini unaotakiwa. Yale ambayo ni geresha na danganya toto, tunayapinga na kuyakataa kwa nguvu zote pamoja na uchache wetu Bungeni. Hatuwezi kukubali Watanzania wauziwe mbuzi kwenye gunia! (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mathalan, Kambi ya Upinzani siku zote imedai kuwa elimu katika ngazi zote hadi Chuo Kikuu ni jukumu la Serikali na lazima iwe bure ili watoto wa Kitanzania wa kawaida au maskini wawe na fursa ya kupata elimu. Bajeti ya 2004/05 imeanza kutekeleza jambo hilo kwa kutenga jumla ya Sh.59,413,581,900/. Kambi ya Upinzani hatuna sababu ya kupinga jambo hilo ambalo siku zote tumekuwa tukilidai. (*Makofî*)

Vile vile, ufutwaji wa leseni za biashara na ushuru wa ttempu kwa biashara zenyenye mauzo yasiyozidi Shilingi milionii 20 na mfumo mpya wa kodi unaotegemea kama biashara husika itakuwa na kumbukumbu za kuridhisha au la na kutoa viwango maalum kwa biashara hizo ni mambo ambayo pia yatawasaidia kwa kiwango kikubwa wafanyabiashara. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kama ambavyo tumeshuhudia bajeti zilizopita, bajeti hii vile vile imejaa maneno mengi matamu yenye malengo mengi yasiyotekelezeka kama inavyokuwa miaka ya nyuma. Mathalan, mwaka wa fedha 2003/2004 kwa mbwembwe zote Waziri wa Fedha alitangaza kutenga fedha kwa ajili ya Mpango wa Zao la Biashara na Chakula kwa kila Wilaya. Tujiulize ni Wilaya ngapi zimepata fedha hizo? Mbona Waziri haongelei tena mafanikio ya mpango huo wa mwaka jana kabla ya kuendelea na huu unaozungumziwa? (*Makofî*)

Mpango wa pembejeo (mbolea) ulioahidiwa kwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini matokeo yake yalikuwaje? Mbona Serikali inapata kigugumizi kwa ahadi zilizopita na inakuwa nyepesi kutoa maneno matamu mapya? Uanzishwaji Benki ya Wakulima na mikopo yenye unafuu wa riba kwa wafanyabiashara wadogo ni dhana ya kufikirika tu, (*idealism*) kwani kutekelezeka kwake kumekaa kikushoto kushoto. Haielezwi chanzo cha kukwama mipango ya mikopo ya asilimia 10 ya bajeti za Halmashauri kwa vijana na akina mama na marejesho hafifu ya hata zile fedha zilizotolewa na Serikali Kuu. Mkakati wa wazi wa kumwondolea umaskini wa kipato Mtanzania wa kawaida haujaonekana bado. (*Makofî*)

Serikali imeendelea kutusomea utajiri wa takwimu kama vile wahusika hawaelewi kina cha umaskini uliokubuhu katika jamii yetu. Ukiachilia mbali takwimu zinazojikinzana zitolewazo na Taasisi tofauti kuzungumzia kupanda au kushuka kwa Pato la Mtanzania, ambapo kila mjenga hoja anachagua ni takwimu zipi za kutumia ili akidhi haja ya lile alilokusudia. Katika mtizamo wa jumla wa *ki-layman* ambao hauhitaji *TX* kutoka Ulaya, kwetu sisi kwa harakaharaka tutapima kuongezeka kwa kipato cha Mtanzania wa kawaida endapo namba ya wadau bila wenyewe kupenda wanalaazimika kuja Dodoma kuwasubiri Wabunge kwenye gate kuomba misaada ya fedha au kuamkia majumbani kwa Wabunge saa 11.00 alfajiri kuomba chochote itapungua, idadi ya watu wanaookoteza mabaki ya mifupa na nyama mnadani maili mbili kwa ajili ya kitoweo nyumbani itaanza kupotea, nyumba za kuwekewa zenge la udongo uliochanganywa na nyasi na mavi ya ng'ombe zitaanza kuwekezwa bati, watu watakapoacha kumpigia mgombea Ubunge, Udiwani au Urais kura kwa sababu ya kupewa mfuko wa chumvi wa Sh. 200/= au sahani ya pilau ama kopo moja la kangara au ulanzi, Watanzania walio wengi watakapomudu kupata milo miwili kwa siku tutaamini umaskini unapungua.

Kupotea kwa viashiria hivyo ambavyo kwa ujumla ndio umaskini wenyewe itakuwa ndio kielelezo sahihi cha kukua kwa uchumi wetu. Vinginevyo, tusidanganyane na kuendelea kucheza na maneno, hiyo haitamsaidia chochote Mtanzania fukara. (*Makofî*)

Pamoja na kufuta leseni za biashara kwa wale wenye mzunguko wa biashara (*Turnover*) wa chini ya Shilingi milioni 20 kwa mwaka kwa lengo la kuhamasisha na kuwapa motisha wafanyabiashara wadogo, Serikali haina mwelekeo wowote wa kuongeza uwezo wa mwananchi, mkulima na mfanyabiashara mdogo kuongeza uwezo wake wa kununua (*Purchasing Power*), ambayo ni jambo muhimu katika mapambano dhidi ya umaskini. Bila kuwalenga makusudi kwa maana ya kumwongezea uwezo, motisha na hamasa pekee kwa kuondoa tu ushuru wa leseni haina maana yoyote kwa wengi wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo ambayo tunaambiwa inatoa ajira kwa Watanzania asilimia zaidi ya 80 na pia kupewa jina zuri la kwamba ndiyo Sekta Kiongozi, bajeti hii haitamsaidia sana mkulima wa kawaida wa Kitanzania kwa vile hakuna mfumo wa kumsaidia moja kwa moja labda kuwa manamba. Punguzo la mara moja la asilimia 100 la gharama za kusafisha pori, ujenzi wa mifereji ya umwagiliaji, kupanda mazao ya kudumu na kutunza mazingira au mmomonyoko wa ardhi; mkulima wa kawaida wa Ranya hana taarifa na hayo mambo labda kama ataanzisha yeye mwenyewe kwa kutumia mtaji wake wa asili yaani nguvu yake, kilimo cha bangi na mirungi ambapo wanunu hutoa hata malipo ya awali kwa mkulima pindi anapoanza kutayarisha shamba. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, punguzo hili linawahu wakulima wakubwa, Waziri hakutaja specifically kuwa hata mkulima mdogo naye atanufaika na unafuu huo. Wakulima wetu bado wanatumia jembe la mkono, hawana mapori ya kufyeka, hata mashamba waliyonayo hayana hata hati wala mabwawa ya kujenga mifereji. Kwa kweli hii tunasema ni kuwadanganya wakulima.

Utaratibu huu au punguzo hili, sana sana linatoa motisha kwa wawekezaji wa nje na wenye nacho kujinyakulia zaidi maeneo makubwa na kupata misamaha iliyoidhinishwa. Jambo hili litaendelea kuwaondolea Watanzania wengi milki ya ardhi na itakuwa hatari huko tuendako. (*Makofi*)

Mipango yetu katika kilimo bado haiko sawa na nchi yetu itaendelea kupata tatizo la njaa mwaka hadi mwaka. Hata hizo pesa kidogo zilizotengwa kwa ajili ya Sekta ya Kilimo maadam hakuonekani mkakati madhubuti wa usimamizi, impact yake kwa mkulima wa kawaida haitaonekana na sana sana zitaishia kwenye urasimu. (*Makofi*)

Mkakati wetu wa kilimo bado haujajikita kwenye mahitaji/matakwa halisi ya wakulima wetu wa hali ya chini ambao ndiyo wengi. Tunashauri kwamba Serikali ianze kuweka mfumo shirikishi ambapo wakulima kwa kila ngazi na kwa kila mazingira yao husika wasaidiane na wataalam kuainisha mahitaji yao halisi yanayozingatia fursa waliyonayo na vizingiti vilivyopo.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyoeleza kwenye hotuba zetu zilizopita tunaendelea kukazia na kusisitiza kwamba hata uwe na bajeti nzuri vipi, hata uwe na mipango mizuri vipi kama mdudu rushwa anavinjari katika bajeti na mipango hiyo mizuri ni wazi

kutekelezeka kwa mipango mizima na bajeti nzima kutakuwa ni finyu na kwa matatizo. (*Makofi*)

Tarehe 17 Juni 2004, inaonekana Serikali ilikereheshwa na kelele za baadhi ya Wabunge wengi waliosimama kuchangia hotuba ya bajeti kwa kulalamikia vitendo vya rushwa na hivyo ikaamua kutoa kauli kuhusu hali ya Utawala Bora na Vita dhidi ya Rushwa. Ni vyema muwasilisha kauli kwa niaba ya Serikali, alitanabaisha utani alionao na baadhi ya wabunge aliowataja wanaotoka Musoma. Tunafikiri muwasilishaji alikuwa anaendeleza utani huo huo wa jadi katika kulielezea suala la rushwa. Vinginevyo, alidhamiria kutumia mbinu ya utani ili kuwachechesha Wabunge na kuwapunguzia hasira zao dhidi ya rushwa kubwa kama kwenye *IPTL, TTCL, TANESCO, NBC*, machimbo ya *Tanzanite* na kadhalika. Kama kweli alikuwa amedhamiria hayo aliyoyazungumza, basi tuna kazi kubwa mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali lazima itambue kwamba kama ambavyo utandawazi unavyobadilisha mwenendo na mfumo wa kiuchumi kidunia, hivyo hivyo na rushwa inajibadili sura na rangi mithiri ya kinyonga. Inasikitisha wakati Wabunge kwa nia njema wanapoitanabaishia Serikali yao kuhusu vitendo vya rushwa na ufisadi unaotendeka Serikalini, Serikali kwa upande wake inang'aka na kuwa mkali mithiri ya koboko, badala ya kuyachukua mawazo hayo kama changamoto ya kutengeneza mikakati thabiti ya kuishughulikia rushwa. Haileti maana yoyote ya kujisifia na kujilinganisha na nchi zingine zinazoendekeza rushwa. Hii ni sawa na marehemu aliyefariki leo kukejeli maiti aliyekwisha oza. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia ni lazima tutambue kwamba kuendelea kuwepo kwa rushwa kunategemea na mfumo uliopo wa kiutendaji na kiusimamizi. Kama mfumo ni *loose* na usimamizi hauko *determined* kuikabili rushwa, rushwa haiwezi kushughulikiwa ipasavyo na sana sana tutaendelea kushughulikia matokeo badala ya kukabili chanzo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, taswira ya rushwa inajibainisha kuitia mambo mbalimbali kama vile mikataba mibovu inayosainiwa na Serikali, uchaguzi ulioja hila na udanganyifu, upendeleo katika mgawanyo wa raslimali za Taifa, unyimaji haki raia, ufujaji mali ya umma na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, si ajabu hivi tunavyopitisha bajeti hizi, tayari kuna watu wana migao yao ya *percent or inflated figure* kwenye mafungu haya haya na mbaya zaidi kwa kuwa Bajeti hii ni ya kuelekea mwaka wa uchaguzi, si ajabu mafungu mengine yametayarishwa kuwasaidia baadhi ya watu kushinda uchaguzi mwaka 2005 au Chama fulani kushinda. (*Makofi*)

Hii ndiyo Rushwa Mama na nyingine zote ni *photocopy*. Maana mnawenza mkapitisha bajeti ya Shilingi trilioni 3.7 kumbe 1/3 ya bajeti nzima ni ulaji mtupu na nyingine nyingi zinapelekwa kuwapata wawakilishi feki wa Wananchi waliotokana na pesa hizo hizo za walalahoi. Rushwa ya namna hii ikishapewa nafasi kustawi, Serikali nzima lazima itatengeneza lugha ya kuyalinda mashina mengine ya rushwa. Lugha

itakuwa ya kulindanalindana maana kila mmoja ana mahala pake anapopakua. Nchi zenyenye kutapakaa rushwa watu wake na viongozi wake roho zao huwakaa juu juu kwa mtazamo wa kupata mgao kwa malipo yoyote yanayofanyika, takrima kwa maamuzi yoyote wanayotaka yafanyike. Mwisho wa yote atakayeishia kunawa bila kula na kuumia ni mwananchi wa tabaka la chini ambaye hana pa kushika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika. Rushwa inazidi kustawi kwa sababu hakuna uwajibikaji ndani ya Serikali. Hata Mheshimiwa Rais anawaonea haya watu wake kuwawajibisha. Uagizwaji computer mbovu Wizara ya Elimu kwa Shilingi milioni 290, kuungua kwa Ikulu, Mikataba ya *IPTL* na kadhalika, ni vielelezo halisi vya kulea rushwa na kutowajibika. Ni vyema kama tuko serious kuanzia sasa taarifa za *PCB* ziwasilishwe Bungeni na Kamati za Bunge ziwezeshwe kufanya uchunguzi maeneo yanayoshukiwa kuwa na rushwa, ubadhirifu na upotevu wa fedha vinginevyo, kwa kuwa Serikali ya CCM inaonekana kuanza kupata kigugumizi katika kuizungumzia na kuishughulikia rRushwa, tunazitaka Taasisi zinazohusika na rushwa ziwawekee Wapinzani takwimu na taarifa za rushwa sehemu nyeti ili zije zitusaidie mahala pa kuanzia pindi tukichukua nchi mwaka 2005. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nyaraka zilizoisaidia Serikali ya Rais Kibaki wa Kenya kukabiliana na ujisadi uliofanyika wakati wa Serikali ya Moi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu zoezi la kubinafsisha mali ya umma, inasikitisha Sera au mpango ambao tumeuamua sisi wenyewe, matokeo yake yawe ni kuwanyanya Watanzania wenyenye. Katika zoezi hili inashangaza kwamba kumetawaliwa na hali ya ubaguzi wa hali ya juu. Hakuna *Clear Policy* namna ya kushughulikia wafanyakazi wanaokuwa wamehusishwa katika zoezi hilo.

Tunatambua wazi kwamba mengi ya Mashirika hayo yaliliwa na Serikali yenyewe, inakuwaje Serikali inashindwa kukaa chini na wafanyakazi ikajadiliana kwa amani na wakafikia muafaka! Tumeshuhudia vurugu kubwa *TRC*, *TANESCO*, *NBC*, *NASACO* na sasa *Tanzania Elimu Supplies*, Serikali imefikia hatua ya kutoa taarifa yenyewe utata kuhusu *TES* eti wamefilisika wakati Serikali imeamua kujifilisi yenyewe yaani *Voluntary Liquidation*.

Tunaitaka Serikali ilete hapa Bungeni nyaraka zinazohusu hayo madeni makubwa ya *TES*. Kwa kweli tutakuwa hatuwatendei haki baadhi ya wafanyakazi wetu na hata mbele ya Mungu iwapo Serikali itatoa mafao kwa njia za kibaguzi au kwa kutegemea kutishika na unyeti wa eneo walilopo wafanyakazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kujibaraguza kwa Serikali, Kambi ya Upinzani bado inasimamia ukweli kwamba hakuna cha maana sana tunachopata kutohakana na madini na yote ikiwa inasababishwa na mikataba ya ovyo tulioingia na wawekezaji. Bado Serikali haiyaoni madini yetu kama mtaji tosha bali inaona na kuamini kwamba mtaji ni mashine au mitambo ya kuchimba madini na teknolojia basi! (*Makofi*)

Katika Kampuni ya Ashanti, Serikali ya Ghana inamiliki asilimia zaidi ya 25 ya hisa licha ya kulipwa mrahaba. Je, kulikuwa na ulazima gani wa kuchimba madini haya iwapo maandalizi yetu yalikuwa bado ni duni au bado sisi ni washamba wa Sekta hii? Mbona Hayati Baba wa Taifa alifanya subira na hakuthubutu kuingia kichwa kichwa shughuli hii ya madini? Nchi kama Namibia na Afrika Kusini, sheria imetamka wazi Kampuni inapochimba madini eneo husika, lazima pia ijenge barabara, mashule, hospitali pamoja na kuepuka uharibifu wa mazingira. Suala hili ni la kisheria na siyo la kihisani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, upo mkataba wa *MEREMETA Company* ambayo ilipoanza tuliambiwa inaundwa kama *Corporation Sole*, lakini hivi sasa haileweki iko wapi na inaendeshwaje na hata taarifa za *Auditor General* zinatia mashaka. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili *MEREMETA* imeandikishwa wapi, kwa mkataba upi na Taifa hili limepata kiasi gani kama mgawo wake?

Pia, Bunge liliwahi kuarifiwa kuwa *MEREMETA* inajishughulisha na kazi ya kununua dhahabu kutoka kwa wachimbaji wadogo wadogo, tunataka tuelezwe inakuwaje tena *MEREMETA* inaendesha uchimbaji badala ya kununua? (*Makofî*)

Kambi ya Upinzani, inaitaka Tume iliyoundwa kuchunguza suala hili la Sekta ya madini, Wasione Soo! kuishauri Serikali isiendolee kuingia mikataba mipyä ya uchimbaji madini mpaka hapo tutakapokuwa tumejipanga vizuri. Suala la kutoa Mrahaba kwa mamlaka ambako kunachimbwa madini hivi sasa lisiwe la mjadala, Serikali itoe utaratibu wa kuanza kutolewa Mrahaba huo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mfumko wa bei, kwenye vitabu inaonekana kuwa “inflation” imeshuka kutoka asilimia 20 mwaka 1995 hadi asilimia 15 ya sasa. Kupungua huko hakujatoa hali halisi na hali halisi ya Mtanzania wa kawaida. Bidhaa karibu zote (*Consumer prices*) katika kipindi hicho zimepanda badala ya kushuka.

Mfano, sukari imepanda toka Shs.300/- hadi Shs.700 hadi shs. 800 kwa kilo. Mafuta sasa hivi huko Bukoba yanafikia T.Shs.980/- kwa lita. Mheshimiwa Waziri Mkuu anajua fika kwamba bei ya mafuta ikipanda, pia inapandisha bei ya bidhaa na huduma. (*Makofî*)

Kwa kuwa Mtanzania anaendelea kuathirika na hali hii, kushuka kwa “Inflation” inabaki kuwa porojo au inawafaidisha tu wakubwa na matajiri wakubwa, hatuwezi kufurahia bajeti inayowanufaisha asilimia 10 tu ya Watanzania, wakati wengi wanahangaika namna ya kupata mlo wao wa siku. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa ni karibu asilimia 10 tu ya Watanzania ndio wananaufaika na umeme kwa nchi nzima, hata hao wachache wamefika mahali pa kurudi kutumia mkaa na kuni kutohana na kutoweza kuhimili tena gharama ya umeme. Kambi ya Upinzani, tumekuwa tukisisitiza matumizi ya nishati mbadala kama vile mkaa wa Mchuchuma au kutumia umeme wa upepo.

Mheshimiwa Spika, tutakuwa tunazungumzia uchumi wa nani kukua iwapo badala ya Watanzania, kufurahia matunda ya maendeleo kidogo yaliyopo, wanaomboleza na kuanza kurudi kwenye matumizi ya kuni na mkaa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hali ya kisiasa, msingi mkuu wa kudumishwa kwa hali ya amani na utulivu ndani ya nchi yetu ni kukubali misingi sahihi ya demokrasia ikafanya kazi yake. (*Makofi*)

Serikali zote mbili za CCM zinalo jukumu la kuhakikisha mazingira ya kuruhusu hali hiyo yanakuwepo. Watanzania wanahitaji uchaguzi ulio huru na haki kuwapata viongozi wao na wawakilishi wao. Wanahitaji kushiriki shughuli za kisiasa katika uwanka ulio huru na linganifu, bila kuwepo vitisho wala manyanyaso. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inaamini kuwa tofauti za kidini na kikabila hazitakuwa chanzo cha uvunjifu wa amani ndani ya nchi yetu kama yalivyo mataifa mengine bali itasababishwa na uvunjaji wa misingi sahihi ya demokrasia. (*Makofi*)

Hali iliyojitokeza katika chaguzi za Marudio huko Bariadi na Kilimanjaro ambapo nguvu za ziada za Kiserikali zilitumika na pia Viongozi wa CCM kuwashambulia Viongozi wa *CUF* na kuvunja gari lote vioo tena kwenye Kituo cha Polisi na vile vile Mbunge wa Moshi Vijijini Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Madiwani wake wa *TLP* kushambuliwa na kutaka kutekwa, hakutoi ishara nzuri huko tunakoelekea kwenye Uchaguzi wa Mitaa, Vitongoji na Vijiji na Uchaguzi Mkuu mwakani. Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi na Maafisa Watendaji ambao kama ambavyo tumeshuhudia wenyewe, wameanza kupokea matamko ya vitisho toka kwa baadhi ya Viongozi Wakuu wa Chama Tawala kwamba maeneo yao yakichukuliwa na Wapinzani, watakuwa wamejfukuzisha kazi.

Je, Vyama vya Upinzani navyo vikianza kubuni mikakati mbadala ya kujitafutia ushindi wa bandia hali itakuwa ya usalama kweli? Ni vyema tukubali kuzuia kuliko kuponya (*Makofi*)

Iwapo *PCB* imewezeshwa kuwa na mtandao wa ofisi zake hadi Wilayani, inashindikana nini Tume ya Uchaguzi, ambayo ndio chombo kikuu cha kusimamia na kuratibu upatikanaji watawala wa nchi hii kupewa fedha za kutosha zitakazoiwezesha kutengeneza mtandao wake kiusimamizi nchi nzima? Lazima Serikali ikubali kwamba demokrasia ina gharama zake. (*Makofi*)

Ni vyema Serikali ya CCM ikakubali na kuona umuhimu hivi sasa wa kuanza kuandaa mazingira yatakayowezesha makabidhiano ya madaraka baina ya Chama kinachokuwa madarakani na Chama kingine kipyra kinachokuwa kimeshinda uchaguzi kuliko kungojea mazingira ya kushtukiza ambayo hayawezi kutengeneza Serikali mpya endelevu na yenye maridhiano. Enzi za kuamini kuwa kuna mtu aliyeumbwa kutawala milele au Riwaya za akina marehemu Thabit Kombo, eti mtu kutoka eneo fulani hawezি

kutawala Zanzibar zimepitwa na wakati. Upepo wa mabadiliko ya kisiasa umethibitika katika nchi nyingi kwamba unaweza kuwa ndani ya siku hata tatu. (*Makofit*)

Ongezeko la Bajeti kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ambalo limetolewa litakuwa na maana endapo litatumika kuwaandaa Polisi kuhakikisha wanasimamia bila upendeleo, taratibu, kanuni na sheria zilizopo. Lakini wakigeuzwa makada wa vyama au wakereketwa na wakajiingiza kwenye ushabiki wa kisiasa na kuviona baadhi ya vyama au wanasiasa fulani sawa na makundi ya majambazi, nchi yetu inaweza kuingizwa katika janga ambalo halijawahi kuonekana tangu tupate uhuru. (*Makofit*)

Wizara ya TAMISEMI inapaswa isikilize kwa makini maoni mbalimbali yaliyotolewa na Vyama vya Siasa kuhusiana na marekebisho ya Kanuni zinazosimamia Chaguzi za Serikali za Mitaa. Hila zozote za kupangwa kimakusudi kwa minajiri ya kukifagilia Chama fulani kishinde kiulaini zinaweza kutupeleka pabaya kama sio watu kuondoana shingo. (*Makofit*)

Tume ya Uchaguzi ni vyema ikaongezewa uwakilishi toka Vyama vya Siasa kama ilivyo kwa wenzetu wa Kenya na Zanzibar ili kuleta hali ya kuaminiana na kuridhiana. Daftari la Kudumu la Wapiga Kura litayarishwe katika misingi iliyio ya wazi na sahihi. Tume iwezeshwe kuwa na watumishi wanaowajibika kwake moja kwa moja badala ya Wakurugenzi (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, fedha za ukimwi na maafa, tunapongeza Serikali imekuwa ikitenga mabilioni ya shillingi kwenye Kampeini dhidi ya Ukimwi kuititia *TACAIDS* na pia kwa mara ya kwanza imekitengea kitengo cha maafa fedha za kushughulikia maafa. Jambo la muhimu ni udhibiti mzuri wa fedha hizo kwani kumekuwepo na taarifa za matumizi mabaya ya fedha hizo.

Fedha za Ukimwi hivi sasa zielekezwe katika kuwahudumia walioathirika na Ukimwi na yatima. Kama ni Semina zimetosha, na sehemu nyingine semina hizo zimeanza kuwa chanzo cha watu kuendekeza vitendo vya ngono. Fedha za maafa zilizotengwa tunaomba ziwekewe utaratibu unaoeleweka wa kuyakabili maafa yanayotokea. Vinginevyo fungu hilo litageuzwa kimbilio la kumaliza yatakayoitwa maafa hata kwa yale mambo ya watu au makundi binafsi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, Serikali kuhamia Dodoma, pamoja na usemi usemao “mtu mzima hatishiwi nyau”. Kwa hili tunataka Serikali ya CCM ikubaliane na ukweli kwamba maamuzi ya kuhamishia shughuli zote za Serikali hapa Dodoma yameshindikana. Huo ndio uungwana na utawala wa ukweli na uwazi. Hivi sasa siyo siri, Mji wa Dar es Salaam, unakua kwa kasi na umekuwa ndio kitovu cha shughuli za Kitaifa na Kimataifa na katika uchumi huria ambao unamgusa kila mmoja wetu kwa kutegemea pale alipo, Mawaziri wetu na maafisa wao wamejikuta wakiwa mionganoni mwa washiriki na hatua ya wao kuhamia Dodoma imeonekana ni ya kujimaliza kiuchumi. Dodoma hakuna mtandao wa “deal” za kimapato na kibiashara. Huo ndiyo

ukweli. Tunawapongeza baadhi ya Wabunge wa CCM ambao wamekuwa wakiliweka wazi suala hili. (*Makofi*)

Pia tunawasikitikia na kuwasuta wale ambao mdomoni wamekuwa wakijifanya wako tayari kuhamia Dodoma, lakini kivitendo na kifikra wala hawako Dodoma na sana sana wanazidi kututia hasara. Kama Serikali ya CCM iko serious kuhamia Dodoma, basi sera hiyo itungwe sheria ili watakaoikiuka wavalishwe kaptula za jela. *Programme*, mikakati, vision na mengine mengi yanayoimbwa Bungeni havitawaondoa Waheshimiwa hawa Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hitimisho, ni jambo la faraja kwa Kambi ya Upinzani na ni msumari wa kuimaliza CCM, tunapotambua ukweli kwamba kipimo halisi cha maneno yote matamu ya hizi Bajeti zinazopitishwa mia kwa mia, ni mwakani kwani mafanikio ya mipango yote yanapaswa kuonekana kabla ya mwezi Julai 2005. Kambi ya Upinzani, inapongeza yale mazuri yanayofanywa na Serikali ya CCM, lakini tunasema mnafanya mazuri machache mno kuliko yale mengi mno ambayo yangefanywa na Serikali iliyo makini na iliyojipanga vizuri.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha ametamka mbele ya Bunge hili tukufu kwamba anayoyazungumza sio porojo, Tunapongeza. Lakini akumbuke njia ya mwongo huwa fupi. (*Makofi*)

Kila Mtanzania, aliyekuwa anafuutilia taarifa za vyombo vya habari atakuwa shahidi namna Wabunge wenzetu wengi wa Chama Tawala, katika michango yao walivyoichanachana hotuba ya Bajeti ya Serikali yao tena kwa ukali mithiri ya Faru. Lakini ilipofika wakati wa kupiga kura kama ulivyo usemi wa kihaya katika tafsiri ya Kiswahili kuwa, “maji moto yakakumbuka kurudi kwao kwenye ubaridi”, wakaenda tofauti na yaliyonenwa na vinywa vyao na bila shaka nafsi zao pia. (*Makofi*)

Tunaamini hiyo yote ni kutokana na mfumo tunaouona ni mbaya wa kufanya maamuzi Bungeni, ambao tunashauri ubadilishwe ili kura zipigwe kwa njia ya siri au Mbunge ahesabiwe kupinga au kukubali kwa kutegemea yale aliyoyanena kwa kiasi kikubwa katika mchango wake. Hizi *Public Address System* tunazotumia humu Bungeni zinatakiwa ziwe na *Option* ya *Voting* na tunaamini kuwa ipo. Kama hiyo haipo basi iwekwe kama Mabunge mengine badala ya njia tunayotumia inayowanyima Waheshimiwa Wabunge, uhuru na haki katika kufanya maamuzi, eti kwa ajili ya *Three Line Whip*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaitakia Ofisi ya Waziri Mkuu na Serikali kwa ujumla kazi njema ya kuisimamia Bajeti ambayo hatkuipigia kura ya upande wowote.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, orodha ya watakaochangia leo imeshawekwa kwenye ubao wa matangazo lakini wanne wa mwanzo watakuwa ni Mheshimiwa Thomas Nyimbo, nadhani wanaofuata watachangia mchana nao ni Mheshimiwa Richard

Ndassa, Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mheshimiwa Danhi Makanga na Mheshimiwa Benedict Losurutia. Sasa namwita msemaji wa kwanza Mheshimiwa Thomas Nyimbo afungue dimba la mjadala wa Bajeti ya Waziri Mkuu. (*Makofii*)

**MHE. THOMAS S. NYIMBO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kwanza kuchangia Hotuba ya Waziri Mkuu Tanzania. Kwanza kabisa nikupongeze Waziri Mkuu, hotuba yako ni ndefu na ya kina imechambua maeneo mengi na imetoa maelekezo mengi kwa mwelewa ye yote atakuwa ameielewa. Lakini hakuna zuri linaloeleweka moja kwa moja na hasa hotuba kama hii kuweza kuielewa kwa kipindi kifupi cha dakika chache hizi na ukachangia inavyopaswa kwa mwelekeo wake siyo rahisi. Lakini turuhusu muda sote tunajifunza na wote tutajifunza utafika wakati tutakuwa na uwezo. Ahsante sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Chama cha Mapinduzi, iliwekwa na wananchi kwa ridhaa yao kwa kazi mbili kubwa. Kazi ya kwanza ni ulinzi na usalama, kazi ambayo kwa ye yote mwenye akili timamu hatatia shaka, Serikali imefanya vizuri na imeendelea kufanya vizuri kwa wakati wote. Ulinzi na Usalama, ni jambo nyeti sana kwa ye yote ambaye ana mambo ya kitukutu na yasiyokubaliwa na sheria. Ulinzi na Usalama ni nguzo bora sana kwa wote wapenda taratibu, sheria, kanuni. Naipongeza sana Serikali kwa kazi hiyo kwa miaka yetu yote ya uhuru imefanywa kikamilifu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kazi ya pili ya Serikali yetu ni kusimamia na kuweka misingi mikuu ya uchumi na maendeleo ya kijamii. Mimi napenda kuanza na elimu. Hapana shaka, mimi nitashangaa sana kama ndani ya Bunge hili yuko ambaye leo haridhiki kuwa Serikali imechukua hatua endelevu zenye kulinda na zenye kuhakiki elimu ya Watanzania. Kila mmoja anaona na kila mmoja jimboni kwake anakotoka kama anawajibika pamoja na wananchi, anafahamu nini kinatendeka. Tangu tumeanza, leo tumeingia hatua nyingine Serikali kupunguza ada ya sekondari na Serikali kusaidia kujenga shule za Sekondari ili watoto wa Watanzania wengi waweze kusoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika suala la elimu napenda kuchangia jambo moja ambalo naishauri sana, Serikali kuitia wewe Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu, alisimamie. Elimu yetu haitatifikisha tunakotaka kwa *speed* endelevu kama tutaendelea kutumia lugha za kigeni. Bila kuanza kutumia Kiswahili, lugha yetu ya taifa hili katika elimu hicho ni kikwazo dhahiri na mimi katika hili naona sioni sababu kwa nini tuogope mabadiliko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika maendeleo mabadiliko ni jambo la kudumu na linaloendelea wakati wote. Najua Watanzania, wengi bahati mbaya tunayeshughulikia namna gani twende na elimu ni sisi tuliosomeshwa na wakoloni. Sasa tunapoongelea elimu iendeshwe kwa Kiswahili, tunapata tatizo ambalo halina msingi. Watoto wetu wakishaanza kuona elimu inatumia lugha ya *Kiswahili* na lugha za kigeni Kingereza, Kifaransa, Kichina na kadhalika vikawa ni masomo yanayofundishwa kama *foreign language* nchi yetu itaendelea haraka na kwa kasi zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni vizuri unapofanya mambo ukatazama aliye mbele yako. Si vizuri kutazama anayekufuata nyuma, yeze atakutazama wewe, hakuna nchi hata moja iliyoendelea ambayo imeendesha elimu yake kwa lugha ya kigeni, imeikana lugha yake ikaenzi lugha ya kigeni. Kwa pekee leo ni ombi langu Waziri Mkuu, kupitia wewe Mheshimiwa Spika, mkakae mtafakari bila uchoyo wala bila kusita tuondokane na dimbwi hili la ukoloni, elimu yetu iwe kwa *Kiswahili*. Tutafanikiwa zaidi hata Wapinzania wataona. Wengine hapa ndani hawaoni vizuri sababu hiyo hiyo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa pekee nimpongeze Mheshimiwa Edward Lowassa. *Lake Victoria* tunayo tangu milele. Ndugu zangu Wasukuma wamekaa kwenye ukame tangu milele. Lakini leo Mtanzania mmoja *daring*. Kila siku nasema unapokuwa kiongozi *you must be daring*, lazima uwe na uwezo wa kufanya, anayebisha, abishe lakini unafanya. Hongera sana Mheshimiwa Edward Lowassa. Leo Wasukumu watatumia maji ya *Lake Victoria*, siyo hadithi tena. (*Makofi*)

Mimi inasomwa hotuba ya Kambi ya Upinzani aliposema ni danganya toto nilidhani ataanza sasa kusema hili na hili halikufanyika. Ni vizuri unasema jambo halafu unalipa sifa zake bayana pale pale. Lakini kama viongozi wakuu wa maeneo yetu tukaanza kuongea mambo kama wana theolojia, wana theolojia wanaongelea Mungu ambaye na wao yeze anayeongoa hajamwona wala na yeze hamjui.

Kwa hiyo, wao tunawaruhusu wanatueleza kwa tafsiri ya kitabu tu, wewe umeshika Biblia na yeze ameshika Biblia anaanza kuongea huwezi kumwambia toa mifano hata yeze hana mifano na wewe huna mifano. Lakini haya tuliyonayo hapa ni vitu vinavyotendeka siku hadi siku, saa hadi sana, lazima tuseme. Mimi nasema Serikali ya Chama cha Mapinduzi, imewaboresha Watanzania katika elimu, katika maji, katika afya, katika kilimo na kadhalika. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana katika suala la maji nishauri Wizara ya Kilimo na Chakula, izingatie kilimo cha umwagiliaji. Mambo mengi sana tunaweza tukafanya, Mtanzania, atabaki maskini, hata tukisema dhahabu yote inayochimbwa huko kwenye machimbo, robo tatu iwe ya Serikali, maana Serikali haiwezi kupita inagawa fedha, kazi yake ni kuweka miundombinu basi tuje Watanzania, wataendelea kuwa maskini.

Lakini Wizara ya Kilimo na Chakula, ikishirikiana na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, wakizingatia umwagiliaji wenye programu inayoelewaka, mkoa fulani na fulani tunaanza wakati fulani, tunajua kila mmoja anakaa akijua suala la umwagiliaji eneo langu litaanza wakati fulani litaisha wakati fulani. Nawahakikishia Watanzania watakuwa na uchumi endelevu na umaskini katika kaya utatoweka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunayo matatizo ya barabara. Unaona jinsi gani Wizara hii inavyoshughulikia barabara ukiulizwa swali huwa unaokoa muda hautoshi maana maswali ya ziada huwa mengi na ungeruhusu ungemaliza muda wako wote kwa Wizara hii moja. (*Makofi/Kicheko*)

Lakini suala la barabara mimi naipongeza Serikali yetu imefanya jitihada kubwa sana, niombe mahususi, tunakokwenda *TAZARA* inaweza ikawa haina kazi. Ili kuokoa *TAZARA* katika Bajeti hii, Serikali itujengee barabara ya lami kutoka Tunduru kwenda ziwani Tanganyika kupitia Sumbawanga basi Reli ya *TAZARA* itakuwa ina kazi na italeta mizigo ya Zaire, italeta chakula kutoka Sumbawanga na uchumi wa watu utaboreka. (*Makofi*)

Ninalosema katika barabara tuwe na *priority* barabara ambazo zitaibua uchumi au zitawezesha mradi mwininge tulionao unataka kufa usife ndiyo maana nimeomba barabara ya lami. Tunduma mpaka *Lake Tanganyika* kwa faida na uchumi wa nchi kupitia *TAZARA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho nniombe Serikali najua mmefanya jitihada ya *Songosongo gas*, sijui *Mnazibay and all that*, kama hatutumii mkaa wa mchuchuma tunatumia *gas* mimi niwahakikishie wanaowashauri wanadanganya na ninyi kwa vile tayari ni viongozi na mnatarajia mnajua mambo na nini mnaona aibu kubisha matajiri au mnaogopa watatunyima hela au ni nini kinawapa tatizo siwezi kuelewa.

Maji tunayopoteza kwa umeme yaende kwenye kilimo, mkaa wa mchuchuma ulete umeme. Tukiingia kwenye *index* mbalimbali hakuna nchi hata moja duniani ambayo ina uchumi ulioboreka na nguvu yake (*energy*) inatokana na *gas*, maji hakuna, ni mkaa. Mungu alitupa mkaa. Waziri Mkuu, asisahau mkaa wa mchuchuma ndiyo utawezesha chuma cha Liganga kuinufaisha Tanzania. Naomba tuwe tunaelewa *priority* tunazokwenda nazo. Tatu ya Serikali kama zilivyo Serikali zote duniani ni mabadiliko. Serikali ni *conservative* sana.

Naomba Serikali ya Tanzania katika suala la umeme ijitahidi iwezavyo kukamilisha. Wengi sana wanaitisha, wale waliokula za *IPTL* ndiyo wanaitisha Serikali sasa itakuwa kama *IPTL*, kila mara wanatoa mifano Waziri Mkuu, aogope kuingia mradi huo maana utaleta tija kwa nchi lakini utaondoa tija kwa watu. (*Makofi*)

Mimi narudia tena naomba mkaa wa mchuchuma utumike kwa umeme 400 *megawatt plus* inaweza kufika mpaka 1200 ili machimbo ya Liganga chuma yawezekane, ili upanuzi wa Bandari ya Mtwara, ili reli iweze kujengwa, ili utalii uweze kufumka na barabara iweze kujengwa na mahusiano yetu katika *SADC* yakamiliike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi naomba sana Serikali yetu kwa hayo ishughulikie. Wenzetu Wapinzani, wamesema Serikali iweke utaratibu wa Chama cha Mapinduzi kupokezana Serikali na Chama kingine, si kiwepo? Chama hicho kiwepo! Hivi chama chenye Wabunge 2, 4 au 6, au tutapokezana Serikali lakini kutawala tuendelee wenyewe?

Mimi nawaomba mkubali kuwa mjifunze wananchi kwa nini hawawataki ili mkishastahilishwa na wananchi CCM iliyowaingiza hapa itawaingiza Serikalini. Lakini kwa idadi ya Wabunge, 4, 5, 6, 7 Serikali haiwezekani! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii nimpongeze Waziri Mkuu, nimpongeza Waziri wa Fedha, nimpongeze Waziri wa Mipango na Ubinafishaji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama ambavyo muda wa maswali ya nyongeza huwa unakwisha, muda wa Mheshimiwa Nyimbo kusema vile vile umekwisha na muda wa mjadala kwa asubuhi hii vile vile umekwisha kwa hiyo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni. (*Kicheko*)

(*Saa 06.57 Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi jioni hii ili niweze kuchangia katika hotuba hii nzito ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu mwelekeo wa mwaka 2004/2005. Nianze kwa kusema kwamba naiunga mkono asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kwamba asubuhi baada ya kikao kuahirishwa mchangiaji Mkuu wa Upinzani alisema maneno fulani. Lakini naomba niseme kama ifuatavyo:-

“Serikali ya Chama Cha Mapinduzi chini ya Rais Benjamin Mkapa ni Serikali sikivu, ni Serikali imara, ni Serikali makini na ni Serikali inayozingatia demokrasia kwenye utawala bora.” (*Makofi*)

Lakini pia Serikali ya Chama Cha Mapinduzi huingia madarakani kwa kupokezana viongozi wake kwa njia ya demokrasia. Haina usultani hata ye ye huyo aliyekuwa anasema asubuhi ana uwezo wa kuihoji Serikali. Kwa hiyo, Serikali yetu ni Serikali ya demokrasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nilipatwa na mshangao kwa kauli ya Kiongozi Mkuu wa Upinzani aliposema kwamba wapo watu wanawafuata fuata Dodoma na majumbani kwao. Kwa kweli kitendo hicho kimenisikitisha kwa sababu wanaowafuata ni wapiga kura wetu na ni haki yao kama ambavyo tutakavyowafuata sisi mwaka ujao. Sasa leo ukisema wasikufuate Dodoma au kwako ina maana kwamba unawafukuza mwaka ujao wasikufuate na bahati nzuri wananchi wa Kagera kwa maana ya Bukoba Mjini wamemsikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe wananchi wa Bukoba Mjini, jamani huyu ndugu yetu amesema msifuate fuate Dodoma, msifuate fuate nyumbani kwake. Kwa maana hiyo na ninyi ndugu zangu msimpe kura mwaka ujao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni sawa sawa na ile hadithi ya fundi mwashi anapomaliza kazi yake na kutupa karai akasahau kwamba karai lile litamsaidia baadaye. Lakini pia niseme tu kwamba Serikali ya Chama Cha Mapinduzi haidanganyi, lilitumika neno geresha au danganya toto. Ni vizuri kama kiongozi unaposimama ndani ya Bunge ukawaeleza wananchi ukweli kuliko kuwadanganya. Serikali ya Chama Cha Mapinduzi haidanganyi mwananchi yejote na wala haina sababu ya kutoa geresha kwa wananchi wake. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mifano ni mingi tu, labda uwe huna macho na uwe huna masikio. Lakini kwa wale wazoefu tunaokuwa humu ndani lakini hata wale walioko nje wanaisikia Tanzania kwa kazi nzuri inayofanya. Miundombinu, kila mtu anaona kwa kweli Chama Cha Mapinduzi kimesimamia ujenzi wa barabara, shule, zahanati na dawa. Sasa leo anasema hii hotuba porojo, geresha, danganya toto, labda yeje kwa hotuba yake hii kwa sababu amekosa sasa pa kushika, ameona atumie hayo. Lakini ni vizuri penye ukweli angeeleza ukweli. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie sehemu mbili ambazo ni ushauri kama Mbunge. Nazo ni sehemu za madini na bei ya minofu ya samaki.

Mimi natoka Kanda ya Ziwa kuna madini, yapo madini mengi tu. Ushauri wangu kwa Serikali, wakati Waziri wa Fedha anawasilisha hotuba yake alisema kati ya shilingi trilioni 3 asilimia 41 ni tegemezi. Mimi natoa ushauri ili kupunguza huo utegemezi. Bado tukijikita vizuri katika ule mrakahaba kwa Serikali kutoka asilimia 3 kwenda asilimia 5 nina uhakika utegemezi kutoka asilimia 41 utapungua. Huu ni ushauri wangu, naomba wataalam waufanyie kazi, tukipata asilimia 5 badala ya 3 nina uhakika utegemezi utapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niende kwenye suala la bei ya minofu ya samaki, bei hii imekuwa ni muda mrefu sana. Nakumbuka ni tangu enzi za Mheshimiwa Simon Mbilinyi, walipokwenda kuifanya utafiti pale Mwanza. Bei hiyo nafikiri sasa imeshaongezeka karibu mara mbili au mara tatu. Niombe Serikali yangu ambayo ni sikiu, ijaribu kufanya utafiti wa suala hili la bei ya minofu ya samaki angalau itoke kwenye dola moja na senti iende angalau kwenye dola 3 au 4 kwa kufanya hivyo nina uhakika lile pengo la asilimia 41 inaweza likasogea ikaenda angalau asilimia 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie vyombo vyaya habari kabla sijasahau kwa sababu na mimi ni mdau. Naomba nivipongeze sana vyombo vyaya habari vyote kwa ujumla, Redio, Televisheni na Magazeti. Ndugu zetu hawa kwa kweli wanafanyakazi nzuri sana na nzito katika mazingira magumu. Wapo baadhi ya watu huwa wanawabeza, lakini kwa kweli kama ungekuwa umeingia kwenye ile *field* ya Uandishi wa Habari nafikiri unaweza ukajua nini kinachoendelea. Kwa hiyo, mimi nasema kabisa kutoka katika sakafu ya moyo wangu, nawapongeza sana Waandishi wa Habari kwa kazi nzuri wanayofanya. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa ombi kwao kwa sababu mwaka 2004 na mwaka 2005 tunakwenda kwenye uchaguzi na wao kama jicho la Watanzania, kuandika

yale yanayotokea, inawezekana na yale yatakayotokea, niwaombe ndugu zangu kwa sababu hii ni taaluma waliosomea, waandike kwa kufuata taratibu na kanuni za nchi yetu, ili kusudi katika uchaguzi ujao unaotegemea kuanzia Novemba kwa mwaka 2004 na ule Uchaguzi Mkuu mwakani ili msifike mahali wananchi wetu mkawapotosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo magazeti, lakini wapo waandishi lakini mimi natoa rai kweli ndugu zangu Waandishi wa Habari kwa faida na manufaa ya Watanzania muandike vitu ambavyo vitaisaidia nchi yetu kuliko kuandika vitu ambavyo vitaiangusha nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo naomba sasa nzungumzie yale yaliyomo kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nzungumzie suala la kilimo. Hili ni ombi Mheshimiwa Waziri Mkuu, wengi wamekuwa wakilaumu sana Wizara ya Kilimo na Chakula, kila Mbunge aliyesimama amezungumzia kilimo. Ni kweli kabisa inawezekana Wizara ya Kilimo na Chakula lipo tatizo na tatizo Mheshimiwa Waziri Mkuu bahati nzuri wewe ulishawahidi kuwa Waziri wa Kilimo. Kwa hiyo, Wizara ile nina uhakika unajua vizuri zaidi. Sasa kulalamika Wabunge wako siku zote kunatokea Wizara ya Kilimo kwa kweli siyo vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hakuna kiongozi anayewajibika vizuri, hata akiwa wa ngazi kiasi gani ni lazima awajibishwe kwa manufaa ya Watanzania. Haiwezekani wananchi kuanzia ngazi ya chini mpaka ngazi ya Taifa wakawa wanaimba Wizara ya Kilimo na Chakula ina matatizo, hivi kweli Mheshimiwa Waziri Mkuu, hakuna tiba katika hiyo Wizara? Ni lazima tutafute tiba, kama askari yule wa mwamvuli hawezi ile kazi tutafute mbadala na bahati nzuri wapo. Maneno matupu, maneno mengi Watanzania leo hawataki, wanataka vitendo, wapo Mawaziri wazuri kabisa humu ndani, umekaa nao huko na kazi zao zinaonekana na Rais anawasifia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa pale kiongozi hafanyakazi yake vizuri inavyotakiwa, utaratibu ubadilishwe ili kilimo kilete manufaa Tanzania. Tunaambiwa ndiyo sekta mama na uti wa mgongo. Sasa uti wa mgongo usiposimamiwa vizuri basi inaweza ikawa tatizo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na kukushauri Mheshimiwa Waziri Mkuu, kweli kabisa kwa dhati, Wizara ya Kilimo na Chakula, kama yapo matatizo lakini ukienda pale Wizarani utakuta madaktari wapo pale waliosomea vizuri tu kilimo. Lakini wamerundikana pale Wizarani. Kwa nini wasiende kule tunakolima? Kwa nini wakae Dar es Salaam? Lakini kama ni muunganisho, kama lipo tatizo kwamba Wizara ya Kilimo na Chakula, Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kama lipo tatizo kwa nini wasikae pamoja ijulikane kwamba huyu aliyeo Wilayani na huyu aliyeo Makao Makuu ni vizuri wawe kitu kimoja kuliko hivi sasa utakuta huyu ni mwajiriwa wa *Council* huyu mwingine ni Wizara ya Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri yapo matatizo Mheshimiwa Waziri Mkuu, tutazame tuone uwezekano wa kuweka mnyororo mmoja unaoanzia chini mpaka ngazi ya juu. Lakini inawezekana huo mnyororo umekatika katikati hapa. Kwa hiyo, yale

mawasiliano yanakuwa ni duni. Kwa hiyo, naomba na kushauri utaratibu ufanywe ili Wizara hii iweze kufanya kazi zake vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima wenzetu walioko mbele kule sasa wathubutu kufanya kazi barabara hasa kwa kipindi hiki tunachoenda kwenye Uchaguzi Mkuu. Zile sehemu ambazo zimebaki ni lazima wazisimamie kwa dhati na niruhusu niwapongeze wale wanaosimamia, wanaothubutu bila kusita wafanye kazi zao bila kushurutishwa, wana ubunifu wao. Wapo wengi tu na niombe niwataje wachache tu ambaao ni Mheshimiwa Edward Lowassa, ametuletea sifa kubwa sana kwa kweli, Mheshimiwa John Magufuli, Mheshimiwa Mama Anna Abdallah, Mheshimiwa Mama Zakia Meghji na wengine wanathubutu, hawaogopi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo la viongozi wetu kutokuthubutu, wanaogopa kufanya au kutenda. Lakini hata katika hotuba ya Mheshimiwa Rais iliyopita wakati akituhutubia hapa alisema: "Ni lazima mthubutu, msisubiri mpaka muelekezwe," na ndiyo maana mkakaa kule mbele, vinginevyo itabidi mrudi huku sisi tuje huko. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niwapongeze sana Ndugu zangu wale wanaotekeleza majukumu yao vizuri. Baada ya maneno hayo, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia moja. (*Makofi*)

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi mchana wa leo na mimi niweze kuchangia machache kuhusu Makadirio ya Matumizi ya fedha ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa mwaka wa 2004/2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri sana. Tena yenyewe mwelekeo mzuri, inayoonyesha sura nzuri ya utendaji wa kazi ndani ya Serikali yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo yote yamejidhihirisha hivyo kwa sababu nchi yetu ina amani, ina utulivu na kila mtu anafanya kazi yake bila bughudha na hali hiyo inajitokeza, hivyo kwa sababu vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama vile vile vinafanya kazi yake nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iendelee kudhibiti hali ya Ulinzi na Usalama kwa uzi ule ule. Serikali inayofuata utawala wa sheria kama Tanzania ni lazima iwe macho kudhibiti vitendo vyote vya uhalifu na uvunjaji wa Sheria bila kuogopa hata kidogo. Haiwezi kuvumilia mtu au watu ambaao wanajidai wao eti wako juu ya Sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nipongeze kwa Serikali kutenga fedha ya kutosha kwa ajili ya vyombo vyetu vya ulinzi na usalama katika kipindi hiki cha mwaka 2004/2005. Kazi ya vyombo vyetu ni kubwa. Labda nirudi tu kwenye hotuba ya Kiongozi wa Upinzani leo asubuhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka ametoa mfano wa hali ilivyokuwa katika Chaguzi za hivi karibuni za Serikali za Mitaa, Mkoa wa Kilimanjaro ukiwa mmojawapo. Nataka nitoe mfano, kwa sababu ya ushahidi nilionao. Si sahihi hata kidogo kutoa lawama kwa Serikali kwamba Serikali imekuwa ikichochea, inachochea uhalifu na hata kuwezesha Mheshimiwa Mbunge akapigwa. Hii siyo sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nithibitishe kwamba hata ndani ya vyama vyenyewe vya upinzani, kuna magomvi wao kwa wao. Sasa wao kwa wao vile vile wanakosana, hawana urafiki, kwa nini leo uthibitishe kwamba ni Serikali ya CCM ndio iliyopiga na siyo wao kwa wao. Hawapendani hata kidogo. Kwa hiyo, si kweli kwamba Serikali ndio inachochea. Sasa kama wanapigana wakatoana meno, pua, mimi sikubaliani kabisa kwamba Serikali inachochea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina wajibu wa kulinda kila Mtanzania inapotokea hali ya namna hiyo, kwa hiyo, basi kama Serikali inatoa fedha ya kutosha kwa vyombo vya dola ni sahihi kwa sababu vurugu ya namna hii ikitokea ni lazima iingilie kati bila kujali kwamba huyu ni wa chama gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tusifu, mambo yaliyo wazi ni lazima tufurahi, tusifu kwamba ni sahihi Serikali inafanya. Ni lazima tuilinde nchi yetu wote, awe wa chama cha upinzani, chama tawala, wote tuna wajibu wa kulinda Serikali yetu na nchi yetu ili watu tufanye kazi. Ndiyo maana mafanikio yanayojionyesha katika hotuba hii ndefu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, mafanikio haya yote yanatokana na hali hii ya kwamba wote tuna amani na tuna utulivu, tunafanyakazi, Mawaziri wanafanya kazi vizuri, wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa amani na utulivu bila bughudha wakisaidiana na watendaji wao, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nichangie mambo mengine mawili matatu, la kwanza ni kuhusu chakula. Katika kipindi cha 2003/2004 hali ya chakula wote hapa tunafahamu hali haikuwa nzuri sana kwa nchi nzima na Mheshimiwa Waziri Mkuu amelizungumzia katika hotuba yake. Hali ilikuwa si nzuri katika Mikoa mingi na ni Wilaya chache sana zilikuwa na neema.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kuipongeza sana Ofisi ya Waziri Mkuu kuititia Kitengo chake cha Maafa, kwa kazi kubwa waliyoifanya kwa nchi nzima kuratibu suala la njaa katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naafikiri Mheshimiwa Waziri Mkuu, alikuwa halali akimtuma kijana wake Mheshimiwa William Lukuvi azunguke kila mahali na kuhakikisha kwamba kuna chakula cha kutosha na kutoa maelekezo nini kifanyike ili wananchi wasife kwa njaa na watendaji wamefanya kazi kubwa na mpaka msimu mpya wa mavuno umeanza hivi sasa hali ilikuwa si mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme katika hali hii wananchi wamepongeza vile vile na wamekiri kabisa kwamba kumbe Serikali yao ya Chama Cha Mapinduzi inawajali sana wananchi wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki cha mwaka 2004/2005 tunamshukuru Mwenyezi Mungu hali si mbaya, hali ya mavuno si mbaya katika Mikoa mingi hasa katika Mikoa ile ya Nyanda za Juu Kusini na Mikoa mingine naambiwa Kigoma, Tabora na Kagera hali siyo mbaya sana kwa sababu mvua zilinyesha za kutosha na wananchi walilima vizuri, tunawapongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna baadhi ya maeneo katika Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha na baadhi ya maeneo katika Mkoa wa Manyara, hali si nzuri hata kidogo. Wananchi walilima sana tena kilimo cha kufa na kupona, wakapanda mazao, lakini yalipofikia katikati yamekauka kama Serikali ilivyoainisha katika hotuba yake.

Nilitaka nichukue nafasi hii kutoa tu kama ombi la tahadhari kwa Mikoa ile ambayo wamepata chakula cha kutosha kwa sababu wenzetu walifanya kazi na Mungu aliwarehemu lakini ni kwa faida ya sisi wote kama nchi basi tuishauri ile Mikoa ya kwamba pamoja na kwamba tungependa wananchi wauze chakula chao hata nje lakini utumike utaratibu wa kudhibiti hali hiyo kwamba chakula hicho hakiuze chote mpaka tuhakikishe Watanzania wote hapa nchini watapata chakula cha kutosha na katika kufanya hivyo vile vile ningependa kutumia nafasi hii niwashauri wafanyabiashara mbalimbali wenyewe uwezo watumie nafasi hii ya sasa hivi ambapo bei ya chakula ni chini, wanunue chakula na kukipeleka katika maeneo ambayo tayari hali inaonyesha ni mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tathmini inafanyika ya kuonyesha namna gani athari itajitokeza na kama mvua za vuli hazitanyesha kwa wingi kwa kweli kipindi cha mwaka 2005 kitakuwa kibaya sana hasa mwanzo wa mwaka. Kwa hiyo, hilo tulifanyie kazi vizuri na naamini kabisa kama maelekezo yakinika sawasawa kila mtu atatimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili ningependa vile vile kusisitiza kwamba katika hali ya namna hii limejitokeza zao la muhogo ambalo watu wengi wanalidharau ni zao ambalo linavumilia sana ukame, ni zao ambalo ukiwahimiza wakulima na wakalima vizuri, kwa kweli muhogo unawenza kutuokoa na tusiweze kuathirika hata kidogo kwa njaa.

Kwa hiyo, naamini kabisa kama Wabunge tulioko hapa kwa vite tuna nafasi zetu nzuri ni vizuri tukasaidiana na Serikali yetu katika kuwahamasisha wananchi wetu waweze kulima zao la muhogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kidogo suala la janga la Ukimwi. Sera ya Ukimwi imeanza kufanya kazi vizuri sana na ni Sera moja kati ya Sera nyingi tulizonazo ambayo inafahamika vizuri sana kwa wananchi vijiji mpaka katika ngazi ya vijiji na kuna Kamati ambazo zinafanya kazi, Kamati zile ambazo ni Kamati za Ushauri kila mahali zinafanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kushauri kwamba isiwe ni vikao tu, Kamati zижиширикише zaidi kwa kwenda kwa wananchi na kufanya kazi ambazo wanawenza kuwasaidia wananchi katika elimu, kazi za Kamati kama ikiishia vikao kama hali inavyokuwa hivi sasa kwa kweli sioni kwamba matunda yake yatakuwa mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba vile vile uwakilishi katika Kamati hizi uongezwe hasa kwa upande wa wanawake. Wanawake waongezwe kwa maana ya kuwa na Wabunge wote wa Viti Maalum Wanawake waingizwe pamoja na Waheshimiwa Madiwani wa Viti Maalum ni vizuri wakawa Wajumbe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kwa kumalizia naomba nzungumzie suala la kukuza uchumi kwa mwananchi wa kawaida. Mimi nafikiri uanzishaji wa vyama vyaa kuweka na kukopa katika suala la kukuza uchumi wa Kaya ni sahihi kabisa.

Kwa niaba ya wanawake wote wa Mkoa wa Mbeya ambao wamedhamiria kuanzisha Vyama vyaa Kuweka na Kukopa katika Kata zote, naomba wadau mbalimbali wasaidie katika kukuza mitaji yao lakini vile vile katika kutoa semina za ujasiriamali ili waweze kujiendesha vizuri. Katika Mkoa wa Mbeya wanawake katika ngazi za vijiji, Kata, wote wameanzisha Vyama vyaa Kuweka na Kukopa wakijua kwamba hili ndio jawabu la kuondokana na umaskini. Wanakopeshana kwa viwango vidogo vidogo lakini matunda yake ni mazuri. Kama Waheshimiwa Wabunge ni kazi yetu kuwapa moyo, kuwaonyesha njia nzuri za kurekebisha makosa yoyote yanayojitokeza ili Vyama hivi vikue na viweze kumkomboa mwanamke.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, naomba kusema kwamba bila wasiwasi wowote naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia, ahsante sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**MHE. DANHI B. MAKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuongea hapa baada ya likizo ndefu ya mwaka mzima, nitatoa pongezi, pole na shukrani kwa walionisaidia kwa namna moja au nyingine. Kwa hiyo, nikianza kuchangia hoja ndio unaanza kunihesabia dakika kumi na tano. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuwapa pole Waheshimiwa Wabunge na ndugu zangu ambao wamepata matatizo mbalimbali nao ni Mheshimiwa Anne Malecela, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere na Mheshimiwa Estherina Kilasi, poleni sana ndugu zangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kutoa pongezi kwa Waheshimiwa Wabunge wote katika Bunge hili. Kwa kweli mmejitahidi sana kutimiza kazi zenu za Kibunge kwa muda wote ambao sikuwepo hapa. Vile vile nawapongeza sana kwa kunisaidia nikashinda uchaguzi huu ambapo kwa kweli yalikuwa ni mapambano makali sana hata ambao hawakufika, kwa sala zenu nawashukuru sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nawapongeza Mawaziri wote wa Mipango na Ubinafsishaji na Fedha ambao wametoa hotuba zao hapa Bungeni na Baraza zima la Mawaziri kwa ujumla kwa kutekeleza majukumu yenu vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kusimamia shughuli za Serikali kwa karibu sana hata sisi tuliokuwa vijijini tumepata matunda yako vizuri. (*Makofi*)

Vile vile niwapongeze waliochaguliwa katika nafasi mbalimbali za Kimataifa, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mheshimiwa Arcado Ntagazwa na Waheshimiwa Wabunge wengine. Najua tumeunda Bunge la Afrika sasa labda linakuja Bunge la Dunia, tutakaowatuma vile vile Rais atatoka Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niipongeze Serikali, kwanza wamejitahidi sana kutekeleza mambo mengi ambayo yalikuwa kero kubwa hasa kwa wapigakura wetu waishio vijijini. Najua hata Wapinzani wameogopa kuja hapa wanafikiri labda nitawalima sana, lakini nina ushauri kwamba kwa kweli tunahitaji Vyama vya Upinzani makini ambavyo wanachama ndio watakuwa wenyewe Chama sio mtu mmoja nyumbani kwake ana Chama. Tukiendeleza mtindo wa mtu kuwa na Chama chake nyumbani, tunamwomba huyo kiongozi atafute *godown*, akifungie Chama chake asubuhi awe anakikagua na mke wake, fulani Chama chetu kimo humo, anafunga anarudi nyumbani. Kwa kweli huku ni kupotosha nia na malengo ya Mfumo wa Vyama Vingi katika nchi hii, ni kuidhalilisha demokrasia, ni matusi kwa wanachama ambao wanajiunga na Vyama hivi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najua wana kazi kubwa ya kupeleka hoja kwa wapiga kura mwaka ujao katika Uchaguzi Mkuu. Kama walivyosema wenzangu mambo mengi yamejibiwa na Serikali. Nilipokuwa Upinzani na mimi nilikuwa napiga kelele sana kwa sababu kero ziliikuwa nyingi, shule hakuna, madawati hakuna, Walimu hakuna, Zahanati hakuna, dawa hakuna, barabara hakuna, maji hakuna sasa yote kwa kiasi kikubwa yametekelizwa na yanaendelea kutekelezwa kwa hali na mali. (*Makofi/Kicheko*)

### **MBUNGE FULANI: Ndio!**

**MHE. DANHI B. MAKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa Upinzani nilikuwa nawauliza ndugu zangu hivi tutaendaje mwaka 2005, tuwapelekee hoja gani wananchi? Sasa kila mtu anaruka na lwake bwana, hakuna umoja katika Upinzani, huyu amekuja na Sera ya Kujaza Watu Mapesa wakati ye ye hana hata shilingi moja. Huyu mwingine anaruka na Utajirisho wakati ye ye hajamtajirisha hata mjomba wake. Nasema katika Vyama vyetu tuna matatizo. Ndugu zangu tafuteni *think tank*, tafuteni wataalam wa kupika hoja za kwenda kwa wananchi msipofanya hilo, mtaendelea kuwa wasindikizaji. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani nyingi kwa Chama chetu cha Mapinduzi kwa ngazi zote kwanza kwa kutupokea sisi kwa mikono miwili na mingine mingi sana mimi na Madiwani ambao tulikuwa Chama cha *UDP*, tuliporudi CCM tulipokelewa kwa

shangwe kubwa lakini vile vile na kututeua kugombea katika Majimbo yetu ya Uchaguzi. Hiyo ni heshima kubwa, ni ukomavu wa kisiasa. Mimi nasema CCM ni timu ya washindi. CCM ni Chama kama timu ya *Real Madrid*. *Real Madrid* haichoki kutafuta wachezaji wazuri hata kama namba hiyo ina wachezaji sita itamsikia mwininge yuko wapi inamleta na mimi nimerudi CCM. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kiasi kikubwa heshima waliotupa wana CCM na sisi tumeweza kuirudisha kwa kufanikisha uchaguzi Bariadi. Katika Madiwani nane waliogombea tumeshinda viti saba na katika Ubunge tukapata vyote. Kwa matokeo hayo, Halmashauri iliyokuwa inaongozwa na Chama cha *UDP* sasa inaongozwa na CCM. Napenda kusema kwamba sasa hivi hata Jimbo la ndugu yangu Isaac Cheyo, liko wazi, tutalirudisha. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru sana Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga; Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Dr. Chegeni Masunga, Mheshimiwa Robert Buzuka, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, Mheshimiwa Paul Makolo, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu kaka yangu na Waheshimiwa Wabunge wote waliotusaidia, nasema ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani za mwisho kabisa na za pekee, napenda kumshukuru Mzee wetu, Mheshimiwa Dr. John Samwel Malecela, kwa kuja kukaa na sisi Bariadi na kufanya shughuli kubwa ya kurudisha heshima ya Chama cha Mapinduzi katika Wilaya hiyo, namshukuru sana. Pia Mwenyekiti wa CCM, Mkoa wa Tabora, Mzee Juma Nkumba, naye tulikaa naye muda wote, nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka niwashukuru sana wananchi wa Bariadi Mashariki na Magharibi kwa kuwachagua Madiwani wetu wote saba katika Kata nane na kunirudisha mimi Bungeni, leo nimesimama nazungumza. Hii ni kuonyesha nguvu ya umma ilivyo kubwa, wewe peke yako huwezi kuizua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipofukuzwa uanachama na hatimaye kupoteza Ubunge wangu kwa kweli yako mambo mengi nimejifunza na yako mambo mengi inawezekana katika taratibu zetu yanatakiwa yaangaliwe na kwa sababu viko vitengo mbalimbali ambavyo vinahusika na Ofisi ya Waziri Mkuu, napenda nivizungumzie. Nilitegemea viongozi wote wa Upinzani wangelaani kitendo cha Mheshimiwa John Cheyo, kufukuza Wabunge. Kati ya Wabunge watatu ulionao, unafukuza wawili wasio ndugu zako unambakiza mmoja ambaye ni ndugu yako? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hicho ni kitendo ambacho nilitegemea viongozi wote wa Vyama vya Upinzani wangelaani kitendo cha kuua Upinzani ndani ya Bunge na Vyama vya Upinzani kwa ujumla lakini kinyume chake vikamchagua kuwa Mwenyekiti wa Vyama vya Upinzani, sijui amepewa nishani ya kufukuza wanachama!

Kama kiongozi hawezi kukaa na Wabunge watatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa ana Wabunge 258 na mimi wa 259 huyu mtu hajapata hata madaraka ya

dola anafukuza Wabunge waliotumwa na wawakilishi bila hata vikao halali anatumia vikao haramu vya nyumbani kwake, huu ni ubakaji wa demokrasia, huu ni uharamia, hii ni *political bandit*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Umoja wa Mataifa ungeunda Mahakama Maalum ya kushughulikia waharibifu hawa wa demokrasia. Kama vile wahalifu wa vita wanavyoshtakiwa na wahalifu wa demokrasia ipatikane Mahakama Maalum ya Umoja wa Mataifa ya kuwashughulikia watu wa namna hiyo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipeleka kesi Mahakamani na kwenyewe ikawa inapigwa tarehe nikaona Mahakama sahihi na yenye uwezo mzuri wa kidemokrasia ni wananchi wenyewe na ndio maana nikarudi Chama cha Mapinduzi. Kwa *step* hiyo tena nawashukuru Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kwa kuruhusu sheria ya kurudia uchaguzi mapema ilivyowezekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo makubwa manne niliyoainisha ni haki ya mpiga kura. Kwa kweli wote tujiulize hivi mpiga kura aliyemtuma Mbunge kuja Bungeni anapata wapi haki yake ya kuhoji kwamba mimi nilimchagua huyu, hakuchaguliwa na Mwenyekiti wa Chama, anapata wapi haki yake ya kuuliza na kufuatilia ili hatimaye kweli apate uwakilishi katika chombo kama hiki? Nafikiri katika Katiba zetu basi tufanye utaratibu wa kubadilisha Mbunge asiye na kosa, kwa sababu hii ni kuwaaadhibu wapiga kura ambao hawana kosa, ni matatizo ya vichaa fulani vinachanganya mambo hapo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa mwagine ni Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, hivi ofisi hii Mbunge fulani anafukuzwa yenye ina nguvu gani? Kama haina basi ilet sheria hapa tubadilishe. Ofisi ya Msajili ipitie Katiba za Vyama hivi, hivi kweli zinaendana na Katiba ya nchi na je, Katiba hizo zinatekelezwa? Msajili anakaa tu Wabunge wanafukuzwa kienyeji kazi yake ni nini na tunapitisha Bajeti hapa, ruzuku inatoka unafuatiliaje kama kweli inafika kwa walengwa? Hawa viongozi wa Vyama hawa wanatekelezaje demokrasia katika Vyama vyao? Wewe una kazi gani ya kuangalia tu Vyama vinasajiliwa au namna gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema Msajili una kazi ya kufanya, fuatilia Vyama hivi, vingine havipo, kama vilisajiliwa vina wanachama Zanzibar leo havipo, kama vina wanachama Bariadi leo havipo. Fuatilia utupe taarifa nzuri na ambavyo havitafaa vifutwe mara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni Ofisi ya Spika na yenye inapokea maamuzi mengine ya chooni. Kwa kweli Ofisi ya Spika ina wataalam wa sheria ingweza kupitia Katiba ya *UDP* na kuona kama kweli Mwenyekiti anaweza kumfukuza kwenye *television* Mbunge aliyechanguliwa na watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Spika inapewa inakubali tu haya ondoka kwenye Ubunge, hapani! Gharama ya kupata Mbunge ni kubwa, leo Bariadi Mashariki

tumetumia si chini ya milioni 600 kumpata Danhi Makanga tena, sasa hizo hela tungepewa tukachimba visima tungepata vingi tu.

Naomba Ofisi ya Spika ifanye kazi hiyo kwa sababu Wabunge hawa wote wakifukuzwa, maana anaweza kuwa kichaa ana Wabunge wengi hapa akaamka tu kwenye *television* Wabunge 200 hakuna, wewe Spika utakaa hapo, maana lazima na wewe uangalie, kulinda kiti chako ni Wabunge tuwepo hapa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni Tume ya Uchaguzi, yako mambo ya ajabu ambapo Tume ya Uchaguzi inatakiwa kufuatilia. Wagombea wanapokuwa kwenye majukwaa wakijinadi wanatangaza mambo ya uongo hadharani, saa sita mchana. Mgombea anasema mimi nimefuta kodi, kodi tumeifuta Wabunge yeze hakuwepo hapa. Mgombea anasema nimejenga shule, nimechonga madawati, sijui amekuwa seremala wa nchi nzima hii? Mgombea anasema naanza kujenga barabara ya lami kutoka Dodoma mpaka Mwanza, wewee! Yako mambo ya uongo nafikiri hata Tume ya Uchaguzi inatakiwa kuyaratibu. Wagombea wanapojinadi kwa kweli watangaze sera zao sio kujigamba. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja hii kwa mikono miwili, ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa kweli naweza kusema kwamba hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imeandaliwa vizuri na kwa kweli ina tija kwa Watanzania. Nampongeza sana yeze pamoja na wataalam wake na Mawaziri wake kwa kazi nzuri sana ambayo wameifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kutoa pole kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda pamoja na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao mzazi na Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi, *Amin*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya hasa nikimpongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, ambaye ni rafiki yangu kwa ushindi mkubwa ambao ameupata na ametoa dozi hapa kidogo. Nadhani wenzetu wamesikia lakini kama sikio la kufa halisikii dawa, basi bwana, lakini wameambiwa. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ndugu zangu katika hili Chama cha Mapinduzi ni imara sana wala hatupigi porojo hapa. Ukienda vijijini kielelezo kikubwa cha juhudi ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi na Ilani yake unakiona. Miaka ya nyuma tulikuwa tunapiga kelele sana hapa, tulikuwa tunaruka, tunaumana lakini sasa tumetulia kwa sababu ya Chama cha Mapinduzi kutekeleza Ilani yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2002, Wilaya ya Kiteto tulikuwa na wanafunzi 6,000 tu kwa miaka miwili sasa hivi tuko 30,000. Tulikuwa na shule 30, sasa hivi tuna shule 70. Sasa wewe utasema vipi Serikali haijafanya kazi? Maji, ndugu yangu

Mheshimiwa Edward Lowassa, juzi wameleta *World Bank* kila mwaka vijiji kumi vinachimbiwa visima, mabwawa, hivi tunataka nini? Siwezi kuzungumzia afya, mawasiliano na hii timu iliyo mbele yetu kwa kweli miaka yote sijawahi kuisifu lakini sasa imefika kikomo nawasifu. Huwa mzito sana kusifu, lakini sasa mmenifikasi mahali pazuri kabisa, nawasifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, sasa tunasema tunarekebisha sio kama wanavyofikiria wao, hapana tunajaribu kutoa maelekezo kama yanafaa yanafanyiwa kazi, kama hayafai yanawekwa pembedi. Hayo ndio majukumu yetu na tunaunga mkono kabisa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kuna Daftari hili la Wapiga Kura, sheria imeshapita, naomba Waheshimiwa Wabunge mnisikilize, mazingira ya watu wetu hasa wafugaji kuwapata ni shida sana na wanatakiwa waandikishwe, wapigwe picha wakati wanahangaika na mifugo inatakiwa wakati wa kiangazi kabisa mwezi wa kumi.

Naomba kabisa Serikali pamoja na wengine mnapoona wanahama pale na pale mtengeneze kanuni, taratibu za namna ya kuweza kuwaandikisha kwenye daftari hili, vinginevyo hawatapata nafasi ya kupiga kura kwa sababu ya mifugo, mwezi wa kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *I am very serious for that* watengeneze taratibu, kwanza kamera kule hakuna halafu unazungumza akinamama, akina nani, kwa hiyo, muda na taratibu zipangwe vizuri ili nao waweze kushiriki katika demokrasia hii otherwise watashindwa kupata wawakilishi wao wa uhakika. Hilo naomba kabisa lishughulikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka nilizungumzie ni utawala bora. Bado tuna matatizo katika utawala bora. Tuna tatizo kubwa la kulindana na hatuwezi kupata maendeleo hata kidogo. Nasema hivi kwa sababu huwezi kuwa na kiongozi ambaye unamhamisha kutoka Wilaya moja kwenda Wilaya nyingine kila mara. Unamtoa Kongwa umpeleka Rombo kila mahali anafukuzwa. Halafu linaloniuzi anaharibu, Kamati zinakaa kule halafu bado kuna watu wanamkumbatia kwa kweli hapo siko na ninyi kabisa, sipo kabisa, waharibifu kabisa. Kwa nini mnawakumbatia watu ambao wanaharibu, wanaleta migogoro? Unamchukua *DED* kutoka hapa unamzungusha nchi nzima, mbovu tu, unamchukua *DC* unamzungusha nchi nzima.

Sisi Wabunge, wananchi wakituchoka hawatupi kura unabaki kule sasa mtu ambaye sisi tumemchoka, tukamnyima kura unaturudishia wa nini tena sisi na kule ndio ameshindwa wamemwagusha unatuletea wa nini sisi? Sisi tulishamkataa kutokana na makosa yake makubwa, hataki maendeleo, hataki sekondari mpaka Mheshimiwa Joseph Mungai amemwandikia barua, bado mnakumbatia, halafu ni muongo, anadanganya ngazi za juu anasema Mheshimiwa Benedict Losurutia, sijui nini, mimi ni *clean bwana* na nina hakika kabisa na watu wangu wanajua. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema hivi kwa sababu lazima liwekwe kwenye *Hansard*, inafika mahali lazima u-register mambo yako ya kihistoria kwa sababu kwa

jinsi alivyoirudisha nyuma Wilaya ya Kiteto hata siku moja wana Kiteto hatutawezza kusahau, kufukuza Wenyeviti 15 katika mikutano ya hadhara, hana utaratibu. Kamati ya LAAC imekwenda wameona, viongozi wamekwenda wanamwona hata kama ni Mmasai, Mmasai mharibifu, eti wapelekeeni Mmasai mwenzao, hamwezi kuongea Kimasai tunaongeaje na mharibifu? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana hilo na TAMISEMI mmesikia, tayari katika historia yangu nimeshasema Ole-Molloemet kwangu hafai, tayari nime-*register* na kazi yangu imekwisha. Kila mahali ugomvi, alipambana na kina Mheshimiwa Edward Lowassa, Mheshimiwa Parseko Kone, kila mahali alipokwenda alipambana, sasa mimi unanilettea wa kazi gani? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Serikali imesikia kama inataka kumkumbatia, imkumbatie, lakini mimi katika uchaguzi nitashinda na kurudi hapa. Nina historia nzuri tu ya mapambano, hakuna shida na watu wangu wananielewa. Mara ya kwanza nilishinda kwa kura 32, mara ya pili nimeshinda kwa kura 5,000, mwaka 2000 nimekuja kwa kura 8,000 fikiria basi mwaka 2005 kwa kura 10 au 20? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nizungumzie suala la chakula kwa sababu tuna tatizo kidogo. Sisi Kiteto tunalisha Dar es Salaam, soko la Tandale, chakula hatuna kingi kuna maeneo ambayo hayajapata chakula. Mwaka 2003, msimu uliopita tulipata taabu sana, watu wa Kiteto wameumia sana tunaomba Serikali iwe makini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukishaona keki ambayo inalisha Dar es Salaam hivi Waziri wa Kilimo na Chakula, kwa nini asitusaidie sisi ili tulime vizuri kwa kutupa mikopo na kadhalika. Ni mahali ambapo ni *potential*, mahindi yaliyoko Kibaigwa yametoka Kiteto lakini hata siku moja hatujapewa mkopo ni wananchi wangu wa Kiteto wanalima, wanahangaika, wanaskia pesa zipo basi tunalisha tu. Kwa kweli tunaomba mtusaidie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la barabara. Waziri Mkuu amezungumzia suala la X na ameliweka vizuri sana, lakini ninachotaka kusema hapa ni kwamba Sheria hii ilipitishwa mwaka 1932 kuna kijiji changu kinachoitwa Dosidosi kimeanzishwa kabla ya Nairobi, wanasema eti ikishafika miaka ya 1932 nyumba ambayo imejengwa nyuma inatakiwa kupewa fidia, hizo ni zamani kabisa. Sasa sisi tunahitaji fidia maana sisi tuko nyuma sio alama X ile Dosidosi chukueni historia yake na mtoe fidia. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu mtoe *clarification* kuna Misikiti, Makanisa, shule yamewekwa alama ya X, hizi ni huduma za kijamii na watu ndio wamepoteza nguvu zao, huko nyumba zao zimewekwa X hizi za kijamii mtafanya nini ili kama mnafidia tujenge tena Misikiti, Makanisa na Shule pale. Hata mimi Mbunge nyumba yangu imewekwa X, lakini hii ni harusi kwa sababu wote tumewekewa lakini naomba tupate *clarification* juu ya suala hilo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo nataka kuzungumzia ni suala la upimaji wa ardhi, wanasema kwamba kila mkulima apime shamba lake ili apate Hati, bado hatujapata ufanuzi wa namna rahisi ya kupata Hati, wataalam na kadhalika. Benki ziko wazi lakini taratibu na gharama bado hazijakamilika kwa sababu ukiwagusa wale wapimaje weee, wanakumaliza, hebu mtuandalie utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda kusema kwamba lililonikera ni hilo moja tu mengine yote ni mazuri, hongereni sana kwa kazi hii na naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hoja iliyo mbele yetu. Hotuba ya Waziri Mkuu imeandalika vizuri, kimakini na inaeleweka na inaonyesha kwamba tangu awe Waziri Mkuu anazidi kukua na kukomaa zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia mahali popote pa kuweza kumkarifu au kufanya nini palikuwa ni pagumu. Kwa hiyo, ni hotuba nzuri sana na inaeleweka na nadhani wenzetu Wapinzani labda kwa sababu waliipata kwa muda mfupi, nawashauri wakaisome tena na ikiwezekana wapewe nafasi ya kueleza watazungumza mengine tofauti na waliyosema leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumpongeza ndugu yangu Mheshimiwa Danhi Makanga kwanza kwa uamuzi wa busara alioufanya. Nadhani wenzetu inabidi wajifunze kwamba kuna mambo ambayo pengine bado yanapungua na inabidi waangalie sana kufuata taratibu. Nimesikitishwa na kusema kwamba walipigwa lakini nikawa najiuliza sehemu zote walizopita mbona hawakupigwa au kuna mahali wanakwenda bila ulinzi kwa sababu kuna utaratibu unapokuwa Rais wa nchi au unatarajia kutawala kuna utaratibu wa kulindwa na nini. Sasa kama kuna mahali pengine umekwenda kienyeji pengine wanakuwa na wasiwasi na wewe.

Kwa hiyo, naomba ndugu zangu wa Upinzani aliyozungumza Mheshimiwa Danhi Makanga ni mazito na nafikiri ni vizuri mkachukue *Hansard* tena mkairudie, mkaangalie, mwone mrekebishe wapi. Sisi tunawahitaji humu ndani ili muweze kutupa joto joto na ni vizuri mkubali (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, kwa heshima aliyoletetea kuwa Rais wa Bunge la Afrika. Ni heshima kubwa hata wale Waafrika ambao hawajui ramani ya Tanzania wameanza kutafuta na hata Kisiwa cha Ukerewe wameanza kukitafuta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nitoe rambirambi kwa ndugu zangu waliopata maafa, Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan kwa kufiwa na binti yake kwa ajali, familia ya Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, kufiwa na mzazi wao, poleni sana. Vile vile niwape pole waliopata ajali Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere na Mheshimiwa Estherina Kilasi na Mheshimiwa Anne Malecela, kwa uvamizi wa njiani. Hizo ni ishara kwamba tunahitaji Serikali kuimarisha ulinzi zaidi na taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Jimbo langu kwa katika Bunge hili ni mara yangu ya kwanza kuzungumza, napenda nipeleke salam za pole kwa wananchi wa Geita ambao walipata ajali tarehe 31 Mei, 2004 baada ya kuvamiwa na majambazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, majambazi waliwavamia wananchi, ilikuwa ni asubuhi, wananchi walikusanyika kujaribu kupambana na majambazi ambao walikuwa na bunduki na wao hawakuwa na bunduki bali walikuwa na mawe, wakajaribu kuwafukuza lakini walikuwa wanawaua kama utitiri lakini Wasukuma walisema *tujage duhu mpaka masasi gakushila. (Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, walipiga yowe wanasema twende tu mpaka risasi zitakwisha tu. Kwa hiyo, wakaenda na *u shape*, wanayafukuza hatimaye kweli mpaka wakafika Wilaya ya Biharamulo, Kijiji cha Mwendakulima risasi zikawaishia wale majambazi, wakawavamia na watu kumi walikuwa na watatu wakawa wamejeruhiwa. Ni ujasiri mkubwa sana kwa kweli. Nafikiri Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ni vema afike kule na kuwapa pole wale wananchi.

Napenda nimpongeze Mkuu wangu wa Mkoa amewahi kufika kule, wananchi wale walijitolea sana kila walipokuwa wanauawa wanachagua watu wanawapeleka wengine hospitali au wengine chumba cha kuhidhia maiti, wengine wanaendelea mbele. Nafikiri yalikuwa mapigano kama ya saa nne kwa sababu ulikuwa ni mwendo wa kutoka Kata ya Katoro, Kaseme mpaka Mwendakulima kwa Mheshimiwa John Magufuli kule ndiyo wakaenda kuwamaliza wale majambazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nisilaumu Polisi kwa sababu taarifa zilipelekwa lakini uwezo wa Polisi kufika kule kulikuwa ni mbali na hawana vyombo vyaa usafiri. Wilaya ya Geita ni kubwa, barabara ni mbaya, wana gari nafikiri moja ambalo na lenyewe mara nyingi ukiwapigia wanasema tuletee gari.

Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika hili amwulize Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, mwaka 2004/2005 amepanga nini kwa Wilaya ya Geita? Mwaka 2003 tulimwuliza, akasema, lakini nafikiri mwaka 2004 kama Bajeti imeongezeka amwulize amepanga nini kwa sababu Wilaya ya Geita inaelekea kukaribia Mkoa wa Singida au Lindi. Ina watu laki saba na zaidi karibu laki nane na inakaribia Zanzibar. Sasa angalia kama ni kusaidia watu hiyo *sharing* ya huduma ikoje? Tunaomba sana kwa kweli. Kule kumekuwa kama eneo la wakimbizi. Kuna madini, pamba, mifugo na watu wengi sana, sasa kimekuwa sana kificho, tunaomba Serikali itusaidie kwa kufanya jitihada za makusudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri kwa kazi wanazofanya ni nzuri na Serikali yetu inafanya vizuri kwa kweli, wanajitahidi. Wenzangu waliotangulia wamesifu, hakuna haja ya kurudia ni kazi nzuri sana inayofanyika, barabara zinaonekana lakini kama alivyosema aliyetangulia kuna mambo

ya kurekebisha rekebisha. Tunaomba, tunapoomba kurekebishana wenzetu Mawaziri wakubali kwamba hapa kunahitaji kurekebishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2003 katika Bunge hili Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, alitoa tamko zuri la kuajiri Watendaji wa Vijiji ili waweze kufanya kazi nzuri. Alikuja tena akarudia katika Bunge la mwezi Februari, akatoa hotuba nzuri sana waajiriwe wale watendaji wa zamani. Napenda kunukuu alisema: "Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ya mwaka 2003/2004, nililiarifu Bunge lako Tukufu uamuzi huu wa Serikali wa kuwaajiri watendaji hao wa Vijiji na jumla ya shilingi bilioni tano, laki saba na arobaini na tano milioni na sitini elfu zilitengwa kwa ajili ya kulipa mishahara yao kuanzia tarehe 1 Januari, 2004."

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu amwulize hizi hela zimeshalipwa au zilikwenda wapi? Mimi kwangu hazijalipwa. Sasa haya ni mambo ambayo tunahitaji kuyarekebisha, yafanyiwe kazi na sasa hivi hawa watu hawajalipwa na ni malimbikizo ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine tena, mwaka 2003 tulihoji sana na tangu nimekuwa Mbunge tumekuwa tukihoji kuhusu madeni ya walimu. Tumezungumzia kuimarisha elimu, tumejenga madarasa, tumeongeza idadi, lakini kama hatuwezi kuangalia huyu mtendaji anayewafanya watoto wetu wabadilike Kimungu, kiakili hatufanyi lolote ni sawasawa tunalisha pua tunasahau mdomo.

#### **MBUNGE FULANI:** Waambie.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu wamekuwa wakidai madai yao ya uhamisho, wanakwenda semina hawapati fedha, wanakwenda kusoma hawapati fedha, wanakwenda hospitali hawapati fedha. Mtu anahamisha mara tatu. Haya yapo na ushahidi upo lakini tunaambiwa wanawashughulikia, hivi mpaka lini? Kweli hata sisi tufikirie kama *seating* zako kila siku wawe wanasegeza mbele utakuja hapa? Hili la madeni ya walimu upande wa Serikali za Mitaa, madeni ni bilioni 14, upande wa sekondari ni billioni nne. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu amwulize Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, tunapanua lakini walimu tunakwenda nao vizuri au tumewaweka sawa sawa? Huwa inasikitisha kwa kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niseme hili kwa uchungu, mwaka 2003 tumepewa majibu mazuri, hata sasa tunaanza kupewa majibu mazuri kweli, yaliyowekwa vizuri. Sasa uzuri wake utaisha lini kwa sababu lazima uwe na hatma, ili ahadi zitimizwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ya Serikali za Mitaa mimi bado nina matatizo nayo. Tunashukuru Wizara ya Ujenzi inatengeneza barabara, imejitahidi sana kwa kweli na napenda nimkumbushe Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa John Magufuli kwamba barabara ya Chippingo-Butundwe haijakamilika lakini kazi inafanyika. Lakini barabara za Serikali za Mitaa bado tunazona ndio tatizo lililobaki. Mimi kwangu sioni,

barabara ya kutoka Katoro kwenda Luamgasa ni tatizo kubwa, ni ya Serikali za Mitaa. Barabara ya kutoka Katoro kwenda Busanda, Msasa mpaka Kamena ni tatizo. Tumeandika barua tumeomba kama *priority*, barabara ya kwenda Kamhanga ni tatizo. Lakini fedha tunaambiwa *Spot improvement*, tutafanya *Spot improvement* hakuna barabara?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu awahoji hawa watu kwamba jamani hizi hela tunazowapa zinakwenda wapi? Nitashukuru tukipata majibu mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye Wizara ya Kilimo na Chakula. Hapa naanza kupata matatizo kidogo, mimi nafikiri tukiwasonga sana mwishowe watashindwa kuandaa Bajeti. Mwaka 2003 tuliambiwa kila Wilaya itatenga mazao mawili, moja la biashara na moja la chakula na yatapewa kipaumbele. Sasa sijui kama kuna Wilaya ambayo imesaidiwa.

**MBUNGE FULANI:** Hakuna.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwangu hakuna, Wilaya ya Geita, hakuna. Tunaomba Wizara ya Kilimo na Chakula, sasa ijiangalie upya jamani hili dude kama ni zito warudishieni wengine. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pageni basi hata mikakati ya kupata hata trekta za bei ndogo ndogo kwenye kila Tarafa angalau ionekane kuna kazi. Sasa tunaambiwa *irrigation*, hatuoni, sana sana kumchangamkia Mheshimiwa William Lukuvi kutafuta chakula cha njaa hata mvua zikinyesha hakuna kitu kinachofanyika. Hapa tuelezane ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo na Chakula hapa naomba tujirekebishe. Pia hapa naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu amwulize Waziri wa Kilimo na Chakula, swali hilo kwamba hivi hayo mazao yalishughulikiwa? Nawaomba wenzetu kwa kweli, sisi kule Majimboni wananchi wanatuhoji kule. Tusingependa tuanze kupata maswali kule, mambo yanakwenda vizuri, lakini tunakutana na maswali au ninyi hamwendi kwenye Majimbo? Tunahojiwa. Ni tatizo, watumishi wanatulalamikia na naomba wenzetu wakubali, Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba katika hili nitakalozungumza la mwisho tujaribu kuangalia jinsi ya kuwasaidia wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi wakati wa Bajeti ya Fedha ya Taifa, wakati wa kujibu hoja ya Mheshimiwa Ibrahim Marwa, mimi nilifikiria kidogo, mwanzoni nilikwenda nikasoma *Hansard*, nikasema kwa nini maneno haya yamesemwa namna hii, lakini nikaona kwamba Mheshimiwa Waziri anajaribu kuukwepa ukweli. *We don't want to call a spade, a spade but we call a spade, a big spoon.*

Mheshimiwa anasema watu wa *TRA* wa kutoka katika Mkoa mmoja ni 15%, 15% katika watu gani, watu wapigiwe hesabu, asilimia 15 katika Mkoa mmoja wakati kuna Mikoa 21 na makabila zaidi ya 120. Sasa hii nyingine ina nini, lazima tuangalie kwamba

kuna haja ya kuangalia kwa nini hatuwezi kuisaidia, *we can not blame you*, ni kweli, ni ya kihistoria.

Mimi nakumbuka mwaka 1990 wakati huo vijana wa Chuo Kikuu wanafukuzwa wakati Tabora wanaripoti watu watano, Mkoa wa Kilimanjaro walikuwa wanaripoti watu kama mia tatu na kitu. Sasa hilo haliwezi kuwa kosa lako lakini ni kuangalia je, namna gani tuwasaidie hawa wengine. Siyo jibu la kusema kwamba unaeleezea ukabila wakati huwezi kuliondoa lipo, wamesoma hawa watu, mimi nimekwenda na Kamati ya Huduma za Jamii, nimetembelea Mkoa wa Kilimanjaro mzima hata watoto wenyewe unawaona *they fill a school* kuliko watoto wa Mikoa mingine niliyokwenda. Sasa na wengine tuwajengee hiyo *spirit waweze ku-move*, lakini ukisimama unasema ahaa, ubaguzi, nini, unaruka ruka pale, hapana siyo hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba yatafutwe majibu yanayostahili, tusifanye kazi kwa kufanya *character assassination* kwa Mbunge alichoeleza ni kwamba *i-reflect* ya Utaifa. Mimi namkumbuka Baba wa Taifa, Marehemu Julius K. Nyerere, kwa kweli natamani kulia kwa jibu hilo. Ndiyo maana juzi Mheshimiwa Ernest Mabina aliomba, sisi Geita tumejenga maboma 800, wananchi ndio wamezinduka sasa hivi, wao walikuwa ni kuo na kuchunga ng'ombe basi, sasa wamezinduka, wamejenga maboma 800. Tunaomba Waziri wa Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Joseph Mungai, atusaidie tutoke huko, vinginevyo tutaambiwa kwamba tunaleta ubaguzi , maboma 800 ni mengi.

Kuhusu shule za sekondari kila Kata ina maboma na tuna shule 33. Mheshimiwa Waziri Mkuu tunaomba kwa kuwa umetaja suala la MMES, tunaomba sisi watu wa Geita lianzie kwetu kwa sababu sisi tumeshaanza. Mheshimiwa Joseph Mungai, tunamkaribisha aje aone yale madarasa ili aweze kupitisha uamuzi wa pesa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri inayoonyesha kwa lugha rahisi kabisa jinsi Serikali ilivyotekeleza kwa umahiri kabisa mpango wake wa mwaka wa fedha uliopita na kuangalia mpango unaokuja wa mwaka 2004/2005. Kwa uhakika hata kama huna macho utakuwa umeona barabara zinavyojengwa, utakuwa umeona upanuzi na uboreshaji wa huduma za afya, utakuwa umeona upanuzi na uboreshaji wa elimu ya msingi, upanuzi na uboreshaji huduma za maji, utaona ujenzi wa kuaminiana na kujenga amani na majirani zetu, kuleta na kuboresha huduma za utalii, watumishi wa Serikali sasa wana matumaini na wanaonekana kabisa kwamba wana shughuli wanayofanya ya kuwashudumia wananchi na mawasiliano nchi nzima yamepanuliwa. Hongereni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwenye Jimbo langu la Uchaguzi sasa unawenza kupata mawasiliano ya *Celtel* katika Tarafa zote na umeme wa Vijiji unapanuliwa.

Kwa hiyo, napenda sana kuipongeza Serikali kwa kweli kwa utekelezaji wake ambao hautetereki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hoja yangu leo itakuwa furaha kubwa ambayo nimeipata hapa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kutangaza kwamba mpango wa *SEDEP* sasa utaanza kwa yakini na kwamba unaanza na nyota njema ya kupunguza ada za elimu ya sekondari hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ningependa tusitumie hili jina la MMES maana mtoto ukimwita Shida atapata shida maisha yake yote. Sasa tukiita mpango huu MMES tutaanza ku-*mess* tangu mwanzo, tuuite mpango huu *SEDEP* kama ulivyoitwa ili uweze kuleta matumaini yale ambayo tunayategemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huu unaonyesha kabisa kwamba Serikali inasikia ikiambiwa na kwa kweli mpango huu unatuletea matumaini makubwa kwa sababu hapo nyuma kama tulivyokuwa tunaeleza hapa Bungeni tangu mwaka 2001. Watoto wetu wanaoingia katika elimu ya sekondari ni wachache sana na moja ya sababu inayofanya wapungue sana ni ada kubwa inayochangiwa na wazazi katika kuwasomesha watoto, hasa watoto wanapojunga na darasa la tisa au *Form One*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hiyo ningependa sana niishauri Serikali igawanye kuchangia gharama ya sekondari katika mafungu matatu. Fungu la kwanza, lichukue mfano wa mpango wa MMEM ambao majengo ya shule yamekuwa yakijengwa kwa kushirikiana kati ya wananchi na Serikali. Wananchi wanaleta mchanga, mawe, kokoto, wanachimba viwanja na kutayarisha yale ambayo wananchi wana uwezo nayo. Hili liwe kwa wananchi wote wanaokaa katika Kata ambapo Sekondari inajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuwepo na mchango wa Serikali Kuu na hii iwe ni kununua vifaa vya madukani, mabati, sementi, *ceiling board* na mambo ya namna hiyo. Serikali pia ipunguze ada kama ilivyoahidi katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini ijenge yale majengo makubwa ambayo wananchi hawayawezi, kwa mfano, mabwalo ya kufanyia mitihani na kulia chakula wanafunzi. Haya wananchi hawayawezi, kwa hiyo, haya kwa yakini yajengwe na Wizara. Wizara pia ilipie mitihani yote ya shule, *mock* na mitihani ya Taifa ya *Form Two*, *Form Four* na *Form Six* ili mtoto asisome, akafika *Form Four* mzazi wake akakosa pesa ya                       kulipa mtihani basi akawa hakufanya mtihani na kwa hiyo hakufaidika na elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya sekondari ni tofauti kabisa na elimu ya msingi, inahitaji maabara, kemikali na inahitaji *furniture* ambazo ni nzuri kwa ajili ya maabara hizi za sayansi. Kwa hiyo, hizi maabara zijengwe na Serikali na vifaa vyake viwekwe na Serikali. Halafu Serikali inunue vitabu vya kiada na ziada. Hapo awali nilipendekeza kwamba kama shule zingekuwa na mtandao na Wizara ikawa na tovuti inayoweka vitabu vyote vile vya kiada na ziada basi shule zingeweza ku-*download* vitabu hivyo zenyewe na kuhakikisha kwamba zina-*print* vitabu vya kutosha kwa ajili ya watoto ambao wanasona katika shule hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu ya uchangiaji iwe sasa ya mzazi wa mwanafunzi ambaye atalipa ada ambayo imepunguzwa, atamlipia mwanawewe chakula, atamnunulia nguo na sare za shule, atatoa tahadhari na kununua madaftari. Ukijumlisha ada hii na kama Serikali itakuwa imepunguza ada hii vya kutosha, basi gharama hizi haziwezi kuzidi shilingi 50,000. Mkulima au mfugaji akijitahidi anaweza kujikwamua kumpeleka mtoto shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa mpango huu tungependa sana utekelezaji huu uwe kama ulivyotekelawa MMEM. Fedha za mpango huu zipitie na kusimamiwa na idara za elimu katika Wilaya ili ufuatiliaji na usimamizi wa Madiwani uwe dhahiri. Hatua hii itatuwezesha kwenda mahali ambapo tumefika maana sasa tuna uzoefu wa kutosha wa miaka mitatu ya MMEM, kwa hiyo tunaweza kusimamia miradi hii. Inapokuja kwenye kujenga majengo makubwa basi Wizara isimamie moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine na hili linategemea uwezo na ni kiasi gani mkopo huu ambao tunapata kwa ajili ya mpango huu wa *SEDEP*, karibu nusu ya shule zote za sekondari zinaendeshwa na jumuiya mbalimbali. Zinaendeshwa na Jumuiya za Dini kama Kanisa la Kikatoliki, Kanisa la KKKT, Kanisa la Anglikana, Baraza Kuu la Waislam wa Tanzania na Jumuiya nyingine za Waislam, Jumuiya ya Wazazi ya CCM na watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu zipo shule za namna hii za sekondari 13 ambazo zinasomesha watoto karibu 6,000. Kati ya hao watoto 6,000 ni watoto 700 peke yake ambao wanatoka Mwanga. Kwa hiyo, watoto karibu 5,300 wanatoka sehemu zote za Tanzania. Shule hizi ni muhimu sana zinafanya watoto wetu wote wa Tanzania kusoma mahali pamoja na kwa kweli zinatoa mchango mkubwa katika kutoa elimu ya sekondari kwa watoto wa Kitanzania. Kama kuna uwezo shule hizi nazo zina matatizo makubwa. Zina matatizo ya walimu, vitabu vya kiada na ziada, vifaa vya maabara na ningependekeza Wizara ifikirie ni jinsi gani inavyoweza kuwapa kitu kama *starter pack* hivi ili ziweze kujiendesha na kutoa kiwango cha elimu ambacho kinakubalika, kwa sababu zinasomesha karibu nusu ya watoto wa Kitanzania.

Lingine ambalo ningependa kulisema, ningependa kuipongeza Serikali kwanza kwa kuleta hapa Bungeni mwezi Aprili, 2004 Bajeti ya kusomesha walimu. Kwa kweli shule za sekondari hazina walimu na zilizozidiwa sana na ambazo ziko hoi ni za kule Vijijini. Walimu wale wanaokwenda kule Vijijini kwa kweli hawana fursa sawa na wale walioko Mijini. Ingekuwa vizuri walimu hawa wa Vijijini wapewe motisha kama *Kijiji allowance, something* ambayo itawavutia walimu hawa wapende kufanya kazi yao na waifanye vizuri katika maeneo ya Vijijini. Kwa sababu mpango huu nia yake itakamilika na sehemu yake kubwa itatekelezwa katika maeneo ya Vijijini, swala la kuwapatia walimu wa vijijini lipewe kipaumbele kikubwa.

Kama mwaka mmoja au mwaka mmoja na nusu hivi tuliondoa watoto kama 30,000 waliokuwa wanapata elimu ya sekondari kwa kupitia elimu ya watu wazima au mpango kama ule wa MEMKWA hivi, elimu ya sekondari kwa wale ambao wameikosa. Sasa utaratibu huu wa *SEDEP* hebu na wenyewe ufikirie ni jinsi gani tunavyoweza

kusaidia na watoto wengine hawa ambao labda wangepata elimu ya sekondari lakini wameikosa kwa sababu pengine wakati walipofika darasa la saba ama hawakupata nafasi ya kujiunga na darasa la tisa ama walikuwa hawana uwezo.

Mimi siamini kabisa kwamba wote tulipokuwa darasa la saba tulikuwa na akili nydingi kabisa tukaweza kufaulu na hatukuweza kuongeza juhudzi zetu tulipoendelea mbele. Wengine wanaanza pole pole, wanapokuwa watu wazima kipaji chao cha kupokea elimu kinaongezeka. Kwa hiyo, tungetafuta njia ya kuwasaidia hawa vijana. (*Makofi*)

Mwisho nilikuwa napenda sana nimpongeze Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa hotuba yake nzuri sana hapa ndani. Mimi nayaona haya madeski ya wenzetu wa Upinzani hapa yapo wazi lakini nadhani waliopo watapeleka taarifa kule. Kwa kweli ukisilikiza hotuba ya Mheshimiwa Danhi Makanga, unajua ni kwa nini hawa wenzetu hasa wale wenye nia ya kulijenga Taifa lenye amani basi wanarudi CCM. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niipongeze Serikali kwa kweli katika Bajeti iliyopita kwa kutoa leseni bure za biashara kwa vijana. Vijana wengi wamefurahia sana suala hili na litawaondoa vijana wetu wengi sana kwenye vijiwe. (*Makofi*)

Lakini ingekuwa vizuri basi kwa kuwa tumeondoa leseni hizi tufundishe vijana wengi ambao wanatoka sekondari hawapati nafasi ya kuendelea na elimu ya juu tuingize au tuwe na mpango wa kupanua elimu ya *VETA* ambayo inawawezesha vijana hawa waweze kuujajiri wenyewe. Pia tuwe na mpango kamambe wa kuwasaidia kukopa vifaa vya fani zao wakishamaliza elimu hiyo ili vijana wengi zaidi waweze kufaidika na nafasi

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo yote, napenda sasa rasmi niunge mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri aliyoiwasilisha hapa Bungeni. Kwa hakika ina mwelekeo wa maendeleo kwa wananchi na kuichangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni wajibu, vinginevyo ingekuwa tunasimama na kuunga mkono kwamba tunapitisha mia kwa mia. Kwa msingi huo mimi naunga mkono mia kwa mia Bajeti ya Mheshimiwa Waziri kwa jinsi ilivyokuwa makini kwa maendeleo ya wananchi. (*Makofi*)

La pili, nimpongeza sana kaka yangu Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kurudi katika Ubunge mara ya pili kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

La tatu, niwape pole wenzetu wote ambao walipata matatizo ya kufiwa na wazazi wao, ndugu na waliopata ajali za magari na Mheshimiwa Mama Anne Kilango, kwa kuvamiwa na majambazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, sasa nichukue nafasi ya kuchangia katika maeneo mbalimbali kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nianze na suala la athari za Ukimwi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu ameелееza vizuri hapa katika hotuba yake kwamba kuna dawa ambazo zinasaidia waathirika si kwa msingi wa kupona ugonjwa wa Ukimwi, ila kuwawezesha kuongeza muda wa maisha yao na dawa hizo zinatolewa bure.

Mimi nilikuwa naomba nimweleza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba nina ushahidi kwamba dawa hizi hazitolewi bure katika hospitali au kwenye maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya kuwahudumia wagonjwa hao, zinanunuliwa dawa hizo kwa shilingi 35,000/= kwa dozi ya mwezi mmoja na ukienda kwenye hospitali za *private* unakuta zinauzwa kwa shilingi 42,000=/. Nipo tayari kutoa ushahidi akihitaji hapo baadaye kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa misingi hiyo mimi nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu afuatilie suala hili kama anavyofuatilia masuala mengine yoyote kwa sababu kama hatutafanya juhudhi, hatutakuwa na wapiga kura itakapofika mwaka 2005. Kwa sababu wale wenye uwezo tutakuwa nao na wale ambao hawana uwezo wataondoka mapema na hao ndiyo wanaotupigia kura sisi kuliko ambao tunawekeana mtima nyongo wakati wa uchaguzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa misingi hiyo mimi nilikuwa naomba fungu la Mheshimiwa Waziri wa Afya lionezwe ili kukidhi haja ya dawa hizi za wagonjwa wa Ukimwi ambao tunawaona sana kwenye *television* walivyoathirika kwa kweli ukiangalia zile picha zao unaweza ukasema wale ambao hawaolewa, hawaolewi na wala hawaoi kwa upande wa wanaume kwa misingi ya uwoga wanavyoonekana katika zile *television* kuhusiana na wagonjwa walioathirika na Ukimwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nizungumzie suala la athari zinazowapata vijana wetu wanaokula dawa za kulevyta na bangi. Kwa kweli hili ni tatizo kubwa sana, vijana ambao tunawategemea ndiyo wanapoteza kumbukumbu za akili, wanakuwa ni matatizo katika familia, lakini hakuna mahali ambapo wameelezea au mkakati uliowekwa na Serikali wa kuokoa hawa waathirika wa dawa za kulevyta na bangi.

Mimi nilikuwa naomba sana ikiwa magonjwa mengine yanapatiwa dawa za kuwanusuru basi hawa vijana Wizara inayohusika iwatengee fungu maalum la fedha kwa ajili ya kuwanusuru hawa vijana. Kwa kweli wamekuwa waoga hata kujitokeza kwa sababu ya utaratibu wa Polisi, vijana hao ukamatwa. Kwa misingi hiyo, wanashindwa kujitokeza kama wagonjwa, wanaishia tu kwa kujificha ficha, lakini Serikali ikitamka kwamba wanaweza wakasaidiwa wanaweza wakajitokeza na sisi wazazi ambao tuna watoto wa aina hiyo tutapata nafuu. Tunakuomba sana Mheshimiwa Waziri hili sikuliona mahali popote kwenye hotuba yako lilipowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze *RPC* wa Mkoa wa Mara kwa kukamata zile bangi kwenye yale masanduku, kwa kweli wamefanya kazi nzito, hongera

sana na tunawatakia kila kheri katika shughuli nzito kama hizo na pia wananchi wanaotoa taarifa hizo kwa sababu wao ndiyo wanatumwa mabegi baadhi yao wakanunue, wanapanga na wanawapa fedha pengine kidogo kwa hiyo nao wanakasirika wanasema ehee! leo utaona, unanipa shilingi 200/= utakutana na wahusika, wanatoa taarifa hizo kwa usiri kabisa na mimi nawashukuru kwamba hawatoi siri Polisi kwa siku hizi. Zamani ilikuwa ukienda kutoa taarifa siku ya pili unapambana na matatizo kwa wale ambao umekwenda kuwataja katika hali ya uhalifu wanaoufanya. Kwa misingi hiyo nawapongeza wote wawili wananchi na *RPC* wa Mkoa wa Mara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele kingine ambacho nimeona nikizungumzie hapa ni kuwapongeza Wanahabari wote wanaotuhudumia hapa Bungeni, kwa kweli tunaonekana, watoto wanafurahi, baba zao wanafurahi na mama wanafurahi kwamba tuko Bungeni wanatuona kwenye magazeti na kwenye *television*, tunawashukuru sana, naona kila kona hapa kuna kamera zinatumulika na hii ni hali ya Sayansi na Teknolojia tunayoipata kwa hivi sasa, tunawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka kuzungumzia kuhusu Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo na Wizara ya Nishati na Madini kwa upande wa umeme. Kwa kweli mimi nasema Waheshimiwa hawa Mawaziri wanajitihada sana kutekeleza wajibu wao. Lakini kuna mapungufu yanayofanywa na watendaji.

Mimi naona niseme tu hapa ili waelewa kwa sababu Waheshimiwa Mawaziri hawa wanapotembelea Mikoa wanapewa taarifa nzuri, wanaandaliwa vizuri tukiwemo na sisi Waheshimiwa Wabunge tunaalikwa tunakuwa nao katika shughuli ambazo wanapita kuzikagua. Lakini utakuta matatizo yanayojitokeza ni ile tabia ya kuwadhulumu wananchi katika ulipaji wa bili za maji na bili za umeme. Mtu akifungiwa umeme wanaweka na mita, kwa misingi kwamba ikizunguka mita inajiandika, ikishajiandika hatimaye unapata bili yako kulingana na jinsi ulivyotumia ule umeme.

Lakini Mameneja wengine watumishi wao hawaendi kukagua mapema badala yake wanafanya makisio tu kwamba nyumba hii ina watu sita basi wanatumia umeme wa shilingi 200,000/=, lakini sasa nini faida ya kuweka mita katika nyumba zetu kwa matumizi ya umeme au kwa matumizi ya maji ikiwa wao wanakaa kufanya makadirio kwa ajili ya bili za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanadhulumiwa sana, kwa kweli mimi nilikuwa naomba Waheshimiwa Mawaziri hawa waangalie na mimi nina ushahidi mara nyingi ninapochangia hapa napenda kuwahakikishia kwamba nina ushahidi hata kama wakiniambia nitoe ushahidi Mheshimiwa Mbunge natoa ushahidi.

Katika Jiji la Dar es Salaam wana tabia hiyo na Mkoa wangu wa Shinyanga wanapenda sana kufanya makadirio kwa wananchi kwa matumizi ya maji na matumizi ya umeme hili kwa kweli watu hawalipendi. Kwa sababu wengine wana visima katika maeneo yao lakini utakuta bili za maji ni za juu sana kulikoni? Mtu ana kisima pale, lakini bado anaonekana ana matumizi makubwa kwa sababu ya makadirio. Kwa kweli hilo Waheshimiwa Mawaziri na Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ye ye ndiye

msimamizi mkuu wa masuala haya kama ulivyonutangazia Mawaziri wako ni wa miavuli basi waendelea kufanya vizuri katika suala zima la kazi zao hasa kwa upande wa watendaji, wawafulilie wasiwaache wanawadhulumu wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu Utawala Bora umeelezea hapa kwa upande wa Mahakama. Mimi nina tatizo moja ambalo mimi binafsi silipendi na wananchi pia hawalipendi. Mtindo wa Mawakili wetu kuchelewesha kesi kwa makusudi kwa ujanja ujanja tu anakwenda mtu Mahakamani, anaambwi kesi imeahirishwa kwa sababu Wakili bado hajaweka sawa masuala fulani fulani au mteja wake anaumwa au mteja wake hayupo ana matatizo, lakini ukizunguka pale pale Mahakamani unamwona amevaa na korti lake pale kwa vile tu yeze ana uwezo wa kubabaisha wenzake katika mambo ya haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu hivyo ni vyombo vyako uangalie hawa Mawakili wako chini ya nani, wanafanya mambo jinsi wanavyotaka wao wenyewe. Kama ingekuwa Polisi hapa ingekuwa matatizo mengi sana, lakini hawa Mawakili mnawaachia uhuru mno, tunaomba muwasiliane nao, muwaeleze linalopaswa kwa faida ya wananchi na sisi wenyewe ambaa baadhi yetu tuna matatizo ya aina hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kilimo, kila mtu hapa anasema kwamba kilimo ni uti wa mgongo katika suala la uchumi. Lakini wanashahau mlimaji ni nani? Wanasemea uti wa mgongo tu mkulima hapo ni mwanamke awezeshwe ili aweze kulima, mikopo inayotolewa sasa hivi Mheshimiwa Waziri Mkuu haitoshelezi mwanamke kuweza kujikwamua katika hali ya mbaya ya uchumi inayomkabili, na nyinyi mnajua kwamba mwanamke akiwa na uchumi basi familia hiyo itakuwa na maendeleo mazuri. Kwa sababu wanawake tuna mkono mmoja tu wa kupokea na kutumia nyumbani, lakini wenzetu mikono yenu ni miwili ikipokea kulia, kushoto dakika hiyo hiyo imekwishatoka na hali inakuwa duni katika familia nyingi tu kwa mtindo huo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu aliangalie hili ili mapato ya wanawake yaongezwe kutokana na mikopo ambayo inatolewa kuititia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki nipigiwe kengele, nimpongeze tena Mheshimiwa Waziri Mkuu na ninaunga mkono hoja hii mia kwa mia. (*Makofi*)

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuchangia naomba niungane na Watanzania wenzangu kumpa pole Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa ugonjwa wake na tumwombe Mwenyezi Mungu amjalie

ili aweze kupona haraka arejee hapa nchini kushirikiana nasi katika ujenzi wa Taifa na *inshallah*, Mwenyezi Mungu atamjalia.

La pili, niungane na wenzangu kuwapa pole wale wote waliopata matatizo mbalimbali wakati wakija Bungeni, tunawapa pole sana na tunashukuru kwamba Mwenyezi Mungu amewanusuru maana pamoja na mikasa waliyopata lakini hawakupoteza maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niungane na wenzangu kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Afrika na hasa kumpongeza Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Rais wa Kwanza wa Bunge la Afrika na Rais wa Kwanza wa Bunge la Afrika Mwanamke wa Kitanzania. Ni fahari ya pekee kwa Wanawake wa Tanzania tunaamini ana uwezo na atatuwakilisha vizuri kabisa. Kama tumeweza kutoa Rais wa Kwanza wa Bunge la Afrika nina hakika tunaweza kutoa hata Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mwanamke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile niungane na wananchi wa Bariadi na wana-CCM wote kumpongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa ushindi wa kishindo katika Jimbo la Bariadi Mashariki. Kwa kweli ushindi wake ni ishara dhahiri ya wananchi wa Tanzania kwamba wana imani kubwa na Chama cha Mapinduzi na sera zake ambazo ndiyo zimeifikisha nchi hii hapa kwa maendeleo mazuri tuliyonayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niipongeze *Twiga Stars* kwa kuiperusha Bendera ya Tanzania vizuri na kutuletea ushindi. Tunawatachia kila la kheri ili waendelee kuiperusha Bendera ya Tanzania na kuendelea kutupatia ushindi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe wito kwa Watanzania wote tuichangie timu yetu kwa hali na mali. Natumaini tukiendelea kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu basi watafanikiwa waje na ushindi kamambe hadi mwisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo niungane na wenzangu kuipongeza hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo kwa kweli imeonyesha mafanikio ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika utekelezaji wake wa Ilani ya CCM na Dira ya Maendeleo ya 2025. Lakini kubwa zaidi juzi Jumamosi wakati tunapewa utambulisho hapa tuliona vile vile kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu imezingatia uwiano wa jinsia vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaipongeza sana Ofisi ya Waziri Mkuu. Ninaamini kwamba wanawake wote waliochaguliwa kushika vitengo mbalimbali wamepata nafasi hizo kwa sababu wanayo elimu na uwezo wa kumudu madaraka waliyopewa na tunaomba Mwenyezi Mungu awajalie. Sasa kwa mfano huu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, tunategemea basi na Wizara nyingine zitafuata. (*Makofi*)

Nimesema awali kwamba Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi imefanya kazi nzuri. Sisi watu wa Mikoa ya Lindi na Mtwara hatuna budi kutoa shukrani kubwa sana kwa Serikali maana kutokana na kukamilika kwa Daraja la Mkapa tunaweza kupita

kwenda nyumbani kule Kusini toka Dar es Salaam bila wasiwasi wowote. Watani zetu Wandengereko waliokuwa wanatusubiri tukwame pale safari hii tumewapiga chenga. Maana hatulali kivukoni wala hatununui kambale wao, sisi inakuwa tukitoka Ikwiriri ni mguu tukikwama mbele lakini tunakuwa tumeshavuka eneo la Wandengereko. Kwa hiyo, tunawapa pole watani zetu ile biashara imekwisha sasa sisi tunapeta. Hiyo yote ni kazi ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama mwalimu nitakuwa na upungufu wa fadhila bila kuelezea juu ya mafanikio ya elimu. Sasa hivi ukienda vijijini unaona kweli tunayo madarasa, hata mwanafunzi anakuwa na hamu kwenda shule kwa kuona tu madarasa. Maana kila kitu kikiwa kizuri mtu anavutiwa, inawezekana wanafunzi walikuwa hawaendi shule kwa sababu ya madarasa yale ya mbavu za mbwa, lakini sasa hivi madarasa yanavutia. Hii yote ni juhudî ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mengi, lakini naona niyataje kidogo na mengine nitayataja wakati nachangia kwenye Wizara husika. Naomba nianze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuangalia maeneo yafuatayo:-

Kwanza kumpongeza kwa kutuzindulia Sera ya Uwezeshaji, Sera hii inatupa matumaini sana, ukisoma ile dira inasema uwezeshaji wa wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za uchumi ni sehemu ya Dira ya Maendeleo ya mwaka 2025. Sasa ukiisoma ile Dira peke yake inakupa matumaini makubwa sana. Katika kifungu kile cha pili, katika ukurasa wa tano kwenye mwelekeo inasema hivi: “Sera ya Uwezeshaji italenga katika maeneo yenye kuleta matokeo ya haraka hasa yale yanayogusa maisha ya wananchi yenye ujasirimali katika kilimo, ufugaji, uvuvi na kadhalika.”

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nataka kwenda kwenye kilimo. Katika Wizara ya Kilimo na Chakula, mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2004, Bunge lako Tukufu liliidhinisha fedha kwa ajili ya Mfuko wa Pembejeo ambapo wananchi walikuwa na haki ya kukopa kwa ajili ya kununua pembejeo na matrekta. Lakini Kamati ya Mfuko wa Pembejeo husika haina matatizo, inachanganua kuona kwamba masharti yanayotakiwa yote yamezingatiwa na mwananchi, lakini ikienda kwenye Benki iliyopelekewa zile fedha ndiyo kuna kasheshe sasa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliuliza katika Bunge hili, Benki ile inayoitwa *EXIM* mhusika ni nani? Kwa nini tumepeleka mabilioni yetu kule? Fedha hizi zilitengwa kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wajiedeleze. Nizungumzie hasa mkopo wa matrekta, maana hata mwelekeo wa CCM unasema tutajitoa kwenye kilimo cha majembe twende kwenye kilimo cha matrekta na ndiyo maana nafikiri Serikali ya CCM ilitenga fedha hizi za mikopo ya matrekta. Lakini ukienda kukopa *EXIM Bank* baada ya kupata kibali kule kwenye Mfuko wa Pembejeo utazungushwa ile ngumu, tunauliza benki hii ni ya nani? Kwa nini kunakuwa na mzunguko mkubwa hivyo? (*Makofî*)

Labda vile vile wanahitaji watufuatilie kwa karibu sana kwa tabia ya Watanzania. Lakini tuijulize kutokana na fedha ambazo tumetenga mwaka wa fedha uliopita ni

wananchi wangapi wameweza kupewa mikopo ya matrekta na kama fedha zimebakizilizobaki ni kiasi gani? Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula atueleze hapa ili tujue fedha ambazo Bunge lako Tukufu liliidhinisha kwamba zipo pale na bado wananchi wana haki ya kuzikopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana mimi ni mmojawapo, nilikwenda pale nilipiga hodi hata sikutazamwa, nikatoa na kadi yangu jamani niko kwenye Kamati mkiwa na nafasi basi niitwe sijaitwa mpaka leo. Yule *MD* anasema hana nafasi ya kuonana na Mbunge nafikiri, sina hakika. Sasa kama mimi mwakilishi wa wananchi nafanywa hivyo je, mkulima wa kawaida atapata?

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo kabisa!

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, lengo letu kutenga zile fedha ni kuwawezesha wananchi. Naomba sana tuliangalie hili. Hivi Mfuko wa Pembejeo kule nyuma ulikuwa unatoa mikopo wenyewe, tulikosea taratibu sisi wenyewe katika mkopo ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikosea utaratibu sisi wenyewe kwa nini Mfuko wa Pembejeo nao basi usiweke utaratibu wa kushika dhamana ile ya mwananchi, ukatoa mkopo kwa utaratibu unaotakiwa, nina hakika pale tutakuwa na heshima zaidi kwa wananchi wote kuliko kwenda kwenye benki ya watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili katika ukurasa wa 32 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia juu ya viwanda na amezungumzia mchango wa *SIDO*. Sisi Mkoa wa Lindi tuna eneo la *SIDO* kubwa tu, lakini yale mabanda ni magofu yamekaa tupu. Mimi nina hakika pale tungeweza tukapaendeleza vizuri sana wananchi wa Lindi, lakini hatuna umeme wa uhakika na hapa imeelezwa vizuri sana kwenye hotuba yake Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Mkoa wa Lindi hatuna kiwanda hata kimoja, *SIDO* iko pale, nina hakika wawekezaji hawawezi kuja kwa sababu hatuna umeme. Kilio cha umeme wa kuaminika ndiyo kikubwa katika Mkoa wa Lindi. Hivi mwekezaji gani atakuja hata utandawazi tunaouzungumzia sisi tutautanda wapi bila umeme. Hata hiyo *Internet* tutaisoma?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kabisa kwamba Serikali wanazungumzia kuna Mradi wa *Mnazi Bay*. Lakini kwa masikitiko naungana na wananchi wenzangu wa Mkoa wa Lindi wote kwamba *Songo Songo Gas* imetoka Lindi ambako hakuna umeme inakuja Dar es Salaam kuongeza nguvu. Ama kweli hata kwenye Biblia waliandika...

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo!

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** “Wale wenyewe nacho wataongezewa na wasionacho watanyang’anywa na kile kidogo.” Jamani na sisi wananchi wa Mkoa wa Lindi tunahitaj maendeleo na tunahitaji sana huo umeme. Pamoja na mipango mizuri ya

*Mnazi Bay*, lakini *Mnazi Bay* si leo wala kesho. *Songo Songo Gas* iko pale. Serikali ya CCM ni sikuvi, Serikali ya CCM inapenda maendeleo ya wananchi, Serikali ya CCM inajali wananchi na wananchi wa Mkoa wa Lindi kilio chetu ni umeme wa uhakika. Tunaomba mtuangalie. Pale Somanga mkiongeza nguvu nina hakika umeme unawenza kufika Lindi na Mtwara kuliko tusubiri mpaka *Mnazi Bay* sijui ni mwaka gani? Kama ni *Mnazi Bay*, basi mtupe matumaini ya kweli ili Sera hii ya Uwezesaji iwe ya uhakika na sisi Mkoa wa Lindi na Mtwara tuweze kuwezesha maana bila umeme wa uhakika uwezesaji huu kwetu sisi utakuwa ni ndoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho niligusie haraka haraka ni juu ya Sera ya Maafa. Napongeza kwamba Sera ya Maafa ipo na imeainisha vizuri kwamba kuna njia ya kuzuia na kutaka kujifunza kutokana na maafa yaliyotokea.

Sisi tulikumbwa na *El-Nino* kule Mkoa wa Lindi na Mtwara na maeneo yanayosumbua ni daraja la Nyagao, eneo la Chipite, daraja la Nangoe juzi juzi wananchi wamekufa pale gari limetumbukia, lakini toka maafa yametokea ni miaka 12 sasa. Labda tulikuwa tunasubiri sera maana katika sera hii wanasema ni lazima *Preventive Actions* zichukuliwe haraka. Sasa kwa sababu sera ipo basi tunategemea utekelezaji.

Juzi juzi hapa Mheshimiwa Rais wakati anatoka likizo Masasi, vijana wetu pale Nyagao kwa sababu Mto Lukuledi ulifurika, walilazimika kusimama kando kando ya daraja lile la Nyagao ili kuonyesha njia msafara wa Mheshimiwa Rais upite. Nawapongeza wale vijana, kwa sababu Mto ule una mamba na una nyoka, lakini walikubali kusimama kuhakikisha kiongozi wao wa nchi anapita kwa usalama. Je, Serikali hailioni hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaacha mpaka lini eneo lile linakaa vile kwa miaka 12. Kweli kuna *feasibility study*, lakini kuna *alternative*. Tukipita barabara ya sasa hivi eneo la Chipite ni mafuriko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia machache katika hotuba nzuri ya Mheshimiwa Frederick Sumaye, Waziri Mkuu. Kwanza naunga mkono kwa asilimia mia moja kwa mia moja au asilimia mia mbili kwa mia mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwape pole wale waliopatwa na misiba Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na mdogo wake Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kuondokewa na mzazi wao, Mwenyezi Mungu aiweke mahali pema peponi roho ya Marehemu. *Amin.*

Simsahau ndugu yangu, bwana mdogo, Mheshimiwa Danhi Makanga. Ule wakati ameshinda nilimwambia hiyo njia uliyopitia si nzuri sasa nilikuwa nikimtabiria unabii. Kama angekumbuka yale yote niliyokuwa nimemwelezea ndiyo yamempata. Hata pale wakati amemwengua huyo mzee wake nilimpigia simu nikamwambia unaona sasa ndiyo matokeo. Sasa hiyo njia ambayo amerudi ndiyo yenyewe. Wengine wamesema hivi

ukisoma ile Biblia ya kitabu cha Luka: "Yule mwana mpotevu alidai kwa baba yake apate vitu vingi mapema, baba yake hakuwa na hila akampatia. Alipokwenda kule akatumia kweli kwa starehe, lakini baadaye alikumbuka baada ya kuwa vyote vimemwishia akasema nirudi kwa baba. Yule baba ukimfuatilia naye alimpokea bila hila, angekuwa baba wa siku hizi angesema hapana sitaki".

Sasa ndio CCM, alivyokuwa ametutukana hapa tungenesema hapana. Lakini CCM ni baba mzuri anayefanana na baba yule kwenye kitabu cha Luka Mtakatifu. Karibu sana Mheshimiwa Danhi Makanga, sisi hatuna hila tumekuchinjia ndama mnono kwa hiyo, umle, ushibe na tunakuvika na pete nyingine iliyo nzuri, tumikia Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Danhi Makanga, ameongea jambo moja zuri, timu ile ya *Real Madrid*. Timu nzuri imechukua ubingwa wa Ulaya mara tisa inafanana na Yanga. Si kazi nyepesi lakini *Real Madrid* wanapofanya kosa kidogo pale pale ndipo unapofungiwa. Kwa hiyo, lazima huku ulikokuja kwenye Chama cha Mapinduzi kimekamilika kwa hiyo, *defence* yake na *forward* yake ni nzuri tu kwa hiyo, shangilia hata mwakani utafunga magoli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nina mambo machache, la kwanza mimi nimekuwa ni msomaji mzuri wa kufuatilia matukio. Hivi Tanzania kwa suala la kilimo watu wanaokaribia idadi ya milioni 40 bado kweli tunaweza ukapata chakula kutoka Ethiopia?

Mimi hapa niliposimama nachukua kama ni hela au nini ninalishwa na mtu wa Ethiopia! Njaa inayonuka tunaomba kila siku mvua inyeshe Ethiopia wao ile mvua ndogo wanayoipata wanazalisha mpaka tunafuata kununua chakula au kinapatikana kutoka Ethiopia. Inakuja kweli?

Mheshimiwa Naibu Spika, tujiulize na twende huko nje tuwaalize kama Watanzania wako tayari kulishwa na Ethiopia. Naomba utaratibu huu tuuache na tuanze kukutana humu tuunde taratibu zinazowenza kutuwezesha sisi kuondokana na njaa. Hatuwezi kuimba njaa kwamba Tanzania ni nchi yenyenye njaa kwa kuanzia wapi? (*Makofi*)

Hivi njaa ya Tanzania tumeilea na utakapokwenda mbinguni Mungu atatuambia ninyi niliwapa raslimali kuliko nchi nyingi za Afrika. Hii njaa mliyopoteza hizi fedha ambazo mngetumia kwa elimu na kwa mambo mengine mlizitumia kununua vyakula kutoka nje visivyo na utaratibu kama Marekani ambavyo vimejaa madawa, kemikali nyingi ingieni *Jahanam*, ipo hiyo. Sasa mnakataaje? Lakini nataka kusema hivi juzi mimi nimekwenda Mbeya nimepita kwenye jimbo la Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mbarali mvua inanyesha saa 24. Wilaya ya Mbarali kwa Mkoa wa Mbeya inasadikika inaweza ikatoa mpunga wa kulisha wananchi wa Tanzania miaka mitano mfululizo. Kwa nini usipeleke hizo fedha nyingi namna hiyo tukahamasisha, ni tatizo gani lipo mpaka tupate chakula kutoka Ethiopia. Inakuja?

## **WABUNGE FULANI: Haiji!**

**MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA:** Mimi simo, nakwenda kushawishi wananchi wangu wa Jimbo la Kigoma Kaskazini kwamba katika mpango wa kilimo ambao Watanzania sasa hivi tunapata chakula kutoka Ethiopia mimi nimesema hivi ninyi hammo, hawamo. Chakula kutoka nje sababu za msingi ni zifi? Unaweza ukachukua muda mwingi kumlaumu Waziri wa Kilimo na Chakula ameshindwa kazi, lakini mimi napendekeza kuwa tukutane, tujadili na tupendekeze mambo yapi, nikubaliane na hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini leo ukimwadamisha Waziri wa Kilimo na Chakula, ameshindwa kazi unautaka wewe Uwaziri wa Kilimo na Chakula kwa mpango huu wakikupa wewe utaweza? Kama sababu ni hizo chakula kinaendelea kutoka Ethiopia. Mimi sitaki kula chakula kinachotoka nje na wala kuanzia leo naikataa.

## **WABUNGE FULANI: Utakunywa uji ?**

**MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA:** Eeh, Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuongea la pili huko nakuja.

La pili, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha kesho alete hizo shilingi bilioni 18 tuwapelekea Walimu. Maana kwenye Bajeti amesema makusanyo zaidi ya shilingi bilioni 100 kwa mwezi. Sasa hebu tufumbe macho tutafute hizo shilingi bilioni 18 tuwape kwanza halafu wawe wamepewa zile fedha wawe wamekula tuwakamate, wawajibike. Wakurugenzi hizi fedha wamekula tunao ushahidi.

Mimi nipo kwenye Kamati ya Huduma ya Jamii, wameleta pale, wamelalamika sisi tukamwita Waziri wa Elimu na Utamaduni, tukafikiri kwamba ndiyo yeye anayehusika. Walimu sasa hivi wanazunguka nchi nzima huku wanapongeza lakini wanang'unika. *Silence protest, they are protesting.* Tuwaokoe Walimu, wako katika mazingira magumu. Sasa wote wamemuatamia wanafikiri Mheshimiwa Joseph Mungai amekula fedha zao, si kweli na sio sahihi. Sasa nani amekula na vinatoka wapi zinazofikia shilingi bilioni 18?

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu mwaka 2003 tumeelezea, Waziri Mkoo uko hapa na wewe hili unalo au labda kwenye jimbo la kwako wenyewe wote wamepata, lakini kwangu ni hali ngumu sana. Naomba hizo fedha mimi nizipeleke kwenye jimbo langu kwamba hali ni ngumu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kwenda katika mazingira ya namna hii, tunakaa humu tunabembelezana, tunaelezana mbili jumlisha mbili jibu lake ni ngapi? Nne. Sasa shilingi bilioni 18 ameshafanya mahesabu tunazitaka Walimu ambao kwa muda mrefu wamekaa nyumbani hawajakwenda likizo, wamekata tamaa. Nani kwenye jimbo lake hawajakata tamaa, Jimbo la kwangu wamekataa tamaa kabisa. Sasa mimi hapa huwa naongea vizuri kwa sauti nzuri, hii sauti sasa imebadilika. Nimekwenda kule Mbeya, Mkoo wa Mkoo wa Mbeya, Mheshimiwa Matheo Qaresi, nampongeza kwa juhudhi ambazo amezifanya za kusimamia zile Shule za Msingi mahali penye moja, mbili,

tatu yeye amefanya kumi, nilikuwa kule. Amefanya kazi nzuri. Lakini Walimu wa Mbeya wanaotoka Kagera wengine waliniambia hatujakwenda likizo Mheshimiwa Mbunge kwa muda wa miaka mitano. Mdogo wangu amefariki, kaka yangu amefariki lakini nitafikaje? Hivi hapa kati yetu nani hajakwenda likizo? Wewe uliye mkubwa likizo ikifika haraka sana. Huyo aliye mdogo hawezi kwenda katika dunia ya nani? Nani hakutambua watoto au nani hakutambua walioko chini. Hawa ni watu wetu wako chini tuwasaidie. Hata wale waliosukuma watoto Yesu alisema hapana waachenai watoto wadogo waje kwangu, Ufalme wa mbinguni ni wao. Ninyi mlioko juu likizo kila siku, hawa walioko chini hapana. Hii inasemwaje? *Seriously* hizo hapo sasa tunazifunga kwanza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba yaani tunataka kuanzia kesho tupate jibu. Maana huu mpira unaodunda unakwenda kwa Mheshimiwa Joseph Mungai unadunda, unakwenda kwa Mheshimiwa Brigedia Mstaafu Hassan Ngwilizi unadunda, unakwenda kwa Mheshimiwa Basil Mramba unadunda, unakwenda kwa Mheshimiwa Mary Nagu wa Utumishi, unadunda, sasa tunakwenda wapi? Kama hakuna basi ingebidi sisi wenyewe Wabunge tutembee kushoto kulia, kushoto kulia mpaka Ikulu kwa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa basi tumwambie bwana tunaomba hizi fedha basi. Lakini hapa ndiyo mahali pa kusemea mambo haya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu naomba umwambie Waziri Mkuu anipe shilingi milioni zangu 600 za *STABEX* za kutengeneza barabara ya Mwandiga - Manyovu. Sasa sijui nani anazo? *Last time* Waziri Charles Keenja alisema shilingi millioni 600 zitatoka. Nikamwuliza Mheshimiwa John Magufuli shilingi milioni 600 zitatoka? Namwuliza Mheshimiwa Basil Mramba shilingi milioni 600. Hii *STABEX* hivi ninyi mnawaonea hawa wakulima wa Kahawa? Zao la Kahawa ndio limesaidia nchi hii kwenye uchumi huu ninyi mnafanya namna gani bwana, nani asiyejua hilo?

Mimi ni Mbunge tangu mwaka 1990, vipindi vitatu mnafikiri ni mchezo na cha nne nakwenda na cha tano cha sita ndiyo napumzika. Lakini huwezi kuniahidi kauli ya Serikali ikishasemwa lazima itimizwe. Sasa naomba sijui ni Waziri gani basi mimi namwomba Waziri Mkuu yuko hapa Mheshimiwa Frederick Sumaye, anipe hizo fedha shilingi milioni 600 nipeleke nikakamilishe ile barabara ya Mwandiga - Manyovu ni *threat* kwangu sasa hivi. Mambo gani sasa jamani?

Mheshimiwa Naibu Spika, au nije mwenyewe huko baadaye ndiyo zitoke hizo? Tufanye hivyo ndiyo utamaduni wa Watanzania. Iwe ndiyo sasa tuanze, sio lakini kama tulikuwa tunakwenda mambo yanaanza kuchenga tunakatisha tamaa. Hawa waliotuchagua hawawezi kuwa na imani wanajua kwamba mambo yanafanana na yale yale mbona Bajeti ya mwaka huu ni nzuri kuanzia mwaka 2003 na mambo mengi yameteklezwa. Hivi vitu vingine mmekwisha kusema na viko kwenye *Hansard* halafu wanasubiri, hawawezi kuona matokeo yake yanakwenda wapi. Naomba Serikali hilo ilichukue na ilifanyie kazi. Naomba vile ambavyo ni ahadi vimeshafanyiwa kazi tumalize hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu muda ni mdogo nakwenda mpango wa Elimu wa Sekondari. Kwa kweli katika hili Watanzania sasa hivi hata huko mitaani wanazipongeza sana juhudzi za Serikali. Sasa huu mpango wa ada nimefanya sensa kwenye Jimbo langu mimi nalipia watoto zaidi ya 25 hii posho ya Ubunge mpaka wakati mwengine sijui, nafikiri hili linawaadabisha Wabunge wanaotoka katika Majimbo hata wale wasiokuwa na Majimbo. Hakuna Mbunge hapa hata mmoja asiyelipia mtoto ambaye ni wa jirani kwa umaskini amba o umekithiri wapo? Labda kama yupo Mbunge ambaye analipia watoto wake ada tu wale wa jirani amba o wanamzunguka kwa kuwaona hawalipii aseme?

Hilo ni agizo tosha kwamba tuna watoto wetu amba o wazazi wao hawawezi kuwalipia ada kwa vinginevyo usipofanya hivyo wewe Mbunge basi hawa watoto hawawezi kusoma. Sasa hivi katika hii Tanzania tunataka tuwaache hata watoto wadogo wasiweze kusoma halafu unakwenda na namna gani. Umri wangu mimi ni miaka 53 hivi nimebakiza miaka mingine mingapi 20 nakufa. Sasa mniombee niende kwa Yesu nikifa siku hiyo tu. Miaka 73 mimi nafikiri itakuwa imenitosha lakini kuongeza mingine mimi nafikiri nitakuwa naleta bughudha hapa. Lakini napenda kizazi kitakachobakia kiwe kimeelimishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Gazeti moja juzi limesema hakuna Wahasibu Wizarani. Juzi tulikuwa na Mheshimiwa Omar Kwaangw', wale Maprofesa walitaka kustaafu mwaka 2005 sijui katika miaka mitatu watu watakaobaki badala ya wale Maprofesa. Hata ukitazama wengine wana miaka 59 au 60 mwaka 2005 wanamaliza watakaofundisha *University of Dar es Salaam* wako wapi. Kama tusipoanza kuwatayarisha hawa vijana wakasoma hata kama ni maskini watasoma kwa kuwa-*exempt* hiyo ada mwambie Mheshimiwa Waziri wa Fedha afanye mahesabu yake mazuri kama alivyofuta kodi nafikiri hili linawezekana. Kwani tumefuta kodi ya kichwa shilingi ngapi ukipiga mahesabu? Mbona leo Watanzania wako na furaha tu? Sasa hii ada ya mtoto kutoka Kigoma kuja kusoma Mazengo anarudishwa. Baba analipa miezi sita, muhula mmoja mwengine amekaa hakwenda, anabaki anatembea kushoto kulia kwa Mbunge, Mbunge nilipie. Wewe unakaa lini jamani Ubunge huu ni *ceremonial* tu. Unalala mahali ambapo basi tu twende na mambo haya ya kuweza kusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kweli mambo haya ni muhimu. Tuyazingatie. Mbolea naomba ujue kwamba Mkoo wa Kigoma sisi hatuna shida ya mvua. Sasa mbolea ulihesabu Mikoo mingine mitano sasa na Mkoo wa Kigoma uingizwe kwenye mbolea tupate ruzuku ya mbolea kwa sababu tuna mvua ya kutosha. Haya matrekta yaje baadaye taratibu lakini tupate mbolea kwanza. Mkoo wa Kigoma tulienaye ana juhudzi ya kilimo, ili walime, wazalishe, waweze kupata hata fedha za kusomesha watoto. Mbarali kule mpunga unastawi vizuri. Maeneo yale yote yana mpunga unastawi. Zalisheni, suala la kupata chakula kutoka Ethiopia hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja kwa mia moja. (*Makofi*)

**MHE. PAUL N. MAKOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie nafasi hii kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wa mawazo yangu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Pili, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo inazungumzia juu ya suala zima la mpango wa maendeleo kwa kipindi cha miaka mitano. Nampongeza sana. (*Makofit*)

Lakini kabla pengine sijaanza kutoa mchango wangu wa mawazo juu ya hotuba hii naomba niipongeze Serikali kwa mambo yafuatayo, kwanza naipongeza sana kwa juhudhi kubwa ambazo imezifanya kuweza kuvuta maji ya Ziwa Victoria hadi kuyaleta katika Mji wa Shinyanga. Naipongeza sana. (*Makofit*)

Pili, natumia nafasi hii vile vile kuipongeza Serikali kwa jitihada zake nzuri za kujenga barabara kutoka mpakani mwa Shinyanga na Mwanza hadi Dodoma, hongera sana. Ni matumaini yangu kwamba baada ya kukamilika barabara hii nadhani hali yetu ya uchumi sasa itakuwa inakwenda vizuri.

Vile vile natumia nafasi hii niipongeze Serikali kwa kujenga daraja la Mto Rufiji. Kwa kweli kwa muda mrefu tulikuwa tuna tatizo hilo lakini kutokana na mipango yake mizuri imeweza kufanya miradi hii na imekwenda vizuri. Tunapongeza na tunaitakia kila la kheri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo naomba nianze mchango wangu kwa mambo yafuatayo:-

Nimeipongeza Serikali lakini kama moja ya kazi ya Mbunge ni kuishauri, kuikosoa na kuisaidia ili itawale vyema. Nilikuwa napenda tu nianze mchango wangu kama namna ya ushauri. Naanza kushauri kwa upande wa mgawanyo wa fedha za Serikali tunazopewa. Naipongeza sana Serikali sasa hivi mapato yake ni mazuri, yanakwenda vizuri tu. Tunapongeza na wote wanaohusika na hilo tunawapongeza lakini bado nina wasi wasi na mgawanyo wa mapato yake katika maendeleo ya mikoa yetu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili niweze kueleweka vizuri zaidi naomba nitoe mifano, labda nianze na eneo ninalotoka. Katika kipindi hiki cha mwaka 2004/2005 Mkoo wa Shinyanga kimaendeleo jumla ya fedha ambazo wamepewa ni shilingi bilioni 1.9. Mkoo wa Mwanza umepewa shilingi bilioni 5.1 na haya usiseme sijui nayatoa wapi kwenye vitabu hivi hivi vya Serikali Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2004/2005 yapo humo. Halafu Mkoo mwingine ambao nautolea mfano tu ni Mkoo wa Morogoro umepewa shilingi bilioni 3.5. Haya Mkoo wa Tanga umepewa shilingi bilioni 3.4.

Sasa ukiangalia mpaka mwaka 2003 mimi nimezungumzia sana suala hili nikatoa mfano wa Mikoo ambayo ilikuwa imepewa fedha kidogo. Nilifikiri pengine panaweza pakatokea mabadiliko lakini inaelekea hali ni ile ile. Tulikuwa na mkoo wa Shinyanga,

Tabora, Kigoma, Rukwa hata ukiangalia zile figure hapa bado mambo ni yale yale na lingine wananiongezea tunaomba mrahaba nao hamtaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nilikuwa naomba sisi tuna mapenzi kabisa na Taifa letu hii keki tunayoipata Kitaifa, jamani tuigawe kwa usawa wote tuna matatizo. Mimi katika Mkao wangu wa Shinyanga tuna matatizo mengi. Jimboni kwangu kuna matatizo mengi. Sasa mgao wa namna hii hebu angalia tofauti iliyopo mnawenza mkasema ooh, mnajua wale sijui wana miradi, sijui akina nani na nani walikuja. *Imagine* Mkao ambao umepewa shilingi bilioni 5. Halafu uangalie na Mkao mwingine ambao umepewa shilingi bilioni 1.9 tofauti ni kubwa sana. Ni kweli mimi sizuui suala la maendeleo na wala sioni wivu lakini tunataka angalau basi ule uwiano uwe basi na mantiki. Tofauti iliyopo hapa unakuta kwa mfano ukiangalia Mkao wa Shinyanga na huu mwingine ulio juu tofauti yake ni zaidi ya shilingi bilioni 3. Sasa ndugu zangu wote tunapenda maendeleo. Niiombe Serikali katika mipango yake inayoifanya ya kugawa fedha za maendeleo basi tofauti hizi ziweze kupunguzwa. Mimi naamini ni kweli haiwezekani mikoa yote ikapewa fedha sawa, lazima tutatofautiana, lakini basi utofauti wenyewe uwe basi angalau ni wa msingi. Tofauti iliyopo hapa ni kubwa mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naishauri Serikali katika mipango yake ya maendeleo basi jambo hili ijaribu kuangaliwa. Kwa mfano, huu Mkao ambao nimeuzungumza Shinyanga, sijui na Tabora, ni Mikoa ambayo ni maskini na iko nyuma. Juzi tulikuwa na semina tunazungumzia juu ya umaskini. Kama mgao ndio huu hii Mikoa itajinasua vipi na matatizo ya umaskini. Kama haiwezi ikajenga misingi ya miundombinu.

Naishauri Serikali ijaribu kuangalia jambo hili. Basi hata ule mgao wa fedha ambao Serikali inautoa. Najua hatuwezi kulingana lakini angalau tofauti isiwe kubwa ili tuweze wote kushirikiana katika suala la maendeleo. Iko mikoa mingi. Kwa mfano, hata Rukwa safari hii wamepewa shilingi bilioni 1.4, vile vile Tabora kidogo afadhali safari hii bilioni 2 hata Shinyanga wameizidi afadhali hawa. Mtwara bilioni 1.7 wale wale.

Sasa ndugu zangu pengine mimi nilikuwa nafikiri katika mipango ya maendeleo labda niulize hivi mnapofanya mipango ya kugawa fedha za maendeleo huwa mnatumia vigezo vipi au kuna mtu fulani anakaa kule ofisini na kuweza kutoa? Sasa mimi nilikuwa nashauri Serikali yetu ijaribu kuliangalia hilo, iliweke sawa kila mmoja anahitaji maendeleo na mimi sioni wivu kwa hili lakini nataka tu ule usawa uwepo. Halafu baada ya hapo nilikuwa naomba nizungumzie suala la upungufu wa chakula. Hali ya hewa kwa mwaka huu imekuwa na matatizo sana.

Kuna maeneo ambayo yameathirika sana na kuna maeneo ambayo yana afadhali. Nazungumzia eneo ambalo natoka Kishapu, Solwa, Shinyanga Mjini, Meatu ni maeneo ambayo yameathirika sana. Mheshimiwa William Lukuvi, alikuja nikampeleka mpaka Vijijini kuna eneo fulani linaitwa Kinampanda. Wananchi wa kule si kwamba hawana uwezo wa kulima, wana uwezo mkubwa tu tatizo ni mvua. Hivi ninavyoongea na Bunge hili sehemu hizo mvua imenesha mara mbili tu hali ni mbaya sana.

**MBUNGE FULANI:** Pole sana.

**MHE. PAUL N. MAKOLO:** Kwa sasa kinachofanyika kule wale wananchi kwa kujinusuru ili waendelee kuishi wanatumia mboga moja inaitwa Songa. Wanajaribu kuitengeneza kama ugali. Kwa kweli ni aibu kuzungumzia njaa lakini inanilazimu niseme. Si vizuri mtu ukasimama unazungumzia suala la njaa. Lakini hii inanilazimu niseme. Naishukuru Serikali imeanza kutoa msaada lakini naiomba iongeze misaada zaidi hali yetu ni mbaya. Hata ile mifugo iliyopo kule nina wasi wasi kama itaishi.

**MBUNGE FULANI:** Itafariki. (*Kicheko*)

**MHE. PAUL N. MAKOLO:** Ni kweli maeneo yale ni ya wafugaji wazuri tu lakini nina wasi wasi na hali ya maisha ya mifugo pamoja na binadamu. Tunaishukuru Serikali imetusaidia, lakini tunaomba iongeze jitihada zaidi kutusaidia kwa sababu hali yetu si nzuri ni mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu, nina tazito moja katika Kijiji kimoja cha Bulimba, Kata ya Ukenyenge. Kuna mtu mmoja amewashtaki wakazi wa eneo hilo akawapeleka Mahakamani ni jamii ya Kaya kumi yenye watu wasiopungua 103. Wamepelekwa Mahakamani, uamuzi wa Mahakama ulipotolewa waliamuliwa wale watu waondoke katika yale maeneo ambayo tangu kipindi cha Operesheni Vijiji walipangwa pale sasa hawana mahali pa kulima. Mwaka 2004 hawakulima kabisa, ni kaya ya watu 103. Jitihada zetu na viongozi wa Wilaya na Mkoa tumefanya lakini hazijazaat matunda. Kwa hiyo, zile familia zenye watu 100 hivi ninavyoongea Mheshimiwa Waziri Mkuu hawakulima mwaka 2004 na hawana chakula, unisaidie. (*Makofi*)

Ni kweli kwamba kiongozi tunaheshimu Mahakama lakini pengine kwa nafasi uliyonayo unawenza ukaangalia namna ya kuwasaidia hawa watu kwa sababu hata wao hawakwenda pale walipelekwa na Operesheni Vijiji. Wamekaa pale na sasa hivi anakuja mtu mmoja kule mtu mwenyewe amehamia Igunga kule anarudi kuja kudai yale maeneo amewafikisha Mahakamani wale watu ni wakulima, hawana chakula, watu karibu 103.

Sasa ningeomba Serikali itusaidie iangalie kwa sababu hawa watu nao hawakupenda, wamepelekwa pale na Operesheni Vijiji. Sasa baada ya hapo Mheshimiwa Waziri Mkuu, mimi nakupongeza kwa hotuba yako nzuri na nakutakia mafanikio mema katika kazi yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sisi wananchi wana imani kubwa na kazi ambazo mnazifanya sasa ni nzuri, zimezaa matunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naomba niishie hapo nikutakie kila la kheri katika kazi na Serikali nzima na naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. MATHEW T. OLE-TIMAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya mwisho kwa siku ya leo au ya pili kutoka mwisho ili niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Pia, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa dhati kabisa kwa hotuba nzuri yenyе mwelekeo na ambayo imejaribu kuelezea kwa kinaganaga mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tatu. Ninampongeza sana kwa kazi nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina kigugumizi hata kidogo kusema kwamba Serikali ya Awamu ya Tatu imefanya kazi vizuri na inastahili pongezi. Ukiangalia barabara, ukiangalia shughuli za elimu, uchumi na kadhalika, mambo mengi mazuri yamefanyika na tunaipongeza Serikali ya Awamu ya Tatu kwa dhati kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hotuba ya Waziri Mkuu, nina maeneo matatu ambayo ningependa kuyachangia. Eneo la kwanza ni mchango wa wawekezaji au uwekezaji ukurasa wa 22, *paragraph* ya 31. Nakubali kwamba ni kweli uwekezaji unatoa mchango mkubwa sana kwa uchumi wa Taifa hili pamoja na kuongeza nafasi za ajira. Ila kwa suala hili la ajira kwa Mashirika, kwa Kampuni na Hoteli za Wawekezaji nina tatizo dogo, sijui kama ni dogo au ni kubwa, ni kubwa tu na tatizo lenyewe ni kwamba kuna tofauti ya viwango vya mishahara kati ya watumishi ambao ni Watanzania na watumishi ambao siyo Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu nimeongea na baadhi ya watumishi hao. Ukiwa Mtanzania na una elimu, ujuzi na uzoefu na una cheo kile kile alichonacho mwenzako wa Taifa lingine, mshahara wako ni wa chini kuliko wa yule mwingine wa Taifa lingine. Meneja kwenye hoteli za kitalii wa Kitanzania anapata takriban shilingi 150,000/= hadi shilingi 250,000/= lakini akiwa Meneja ambaye siyo Mtanzania anapata shilingi milioni 2 na zaidi, uwe ni Mzungu au Mkenya hakika unapata zaidi ya Mtanzania anayefanya kazi ile ile.

Sasa huyu Mtanzania wetu ndani ya Tanzania aliyeajiriwa lakini analipwa kiwango kidogo kuliko asiye Mtanzania, kosa lake ni nini? Ni kuwa Tanzania! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naona hali hii haikubaliki kwa sababu kuu tatu. Moja, naona ni ubaguzi unaofuata misingi ya rangi na Utaifa. Pili, naona ni kinyume na haki za kibinadamu na tatu, naona ni uvunjaji wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ukisoma sehemu ya 3, ibara ya 12(4) mpaka ya 5 inakataa ubaguzi wa aina yoyote. Sasa kwa nini ubaguzi huu unaendelea huku nchini kwetu kwenye maeneo ya kazi? Suala hili ninaomba Serikali ilitupie macho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili naita mimi ni uporwaji wa maliasili zetu na wageni. Kwa lugha nzuri tunasema wawekezaji. Ukiangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ukurasa wa 34, aya ya 47 naomba kunukuu, inasema hivi: “Kumekuwepo na malalamiko kutoka kwa baadhi ya Wananchi kupitia kwa Waheshimiwa Wabunge na Vyombo vya Habari kuhusu Sekta ya Madini. Kwa kuzingatia malalamiko hayo, Serikali

imeunda Kamati maalum ya kitaalam ya kuchunguza na kuchambua matatizo ya Sekta ya Madini na kutoa mapendekezo ya kuboresha Sera ya Madini.” Mwisho wa kunukuu.

Hayo ni kweli, lakini naomba kuongeza kwamba malalamiko na manung’uniko hayapo tu kwenye Sekta ya Madini, bali kwenye Sekta nyingine zaidi ya Madini. Kwa mfano, kwenye Sekta ya Misitu wenzetu wa Kusini wanalamika kwamba misitu ya asili inaisha na magogo yanakatwa na kusafirishwa. Hilo ni eneo lingine ambalo kuna malalamiko.

Pili, kuna malalamiko kuhusu Sekta ya Wanyamapor, Wananchi Loliondo, Wilaya ya Ngorongoro, wamelalamika miaka nenda rudi kwamba wawindaji wa Kiaribu wanamaliza wanyama, wanawinda nje ya utaratibu na wanawanyanya Wananchi. Hilo ni eneo lingine ambalo kuna malalamiko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maeneo hayo mawili, napendekeza na kumwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa heshima kubwa kwamba, kama alivyoona umuhimu wa kuunda Kamati maalum ya wataalam wa kuchunguza masuala ya Madini, utaratibu na busara hiyo hiyo itumike kuunda Kamati nyingine kuchunguza masuala ya Sekta ya Wanyamapor pamoja na Sekta ya Misitu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ni TAMISEMI au Serikali za Mitaa. Ukiangalia ukurasa wa 52 kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, *paragraph* ya 69 naomba kunukuu: “Serikali imepitisha rasmi pendelezo la kupeleka sehemu kubwa ya pato lake kwa Serikali za Mitaa kwa ajili ya maendeleo ya Wananchi kwa kutumia vigezo maalum.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa suala hili nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, naipongeza Serikali kwa kukubali na kuamua kutenga fungu kubwa kwa ajili ya maendeleo ya Wananchi kwa kupitia Halmashauri zao, ila tuna tatizo sugu na tatizo kubwa kwenye Halmashauri zetu. Matatizo makubwa ya Halmashauri zetu yanatokana na Ofisi za Wakurugenzi Watendaji. Hawa watu wanaoitwa Wakurugenzi Watendaji labda siyo wote, lakini sehemu kubwa ukiangalia ni kama wamerudufiwa na mashine moja. Matatizo ya Wilaya ya Ngorongoro na matatizo ya Wilaya nyingine kuhusu Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji karibu yanafanana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika kwa hili tukijaribu kuitisha *memorandum* hapa Bungeni na kupiga kura, tutaona kwamba kwa Waheshimiwa Wabunge wengi wana matatizo na Ofisi za Wakurugenzi Watendaji. Siyo kwa sababu wanawachukia watu fulani fulani, hapana, bali ni kwa sababu kuna matumizi mabaya, ubadhirifu wa fedha za Wananchi, tatizo ni hilo. (*Makofi*)

Nashindwa kuelewa ni kwa nini Wizara husika inashindwa kushughulikia na kutatua tatizo hili. Sielewi kwa nini, sielewi kwa nini hata kidogo! Siwezi kusema kwamba wanakula pamoja, wala sisemi kwamba kuna kulindana au labda ni urasimu wa Serikali, lakini tatizo lipo, Wakurugenzi Watendaji wamekuwa ni Miunguwatu na ni

wabadhirifu wakubwa. Lakini huyu Mungu anayekuwa mbadhirifu sielewi na ndiyo maana nasema ni Miungu siyo Mungu, ni Miungu isiyokuwepo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nitoe tu mfano mdogo wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro. Nimejaribu kupitia *Hansard* kuanzia mwaka 2001, nilichozungumza kuhusu Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Ngorongoro masuala haya ya ubadhirifu na hatimaye nimemalizia kwa kusema hivi, naomba kunukuu: “Naomba kutoa ombi kwa Waziri mwenye dhamana hiyo kuunda Tume kutoka Wizarani kwenda kukagua upya hesabu za Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2002 nikazungumzia tatizo hilo hilo kwenye Bunge lako Tukufu na nimechukua *Hansard* kujaribu kuangalia nilichosema. Nimezungumzia matatizo hayo hayo ya ubadhirifu wa mali ya Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro na nikaomba kwa mara ya pili: “Wizara husika, tafadhali tuma Tume pale kujaribu kuthibitisha au kukanusha hayo ninayoyasema mimi pamoja na Madiwani.” Nikaomba hivyo hivyo. Kana kwamba haitoshi, nikaenda kwa Mheshimiwa Waziri, nikaenda kwa Katibu Mkuu tukafikisha ombi hilo hilo. *RC* yupo hapa na yeye tumemwomba akaahidi, lakini hakuna lililotendeka!

Aah, kama haiwezekani au labda niseme hivi, juzi niliuliza swali Wizara ya Mambo ya Ndani kuhusu gari la Polisi Kituo cha Kakesio. Limeenda matengenezo miaka mitano halirudi Wilayani Ngorongoro, Kituo cha Kakesio, nikaambiwa, limetengenezwa likaenda Makuyuni Monduli. Kumbe limetengenezwa limeenda Monduli, lakini haliwezi kwenda Kakesio Ngorongoro, kwa nini? Leo hiyo Tume tunayoiomba Wananchi wa Ngorongoro pamoja na Madiwani inaenda kila mahali huko nchini, lakini haiendi Ngorongoro, kuna nini huko? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge, huyo ndiyo alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa jioni hii. Nina tangazo moja tu linatoka kwa *Chief Whip*, Mheshimiwa William Lukuvi. Kulikuwa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wamepata matatizo ya kubadilisha namba za magari, kwa hiyo, wakaomba utaratibu ungewekwa hapa ili wapate urahisi wa kupeleka kumbukumbu na magari yao yabadilishwe namba. Sasa anawatangazia kwamba huduma hiyo sasa iko hapa, wafanyakazi wa *TRA* wako Chumba namba 9 hapa kwenye jengo la Bunge. Kwa hiyo, wale ambao wangependa kubadilisha namba basi huduma hiyo iko Chumba namba 9.

Baada ya tangazo hilo, sasa nasitisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 1.42 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumanne, tarehe 22 Juni, 2004 saa tatu asubuhi*)